ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Saba – Tarehe 6 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuita Mhe. Waziri ili aweze kuja kutusomea bajeti yake, kwanza tuna wageni hapa ambao vile vile wametufikia hapa siku ya leo. Na wageni hawa ni wageni wa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Tunae Mhe. Abass Kombo Khamis Diwani wa Mtoni naomba asimame, Mhe. Haji Abrahman Shaame, Sheha wa Mtoni, tunae Mhe. Yussuf Ali Mussa Mwenyekiti Jimbo la Mtoni *CUF*, lakini pia tuna Mhe. Kitwana Juma Kondo, Katibu wa Jimbo la Mtoni *CUF* na tunae Mhe. Hassan Masoud Hassan, Sheha wa Shehia ya Mtopepo na Mhe. Ame Salum Juma Sheha wa Mtoni. Majina yao kwa mujibu wa hizi karatasi nilizoletewa wote ni Waheshimiwa hao. Ahsante tuendelee.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Waziri wA Biashara, Viwanda na Masoko: *Audhubillah minashaitwani rajjim, Bismillah Rahmani Rahiim. Alhamdulillah Rabil-alamin Waswalatu Wasalamu Alarasulillah Swalallahu Alaihi Wasallam.* Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika ukumbi huu hii leo tukiwa wazima wa afya njema. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa na kwa michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Na pia kwa ushauri na maelekezo yenu kwa utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Kipenzi chetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na upendo uliopelekea kuwepo amani na utulivu na kuwafanya wananchi wa Zanzibar kuweza kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi, biashara na uwekezaji bila ya bughdha. Aidha, napenda kumpongeza pia kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatumikia wananchi kwa usawa. Kadhalika, nachukua fursa hii kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad na Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zao za dhati wanazozichukua za kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu Naibu Waziri wangu Mheshimiwa, Thuwaibah Edington Kissasi, Nd. Julian Banzi Raphael – Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Nd. Rashid Ali Salim pamoja na Wakurugenzi wote, Meneja wa *ZSTC* na *MTC* pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia. Hakika bila ya msaada wao ningeshindwa kufanya kazi zangu ipasavyo, na nawaomba wazidishe mashirikiano yao kwangu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu kwa mafanikio makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, matayarisho ya bajeti hii yamezingatia misingi na ala kuu za kusimamia Uchumi na maendeleo ya nchi kama hivi ifuatavyo:-

(i) Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020;
(ii) Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar (MKUZA);
(iii) Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi;
(iv) Mpango Kazi (*Strategic Plan*) wa Wizara 2012 – 2015;
(v) Miongozo ya Kisera inayosimamiwa na wizara.
(vi) Ukomo wa rasilimali uliowekwa kwa wizara

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mazingatio ya hapo juu katika utayarishaji wa mapendekezo haya ya bajeti ya wizara, matukio mbali mbali yaliyojitokeza ulimwenguni na ambayo yamekuwa na athari za moja kwa moja katika mwenendo wa biashara duniani pia yalizingatiwa. Mazingatio hayo ni kama vile mwenendo wa uwekezaji duniani, biashara, fedha na pia machafuko ya kisiasa katika maeneo ambayo ni mlango wa biashara kwa bidhaa zinazoingia hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya bajeti hii yamepitia na kuzingatiwa katika hatua na ngazi mbali mbali muhimu na hususan Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo. Naomba kutanguliza shukurani zangu kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa kuchambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara kuikubali na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu. Baadhi ya maeneo na maelezo ya mapendekezo ya bajeti hii, Mhe. Mwenyekiti, yamegusiwa kwa muhtasari katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya kuwasilisha Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ambayo tayari imezingatiwa na kuidhinishwa na Baraza lako tukufu.

Hivyo, katika hotuba hii, Mhe. Mwenyekiti, nitafanya mapitio ya jumla ya hali ya biashara ulimwenguni na jinsi mwenendo huo wa biashara ulivyoathiri mwendo wa biashara wa Zanzibar. Kadhalika nitafanya mapitio kuhusu hali ya maendeleo ya Viwanda, utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka 2011/2012, mwenendo wa mashirika ya serikali yaliyochini ya wizara, kubainisha changamoto mbali mbali na hatimae kubainisha malengo kwa mwaka 2012/2013 na sura ya bajeti ya Wizara kwa kipindi hicho.

MWENENDO WA BIASHARA

Hali ya biashara ulimwenguni:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011 mwenendo wa uchumi na biashara duniani uliendelea kuwa wa kuyumba licha ya juhudi kubwa za kuufufua kutokana na athari za kuanguka kwa masoko ya fedha na hisa, athari za madeni kwa baadhi ya nchi zilizomo katika ukanda wa sarafu ya '*Euro'* pamoja na machafuko ya kisiasa yanayoendelea kuzikumba nchi za mashariki ya kati. Hali hiyo imeendelea kuathiri biashara duniani ambayo mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa dunia (*World Merchandise Trade Percentage of GDP)* ulipungua kutoka asilimia 53.2 mwaka 2008 na kufikia asilimia 48.2 mwaka 2011 kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 1** hapo chini.

Jadweli Nam. 1:

Mchango wa Biashara katika Uchumi wa Dunia 2008 – 2011:

Mwaka	**2008**	**2009**	**2010**	**2011**	
Asilimia	53.2	43.4	47.9	48.2	

Chanzo: Benki ya Dunia

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji bidhaa kwa mwaka 2011, nchi za Ulaya zimeendelea kuongoza kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 6,601 bilioni sawa na asilimia 37 ya usafirishaji wote wa bidhaa duniani (*World Total Exports)*. Kundi la nchi za Asia linafuatia kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 5,534 bilioni sawa na asilimia 31 ya usafirishaji wote. Marekani ya Kaskazini ilikuwa ni nchi ya tatu kwa kusafirisha bidhaa zenye thamni ya *USD* 2,283 bilioni sawa na asilimia 13 ya usafirishaji wote. Nchi za Afrika kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2011-2012, zimeendelea kuwa na sehemu ndogo sana ya usafirishaji huo ambapo ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 597 bilioni za usafirishaji wote sawa na asilimia 3 tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uagiziaji, nchi za Ulaya ziliagiza bidhaa zenye thamani ya *USD* 6,854 bilioni sawa na asilimia 38 ya uagiziaji wote duniani (*World Imports*) zikifuatiwa na nchi za Asia zilizoagiza bidhaa zenye thamani ya *USD* 5,568 bilioni sawa na asilimia 31. Marekani ya Kaskazini iliagiza bidhaa zenye thamani ya *USD* 3,090 bilioni sawa na asilimia 17. Uagiziaji kwa kundi la nchi za Afrika ulikuwa ni *USD* 556 bilioni sawa na asilimia 3 tu ya uagiziaji wote duniani. Mwenendo wa uagiziaji huo ni kama unavyoonekana katika **Jadweli Nam. 2** hapa chini.

Jadweli Nam. 2:

Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2011 (*USD* bilioni):

Kanda	**Usafirishaji**	**Asilimia**	**Uagiziaji**	**Asilimia**
Ulaya	6,601	37	6,854	38
Asia	5,534	31	5,568	31
Marekani/	2,283	13	3,090	17

kaskazini				
Mashariki ya Kati	1,228	7	665	4
Jumuiya ya Madola	788	4	540	3
Marekani/Kusini	749	4	727	4
Afrika	597	3	556	3
Jumla	**17,780**	**100**	**18,000**	**100**

IMF/Word Bank na WTO.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011 dunia iliendelea kushuhudia uwepo wa viwango vikubwa vya kasi ya mfumuko wa bei ambavyo vimechochewa zaidi na mwenendo wa kuyumba kwa bei za chakula na zisizo za chakula hasa bei za nishati. Katika kipindi hicho kiwango cha mfumko wa bei kwa nchi zilizoendea kiliongezeka kutoka asilimia 1.6 mwaka 2010 na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kiwango cha mfumko wa bei umefikia asilimia 8.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.4 mwaka 2010. Kwa nchi za Afrika Mashariki wastani wa kasi ya mfumko wa bei ulifikia asilimia 9.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2010.

Hali ya Kibiashara Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, na kama ilivyoarifiwa katika bajeti ya Serikali usafirishaji bidhaa nje ulifikia Shilingi 61,261.4 milioni mwaka 2011 kutoka Shilingi 17,906.7 milioni mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 242. Usafirishaji wa kiwango hicho cha bidhaa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na usafirishaji wa Zao la Karafuu (Shilingi. 50,036 milioni) na mwani wenye thamani ya Shilingi 6,404 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya Shilingi 164,187.1 milioni kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na uagiziaji wa Shilingi 129,139.8 milioni mwaka 2010.

Ingawa kwa matokeo hayo ya kibiashara bado tunakabiliwa na nakisi ya urari wa biashara, Mhe. Mwenyekiti, mwenendo huo umeonesha matumaini ya kuimarika kwa urari wa biashara kwa kupunguza nakisi yake kwa asilimia 7.5. **Jadweli Nam. 3** hapa chini linatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli Nam. 3:

<u>Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2007 – 2011):</u>

TZS. (Milioni)

MAELEZO	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**	**2011**	**%**
Usafirishaji	21,177.7	30,189.2	29,744.5	17,906.7	61,261.4	242
Uagiziaji	107,689.0	93,439.6	120,882.0	129,136.8	164,187.1	27
Urari wa Biashara	**-86,512.8**	**-63,250.4**	**-91,137.5**	**-111,230.1**	**-102,925.7**	**7.5**

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Usafirishaji

Bidhaa Kwenda na Kutoka Tanzania Bara (Inter-state Trade Balance):

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji bidhaa kwenda Tanzania Bara, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya Shilingi 71,396.8 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Shilingi 2,203.8 milioni mwaka 2010.

Aidha, kwa upande wa Uagiziaji bidhaa kutoka Tanzania Bara, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya Shilingi 74,738.3 milioni kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na Uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya 23,268.7 milioni kwa mwaka 2010.

Kutokana na mwenendo huo Mhe. Mwenyekiti, urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara uliimarika baada ya nakisi yake kupungua kutoka asilimia 90.5 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 4.5 mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012 niligusia suala la ufuatiliaji wa malalamiko ya wafanyabiashara katika bandari ya Dar es Salaam kulipishwa kodi mara mbili. Suala hili limejadiliwa na kuchukuliwa hatua za kisera katika maamuzi ya vikao vilivyokutana kutatua kero za Muungano. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, kulingana na takwimu zilizopo, hali ya biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara imeimarika kama nilivyokwisha eleza hapo juu, ingawa malalamiko bado yanaendelea. Ili kuweza kushughulikia vyema malalamiko hayo, wizara inawaomba wafanyabiashara kuwasilisha wizarani nyaraka za ulipishwaji kodi mara mbili ilikuweza kujenga hoja za majadiliano.

Mhe. Mwenyekiti, usafirishaji bidhaa kupitia utaratibu wa Bandari Huru (Free Port) nao umeongezeka kwa mwaka 2011 ambapo thamani ya usafirishaji huo ilifikia Shilingi 1,307.6 milioni ikilinganishwa na Shilingi 1,099.7 milioni mwaka 2010. Hili ni ongezeko la asilimia 19 kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam 4.** hapa chini.

Jadweli Nam. 4:

Usafirishaji kwenda na kutoka Tanzania Bara na kupitia Bandari Huru:
TZS. (Milioni)

Mwaka	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**	**2011**
Kuja Zanzibar	27,608.5	25,926.5	19,651.0	23,268.7	74,738.3
Kwenda Tanzania	968.2	1,479.6	1,341.1	2,203.8	71,396.8

Bara					
Urari wa Biashara	-26,640.3	-24,446.9	-28,309.9	-21,064.9	-3,341.1
Uhaulishaji	6,188.6	1,459.1	2,915.5	1,099.7	1,307.6

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika Bajeti ya Serikali kwamba kwa upande wa Zanzibar, wastani wa mfumko wa bei ulifikia asilimia 14.7 kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2010. Wastani mkubwa wa viwango vya mfumko wa bei kwa Zanzibar, unachangiwa pamoja na mambo mengine, uwepo wa hali ya ushindani mdogo wa ndani katika masoko ya bidhaa na huduma mbali mbali ingawa ni kweli kuwa uagiziaji kutoka masoko ya nje unachangia katika kuyumbisha masoko ya ndani. Bidhaa za mafuta nazo zimeendelea kuwa na mchango katika kupandisha kasi ya mfumko wa bei na hivyo kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wetu.

Mwenendo wa Bei za chakula:

(i) **Bei katika Masoko ya Dunia:**

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa bei za chakula katika masoko ya dunia ziliendelea kuyumba na hivyo kuwa na athari za moja kwa moja katika bei za soko la ndani ya bidhaa hizo. Kwa jumla, mwenendo wa bei kwa bidhaa za mchele, ungangano na sukari katika masoko ya dunia kwa mwaka 2011 ulikuwa kama unavyoonekana katika **Jadweli Nam 5** hapa chini.

Jadweli Nam.5:

<u>Wastani wa Bei za chakula muhimu katika Soko la Dunia 2011:</u>

(USD/MT)

Bidhaa	**2010**	**2011**	**Ongezeko (%)**
Mchele	570	572	0.4
Sukari	830	860	3.6
Unga Ngano	490	525	7.0
Ongezeko la			**3.7**

Jumla (%)				

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Katika jadweli hilo Mhe. Mwenyekiti, itabainika kuwa bei za chakula katika masoko ya dunia ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 3.7 kati ya mwaka 2010 na mwaka 2011 na hivyo kusababisha msukumo wa jumla wa upandaji wa bei katika soko la ndani kwa kiwango hicho hicho.

(ii) **Bei katika Soko la Zanzibar:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa bei za bidhaa hizo muhimu katika soko la ndani zilikuwa za utulivu ikilinganishwa na bei za bidhaa hizo kwa jirani zetu Kenya, Uganda na hata Tanzania Bara licha ya kuwepo kwa ongezeko la jumla la bei za bidhaa hizo katika masoko ya dunia. Nililiarifu Baraza lako tukufu mwaka jana kuwa Serikali imeanzisha utaratibu mpya wa kusimamia bei za bidhaa hizo kwa kuwashirikisha wafanyabiashara wenyewe. Kwa kiasi kikubwa utaratibu huu umesaidia kuweka nidhamu katika upangaji bei za bidhaa hizo ingawa bado unakabiliwa na changamoto nyingi za ukiukwaji wa makubaliano kwa baadhi ya nyakati. Kadhalika, nafuu ya kikodi inayotolewa na Serikali kwa bidhaa hizo imesaidia kuzifanya bei za bidhaa hizo kuwa chini na hivyo kuwawezesha wananchi wengi kumudu ununuzi wa bidhaa hizo.

Kwa jumla, Mhe. Mwenyekiti, wastani wa bei za reja reja za bidhaa hizo kwa mwaka 2011 ni kama zinavyoonekana katika **Jadweli Nam 6** hapo chini:

Jadweli Nam 6:
Wastani wa Bei za Reja Reja za Chakula muhimu katika soko la Zanzibar: (TZS/Kilo)

Bidhaa	**2010**	**2011**	**Ongezeko (%)**
Mchele	1,075	1,200	11.6
Sukari	1,450	1,750	20.7
Unga Ngano	1,000	1,125	12.5
Ongezeko la Jumla (%)			**14.9**

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuchunguza hali ya mwenendo wa bei za chakula muhimu katika masoko ya dunia na mwenendo wake katika soko la Zanzibar yanajitokeza mambo makubwa yafuatayo:-

(i) Kutokana na hatua za serikali ya kupunguza thamani ya kutozea ushuru na kiwango chake, serikali imeweza kudhibiti athari za ongezeko la jumla la bei kwa bidhaa hizo katika masoko ya dunia kuweza kuathiri moja kwa moja bei za bidhaa hizo katika soko la ndani.

(ii) Kutokana na kuyumba kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani na hasa dola ya Marekani, mahitaji makubwa ya bidhaa hizo na uzalishaji mdogo wa ndani ulisababisha wastani wa mwenendo wa jumla wa bei hizo kupanda kwa kiwango kikubwa.

Hali hii haishangazi kwa kuwepo kwa kiwango kikubwa cha mfumko wa bei kama ilivyoelezwa hapo awali. Hivyo, mwenendo wa bei za chakula utaendelea kuwa na athari kubwa katika kiwango cha mfumko wa bei hapa Zanzibar.

Uhamishaji Bidhaa za Chakula Muhimu kwenda Nje ya Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi Februari – Juni, 2012 kumejitokeza wimbi kubwa la kusafirisha bidhaa muhimu za chakula hasa mchele na sukari kwenda nje ya Zanzibar. Serikali ilifanya uchunguzi wa sababu za wimbi hilo na kubainisha kuwa bei za bidhaa hizo kwa soko la Dar es Salaam zilikuwa ni kubwa na hivyo kuwa kivutio cha kusafirisha bidhaa hizo. Ili kukabiliana na wimbi hilo, serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

a. Kuviomba vyombo vya ulinzi kuzuia usafirishaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya Zanzibar;

b. Kuweka utaratibu mpya wa kuhaulisha bidhaa hizo kwenda Pemba; na

c. Kutumia Sheria zilizopo kushughulikia kesi za waliokamatwa na uhamishaji wa bidhaa hizo nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti unaonesha kwamba kumekuwa na kivutio kikubwa cha bei katika masoko ya nje ya Zanzibar kutokana na tofauti ya viwango vya ushuru kwa bidhaa hizo kati ya Zanzibar na masoko ya nje ya Zanzibar. Tofauti hiyo inatokana na sera ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kumudu bei ya kununulia bidhaa hizo kwa kuweka viwango vidogo vya kuthaminia na kutozea ushuru kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Viwango vya kuthaminia ni *USD* 160 kwa tani ya mchele badala ya bei ya kununulia nje ya wastani wa *USD* 570 kwa tani na kiwango cha kodi cha asilimia 12.5 kwa bidhaa hiyo badala ya kiwango cha asilimia 75 (viwango vya *EAC*). **Jadweli Nam. 7** hapa chini linatoa mchanganuo wa nafuu inayotolewa na serikali katika bidhaa hizo kwa madhumuni niliyoyaeleza hapo awali.

Jadweli Nam.7:

Viwango vya Unafuu wa Thamani, Ushuru na Kodi kwa bidhaa muhimu za chakula:

Bidhaa	**Gharama za Uagiziaji**	**Kodi za ndani**	**Unafuu uliotolewa**

	Wastani wa Bei ya Dunia (USD)	Kiwango cha Ushuru (%)	VAT (%)	Ushuru wa Biashara (%)	Ushuru wa Stempu (%)	Thamani (USD)	Kiwango cha Ushuru (%)
Mchele	570	75	0	2	1.5	160	12.5
Sukari	860	100	18	2	1.5	200	12.5
Ungangano	525	35	0	2	1.5	160	12.5

Chanzo: (i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko
(ii) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Unafuu unaooneshwa katika jadweli la hapo juu ndio unaotofautisha viwango vya bei za bidhaa zilizoainishwa kwa upande wa Zanzibar na vile vinavyoonekana katika masoko ya chakula kwa majirani zetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kuwa na usalama na uhakika wa chakula hapa Zanzibar pamoja na kuzuia upandaji bei kiholela kwa bidhaa hizo, serikali ililazimika kuzuia utoaji wa chakula kwa kutumia Sheria Nam 5 ya mwaka 1986 inayozuia uhamishaji wa bidhaa muhimu za chakula kwenda nje ya Zanzibar. Kadhalika, katika utekelezaji wa zuio hilo, Serikali ilikuwa inatumia Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) Namba 4 ya mwaka 1998 na hasa kifungu namba 48 cha *"Compounding of an offence"* kwa kurejesha kiasi cha ushuru kilichosamehewa awali na kumrudishia mfanyabiashara aliekamatwa bidhaa yake. Tokea kuanza kwa '*operation'* hiyo Mhe. Mwenyekiti, jumla ya paketi 1,722 za mchele sawa na tani 86.1 na paketi 1,208 za sukari sawa na tani 60.4 zilikamatwa. Fedha iliyokusanywa kwa ajili hiyo ni Shilingi 33.7 milioni hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012.

(iii) **Urahisishaji Biashara *(Trade Facilitation)***

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya maeneo muhimu katika ukuzaji biashara ni urahisishaji wa ufanyaji biashara hasa katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege, taratibu za kiforodha, miundo mbinu mbali mbali ya maji, umeme, barabara na taratibu za usajili biashara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2007 – 2011) Zanzibar imeshuhudia kukua kwa biashara inayojitokeza katika ongezeko la idadi ya makontena yaliyoingizwa katika kipindi hicho. Idadi hiyo iliongezeka kutoka makontena 6,615 sawa na makontena 550 kwa mwezi mwaka 2007 hadi kufikia makontena 19,773 sawa na makontena 1,648 kwa mwezi, mwaka 2011 kama inavyoonesha katika **Jadweli Nam 8** la hapa chini.

Jadweli Nam 8:
Uingizwaji na Utoaji Makontena:

Mwaka	2007	2008	2009	2010	2011
Discharged (Import)	6,615	8,693	12,576	15,072	19,773
Loaded (Export)	6,531	8,743	12,291	14,937	19,522

Chanzo: Shirika la Bandari, Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni wizara

ilipokea malalamiko kutoka kwa Wafanyabiashara wa Zanzibar kuhusu ucheleweshaji mkubwa wa kupata bidhaa zao na kwa wenye Meli kuzipeleka bidhaa hizo Dar-es-Salaam kutokana na mrundikano wa makontena katika bandari ya Zanzibar. Wizara imeliwasilisha suala hili kwa Uongozi wa Shirika la Bandari ili kuandaa Mpango wa Dharura wa kurahisisha utoaji wa makontena hayo na biashara kwa jumla ikiwemo utumiaji wa eneo la Bwawani kwa muda mfupi.

HALI YA VIWANDA

Maendeleo ya Viwanda:

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya mwaka 2011/2012 kuwa Miongoni mwa malengo makubwa ya serikali katika juhudi zake za kuwavutia wawekezaji ili kuanzisha viwanda hapa nchini ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje, kutumia malighafi za hapa nchini, kuongeza thamani na usarifu wa bidhaa, kuongeza ajira kwa wananchi pamoja na kuongeza mapato ya serikali na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu na kuimarisha juhudi zetu za kupunguza umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, kimuundo, Sekta ya viwanda inaundwa na maeneo madogo (sub sectors) manne kama ifuatavyo:-

(i) Uchimbaji Madini na Mawe (*Mining and Quarying*);
(ii) Maji, Umeme na Gesi (*Water, Electricity and Gas*);
(iii) Usarifu wa Bidhaa (*Manufacturing*); na
(iv) Ujenzi (*Contruction*).

Kwa ujumla sekta hiyo ilichangia asilimia 12.5 ya Pato la Taifa katika kipindi cha mwaka 2009 – 2011.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ndogo ya Usarifu wa Bidhaa (*Manufacturing*) peke yake, mchango wake ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.1 kwa kipindi cha miaka 2010-2011, ambapo thamani ya mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa kwa bei za sasa (*current price*) umeongezeka na kufikia Shilingi 49.9 bilioni mwaka 2011 kutoka Shilingi 39.5 bilioni mwaka 2010**.** Hali ya uzalishaji viwandani kwa ujumla imeimarika kidogo katika mwaka wa 2011 ikilinganishwa na mwaka 2010 kwa viwanda vilivyopo, ingawa bado viwango vilivyofikiwa vinatoa mchango usioridhisha katika pato na uchumi wa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, ongezeko hilo la thamani limetokana na kupanuka kwa uzalishaji wa baadhi ya viwanda, vikiwemo kiwanda cha usagishaji nafaka, viwanda vya maji, soda na juisi pamoja na viwanda vyengine vidogo vidogo vya usarifu wa bidhaa, utengezaji wa samani na bidhaa za mikono (*hand craft*), uzalishaji wa matofali na kokoto kutokana na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa **u**safirishaji nje ya nchi kwa bidhaa zilizozalishwa na viwanda vinavyofanyakazi katika Maeneo huru ya Kiuchumi (*EPZ*) ulifika thamani ya *USD*. 943,527.20

kwa mwaka 2011 kutoka *USD* 835,524 za mwaka 2010. Bidhaa hizo ni pamoja na kanda za sauti kwa ajili ya redio na *video*, *CD* na mitumba zinazopelekwa katika nchi za Kenya, Uganda, Malawi, *DRC*, Zambia, Ethiopia, na Rwanda

Mheshimiwa Spika. Katika kipindi cha 2011/2012, jumla ya miradi tisa ya viwanda yenye jumla ya mitaji ya *USD* 7.484 milioni iliidhinishwa na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*). Kati ya miradi hiyo imo mine (4) ya kuzalisha maji ya chupa na vinywaji baridi, sabuni na vipodozi (1), kiwanda cha rangi (1), ushoni (1) na miwili (2) ya kusarifu vyakula. Baadhi ya miradi hiyo imeshaanza hatua za ujenzi, na tutaendelea kufuatilia maendeleo ya miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012 kwamba pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa za kuhuisha sekta ya viwanda hasa usarifu wa bidhaa (*manufacturing*), bado uwekezaji katika Sekta hii haujawa na kasi ya kutosha. Kudorora kwa uwekezaji katika Sekta hii kunatokana na baadhi ya sababu kuu zifuatazo:

- Ukosefu wa maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nje ya utaratibu wa *EPZ.*

- Ukosefu wa miundo mbinu ya umeme, maji, barabara katika maeneo ya *EPZ* ya Fumba na Micheweni na gharama kubwa za nishati nchini.

- Huduma dhaifu za bandari ambazo zinasababisha meli kubwa za kuleta shehena kushindwa kuja Zanzibar.

- Kuondoshwa kwa vikomo vya uingizaji bidhaa (*Import quotas*) katika soko la Marekani na Ulaya, jambo ambalo lilitoa fursa kwa wazalishaji wa nchi za Ghuba na Asia kuweka viwanda katika nchi zao na kusafirisha bidhaa katika masoko hayo bila ya ukomo. Hali hii imeathiri baadhi ya nchi za Kiafrika kama Botswana kwa kuondokewa na wawekezaji kutoka China.

- Uwezo mdogo wa wafanyakazi (*productivity*) unaosababisha baadhi ya wakati miradi kushindwa kukidhi mahitaji ya wateja (*Orders*):

- Ukosefu wa ubora wa viwango na namba ya usafirishaji bidhaa (*export code*) hasa kwa bidhaa za chakula zinazopelekwa nchi za Ulaya.

- Ukosefu wa mitaji kwa wazalishaji, ikiwemo kukosekana kwa benki ya uwekezaji katika sekta ya viwanda

Sababu hizo, Mheshimiwa Spika bado zinaendelea kuathiri mwenendo wa uwekezaji katika sekta ya usarifu wa bidhaa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko (Anaendelea) Mhe. Mwenyekiti**,** katika juhudi za kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya viwanda, Serikali imechukua hatua ya kufanya utafiti kubainisha uwezekano wa kuigeuza Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi (Special Economic Zone- SEZ). Naomba kutoa taarifa kuwa utafiti huo umekamilika

na kubainisha maeneo ambayo yataweza kukuza uzalishaji katika sekta ya viwanda na kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Eneo Huru la usafirishaji wa mazao ya kilimo (Development of Agricultural Export Zones (AEZ))

(ii) Usarifu wa bidhaa kwa ajili ya usafirishaji (Development of Agro-Processing-cum-Light Manufacturing Zone);

(iii) Eneo la usafirishaji wa bidhaa katika bandari (Transshipment Container-cum-Trading Hub);

(iv) Eneo Huru la Biashara (Duty-Free Zones).

Mhe. Mwenyekiti**,** utekelezaji wa Mkakati huo wa SEZ utakwenda sambamba na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa za uendelezaji wa miundombinu ya bandari, uwanja wa ndege, pamoja na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uendelezaji wa mazao ya kilimo na viwanda hatua ambazo zitakuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji hasa katika kuendeleza sekta ya viwanda na kukuza biashara Zanzibar.

I. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2011/2012:

Mhe. Mwenyekiti**,** baada ya kutoa maelezo ya jumla ya hali ya biashara pamoja na maendeleo ya viwanda kwa mwaka 2011, naomba sasa kuelezea utekeleaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011 – 2012.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 2,662 milioni. Kati ya fedha hizo TZS. 1,462.0 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS 300.0 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo na TZS. 900.0 milioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara, kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam.9 hapa chini**.

Jadweli Namba 9:
Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2011-2012:

A: **Matumizi ya Kawaida:**		**TZS. (Milioni)**
(i)	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	556.2
(ii)	Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko	225.4

(iii)	Idara ya Viwanda na Ujasiriamali	181.5	
(iv)	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	230.6	
(v)	Ofisi Kuu – Pemba	238.4	
	Jumla Ndogo:		**1,462.0**

B: **Matumizi ya Maendeleo:**

(i)	Mapitio ya Sheria za Biashara	50.0	
(ii)	Kuendeleza Viwanda na Wafanyabiashara wadogo wadogo	200.0	
(iii)	Utafiti wa uanzishaji Eneo Tengefu la Uchumi	50.0	
	Jumla Ndogo:		**300.0**

C: **Ruzuku:**

(i)	Mamlaka ya Vipimo	200.0	
(ii)	Mamlaka ya Ushindani	200.0	
(iii)	Taasisi ya Viwango	250.0	
(iv)	Baraza la Biashara	250.0	
	Jumla Ndogo:		**900.0**
	Jumla Kubwa:		**2,662.0**

Mwenyekiti**,** Mhe. Kutokana na fungu la Wizara yangu lilipatiwa jumla ya TZS. 255.0 kwa nyongeza ya kugharimia ajili ya marekebisho ya matumizi ya yaliyofanywa mishahara na Serikali. jumla ya fungu nyongeza hiyo iliongezeka la Wizara kutoka TZS. 2,662.0 milioni hadi kufikia TZS. 2,917.0 milioni. Hadi kufikia mwezi Juni, 2012 Wizara yangu iliingiziwa jumla ya TZS. 2,626.0 milioni sawa na asilimia 90.0 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TZS. 1,468.1 milioni zilitumika kwa kazi za kawaida, TZS. 299.0 milioni kwa kazi za maendeleo na TZS. 859.0 milioni matumizi ya ruzuku. Upatikanaji huo wa fedha na matumizi yake kwa kila Idara unaonekana katika **Jadweli Nam. 10** hapa chini.

Jadweli Nam 10:

Upatikanaji wa Fedha:

Vote Nam.	Idara	Makisio ya Bajeti 2011 – 2012 (TZS Mil)	Bajeti baada ya ongezeko (TZS Mil)	Kilichoingizwa Julai 2011-Juni2012 (TZS Mil)	Asilimia ya Makisio ya mwaka
KAZI ZA KAWAIDA					
03:	Afisi Kuu Pemba	238.4	271.4	267.2	98.4
04:	Mipango, Sera na Utafiti	230.6	257.0	204.6	79.6
05:	Maendeleo ya Viwanda	181.5	207.8	137.4	66.1
06:	Biashara na Masoko	255.4	283.6	255.5	90.1
07:	Utumishi na Uendeshaji	556.2	697.3	603.4	86.5
	Jumla ndogo	**1,462.0**	**1,717.0**	**1,468.07**	
KAZI ZA MAENDELEO					
	Mapitio ya sheria zinazoendana na biashara	50.0	50.0	50.0	100
	Utafiti wa SEZ	50.0	50.0	50.0	100
	Mpango wa kuendeleza Viwanda vidogo vidogo (SMEs)	200.0	200.0	199.0	99.5
	Jumla ndogo	**300.0**	300.0	299.0	
RUZUKU					
	Baraza la Biashara	200.0	200.0	197.2	98.6
	Taasisi ya Ushindani	250.0	250.0	250.0	100
	Taasisi ya Viwango Zanzibar	250.0	250.0	211.8	84.7
	Taasisi ya Vipimo	200.0	200.0	200.0	100
	Jumla ndogo:	**900.0**	**0**	**859.00**	
	Jumla Kuu:	**2,662.0**	**2,917.0**	**2,626.0**	**90.0**

Utekelezaji wa Malengo:

Mhe. Mwenyekiti**,** Kwa mwaka wa fedha wa 2011-2012 Wizara ilijipangia kutekeleza malengo kumi na saba (17) kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Nam 1.

Hata hivyo, kwa madhumuni ya kurahisisha ufafanuzi wa utekelezaji wa malengo hayo kulingana na muundo wa Wizara unaooneshwa katika kiambatanisho Nam. 2, naomba kutoa maelezo yake kiidara kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa Idara ya Mipango Sera na Utafiti iliweza kutekeleza malengo yaliyopangwa kama ifuatavyyo:

Kuendeleza Eneo la Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya biashara:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011-2012, Wizara ilipanga kutayarisha michoro ya matumizi ya ardhi (Land Use Plan), michoro ya kiufundi (*Structural and Architectural Design*) pamoja na kutayarisha gharama za mradi (*Bill of* Quantity), kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja huo wa maonesho. Mradi huu ulitengewa jumla ya TZS 780.0 milioni kupitia udhamini wa miradi ya BEST na UNDAP inayofadhiliwa na Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, utekelezaji wa lengo hili haukufanyika kwa sababu fedha zilizotarajiwa kutoka kwa wafadhili hazikupatikana. Wizara kwa upande wake iliandaa zabuni kwa ajili kutafuta mshauri mwelekezi atakaeandaa michoro ya usanifu na ufundi kwa ajili ya mradi huo.

Kuigeuza Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi (SEZ):

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012, kuwa Wizara itafanya utafiti kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi makini kuhusu mkakati wake wa kuimarisha uchumi na uendelezaji viwanda wenye lengo la kuchangamsha biashara. Naomba kuchukua fursa hii Mheshimiwa Spika, kuliarifu Baraza lako kuwa utafiti huo umekamilika na taarifa yake imeshawasilishwa Wizarani na inaendelea kuzingatiwa na Kamati maalum ya Makatibu Wakuu iliyoundwa kufuatilia suala hili na baadae kuwasilishwa Serikalini kwa mazingatio.

Uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa Nje (National Export Strategy –NES)

Mhe. Mwenyekiti, Ili kuimarisha usafirishaji wa bidhaa nje, Serikali imeanzisha mkakati maalum kwa ajili hiyo. Mkakati huo unaratibiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na unatekelezwa na Wizara mbali mbali na Sekta binafsi. Katika bajeti ya 2011/12 jumla ya TZS 51,453.3 milioni zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mkakati huu katika Wizara

hizo. Fedha zilizotengwa Mkakati huo katika maeneo yafuatayo:

	Sekta	TZs (milioni)
a.	Masuala Mtambuka na Kurahisisha mifumo ya ufanyaji biashara hasa katika kuimarisha (miundombinu ya viwanja vya ndege na bandari).	47,200.0
b.	Kuendeleza Sekta ya Viungo (Spice Sector Development).	0
c.	Kuendeleza Sekta ya Uvuvi.	795.2
d.	Kuendeleza Mazao ya Bahari (Mwani na Chumvi)	1,003.8
e.	Kuendeleza Sekta ya Matunda na Mboga mboga	1,769.7
f.	Kuendeleza Sekta ya Mifugo	81.7
g.	Kuendeleza Sekta na Utalii	129.8
h.	Kuendeleza Sekta ya usarifu wa Bidhaa	473.1
	Jumla	**51,453.3**

hizo kwa ajili ya zilielekezwa makubwa

Mhe. utekelezaji wa mkakati huu unaendelea tofauti. Hatua

Mwenyekiti**,** malengo ya umeanza na kwa viwango zifuatazo

zimechukuliwa katika utekelezaji wa malengo yake:-

(i) Uendelezaji wa miundo mbinu na hasa kuimarisha usafirishaji kwa ununuzi wa vifaa vya kupakia mizigo bandarini, ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege na uimarishaji barabara;

(ii) Utayarishaji wa Sera ya Uendelezaji wa Masoko ya bidhaa za Kilimo (Agricultural Marketing Policy), Uendelezaji wa Mazao ya Bahari (Marine Resource Policy) na Sera ya Mifugo;

(iii) Utayarishaji wa Mpango wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji ili kuongeza tija ya uzalishaji;

(iv) Utoaji mafunzo ya uzalishaji wa mazao ya mboga mboga; na

(v) Ushiriki wa Zanzibar katika Maonesho ya Kimataifa ya Utalii ambayo yameleta matumaini ya kuifungua Zanzibar katika ulimwengu wa Usafiri wa anga kwa kuwepo kwa uwezekano wa kuanzishwa kwa safari za moja kwa moja za baadhi ya mashirika ya ndege makubwa na kuvutia mikutano ya kimataifa ya wadau wa usafirishaji wa anga.

Pamoja na hatua hizo Mheshimiwa Spika, bado tumekabiliwa na kazi kubwa ya utekelezaji wa Mkakati huu ili kuongeza kiasi na thamani ya usafirishaji bidhaa nje kulingana na malengo ya Mkakati huo.

Mkakati wa kuongeza thamani ya Mauzo kwa Bidhaa zinazosafirishwa Nje kwa kutumia Tasnia ya Malibunifu (IP Value Capture Strategy na Branding):

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa miaka Zanzibar imekuwa ikisafirisha bidhaa mbali mbali kwa kuuzwa katika masoko ya kimataifa bila ya kumuelewa mtumiaji wa mwisho (final consumer) wa bidhaa zake. Kutokana na hali hiyo thamani ya bidhaa zake ziliendelea kuwa za kiwango cha chini na hivyo kukiacha kiwango kikubwa cha thamani ya bidhaa kwa mawakala na madalali wa kati. Utafiti uliofanywa hivi karibuni umeonesha kuwa Zanzibar pamoja na nchi nyingi zinazoendelea zinaambulia asilimia kati ya 3 hadi tano tu ya bei za bidhaa zake katika masoko ya dunia. Asilimia 95 ya bei ya bidhaa hizo huwafaidisha wafanyabiashara wa kati na mawakala.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuongeza thamani ya bidhaa za Zanzibar zinazouzwa katika masoko ya kimataifa na hasa mazao ya viungo, Serikali imeanza maandalizi ya Mkakati wa Kibiashara kwa kutumia tasnia ya malibunifu kwa ajili hiyo (Intellectual Property Value Capture Initiative and Branding). Katika maandalizi ya Mkakati huo ipo michakato (processes) miwili inayoendelea hivi sasa kama ifuatavyo:-

> **Kwanza,** upo mkakati wa kuifanyia utambulisho maalum (branding) karafuu peke yake. Katika hatua hii, Serikali inashirikiana na taasisi za kimataifa zinazohusika na usimamizi wa malibunifu ulimwenguni na biashara (World Intellectual Property Organization – WIPO) na Taasisi ya Kimataifa ya Biashara (International Trade Centre – ITC).
>
> **Pili,** Mhe. Mwenyekiti, upo Mkakati wa kibiashara wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazouzwa nje kwa kutumia mbinu hiyo hiyo na tasnia ya malibunifu kwa mazao mengine ya viungo. Katika maandalizi ya Mkakati huu, Serikali inashirikiana na Serikali ya Marekani kupitia Kampuni ya Light Years IP kwa lengo hilo hilo.
>
> Kazi za utekelezaji wa maandalizi hayo Mheshimiwa Spika, yameshaanza na yanaendelea vizuri. Hata hivyo ningependa kutanabahisha kuwa utekelezaji na matokeo ya kibiashara ya Mikakati hiyo hayawezi kuonekana katika kipindi cha muda mfupi. Utekelezaji wa Mkakati huu ni suala la muda mrefu na endelevu na itahitajika kufanya mageuzi makubwa katika taratibu zetu za uzalishaji, ubora wa bidhaa zenyewe, kiasi cha uzalishaji kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko n.k. Mambo yote haya yatachukua muda kuweza kuwa na tija ya moja kwa moja kwa mkulima.

Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu (Clove Development Fund):

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika bajeti iliyopita kwamba Serikali inakusudia kufanya maerekebisho ya Sheria ya Karafuu ya mwaka 1985 ili iendane na wakati pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kwa lengo la kuendeleza zao la karafuu. Rasimu ya Sheria ambayo itaanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu imekamilika baada ya kuwashirikisha wadau mbali mbali na iko tayari kwa kuzingatiwa na Serikali. Serikali inatarajia kuwasilisha Muswada wa Sheria kwa ajili hiyo katika Baraza lako tukufu katika kikao cha Mwezi Septemba 2012 ili kusomwa kwa mara ya kwanza.

Kuimarisha Mazingira ya Biashara:

(a) **Kufanya mapitio ya Sheria za Biashara**

Mhe. Mwenyekiti**,** miongoni mwa malengo ya Wizara ni kuimarisha mazingira mazuri ya biashara hapa Zanzibar. Eneo hili lilijumuisha utekelezaji wa hatua mbali mbali zilizolenga katika kukuza biashara kwa ujumla wake. Mapitio hayo yalilenga Sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya Biashara Nam. 4 ya Mwaka 1989;
(ii) Sheria ya Leseni Nam. 4 ya Mwaka 1983;
(iii) Sheria ya Mizani na Vipimo ya Nam. 4 ya Mwaka 1983; na
(iv) Sheria ya Kumlinda Mtumiaji Nam. 2 ya Mwaka 1995.

Naomba kutoa taarifa Mheshimiwa Spika, kuwa maandalizi yote ya msingi kuhusu mapitio na uandaaji wa rasimu za Sheria hizo yamekamilika na kwamba zitaanza kuzingatiwa na Serikali hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kama wajumbe wa Baraza lako tukufu watakavyokumbuka kuwa niliahidi kuwasilisha mbele ya Baraza hili mapendekezo ya miswada ya Sheria zilizotajwa hapo juu na kwamba tulianzisha vyombo vya kusimamia utekelezaji wa Sheria hizo, katika bajeti ya mwaka 2011-2012. Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa matarajio ya mageuzi makubwa ya mfumo wa utoaji leseni na kwamba mapitio ya mfumo wa sasa yalichukua muda mrefu zaidi kuliko ilivyotarajiwa, uwasilishaji wa miswada mengine ya Sheria ulionekana siyo busara kabla ya kuwa na mfumo wa Sheria mpya ya Leseni za biashara. Hivi sasa rasimu ya miswada wa Sheria ya mfumo wa Utoaji Leseni za kibiashara nchini iko tayari na kwamba uzingatiaji wa rasimu hiyo sasa unaendelea.

(b) **Tathmini ya Sera ya Biashara ya Zanzibar ya mwaka 2006**

Mhe. Mwenyekiti**,** katika utekelezaji wa lengo hili, Wizara ilifanya mapitio ya utekelzaji wa Sera hiyo na kubaini kuwa baadhi ya malengo yaliyowekwa katika Sera hiyo yametekelezwa. Malengo hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kutafiti uwezekano wa kuigeuza Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi;
ii. Kuanzisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar;
iii. Kuandaa Mkakati wa Usafirishaji bidhaa nje (Export Strategy);
iv. Kuimarisha Shirika la ZSTC na biashara ya Karafuu;
v. Kuimarisha mashirikiano ya kibiashara kimataifa na Kikanda;
vi. Kuimarisha Maeneo Huru ya Kiuchumi (EPZ) na kuendeleza huduma za Bandari Huru (Freeport services).

Pamoja na mafanikio hayo Mhe. Mwenyekiti, bado yapo maeneo mengine ya kisera ambayo hayajafanyiwa kazi kama vile:

(i) Kuanzisha ukaguzi wa bidhaa nje ya Nchi (Pre-shipment Inspection); na

(ii) Kuanzisha Sheria ya kuzuia utumiaji wa mbinu za kibiashara zisizo halali hasa 'Dumping'.

Aidha, mapitio yaliyofanyika Mhe. Mwenyekiti, yamebainisha kuwepo kwa upungufu wa kutozingatiwa kwa maeneo mengine muhimu ya kisera kama vile:

i. Masuala ya maonesho ya kibiashara ya kimataifa;
ii. Biashara inayofanywa kupitia mtandao (e-commerce);
iii. Biashara inayoendeshwa kupitia makampuni yaliyosajiliwa nje ya nchi (offshore companies and business);
iv. Masuala yanayohusiana na biashara za ndani, yakiwemo mazao gani ya biashara, ufungashaji wa bidhaa, ushindani, vipimo, na kumlinda mtumiaji;

Maeneo yote hayo Mhe. Mwenyekiti, yatazingatiwa katika mapitio ya Sera hiyo yatakayofanywa.

(c) **Uwekaji wa Mfumo Mpya wa Utoaji Leseni za Biashara:**

Mhe. Mwenyekiti**,** katika hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka wa fedha uliopita nililiarifu Baraza lako tukufu juu ya nia ya serikali ya kuufanyia mageuzi mfumo wa sasa wa usimamizi na mfumo wa utoaji leseni za biashara nchini kutokana na athari zake za mfumo wa ukuzaji biashara, gharama za uendeshaji na usimamizi wake na pia utitiri wa leseni za biashara ambapo baadhi yake hazina misingi ya kisheria katika utoaji wake. Serikali iliendesha utafiti wa kina katika eneo hili na kubainika kuwepo kwa aina nyingi za leseni, usimamizi dhaifu, kutobainisha dhamira ya utoaji wa baadhi ya leseni zaidi ya kutumika kama njia ya kukusanyia mapato tu na hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha biashara kufanywa nje ya mfumo rasmi na hivyo kudhoofisha wigo wa kodi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika utafiti huo imebainika kuwa Zanzibar inatumia njia zifuatazo katika utoaji wa leseni za biashara:

(i) Leseni (licenses);
(ii) Vibali (permits);
(iii) Vyeti (certificates);
(iv) Usajili (Registrations); na
(v) Ruhusa (authorisation)

Kadhalika, imebainika kuwa zipo taasisi nyingi zinazotoa leseni kwa biashara zinazofanana, kuwepo kwa kanuni na Sheria ndogo ndogo nyingi zinazoruhusu utoaji wa leseni au vibali vya biashara na hivyo kusababisha mkanganyiko katika usimamizi na udhibiti wa mwenendo wa biashara na maendeleo yake. Kukosekana kwa chombo cha kusimamia (regulatory authority) mfumo wa utoaji leseni za biashara ni moja wapo ya mambo yaliyobainika kama ni udhaifu katika mfumo wa sasa wa utoaji leseni za biashara nchini.

Rasimu ya Sheria mpya Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mfumo mpya wa utoaji leseni za biashara imeshaandaliwa na inaendelea kuzingatiwa na wadau mbali mbali. Rasimu hiyo inakusudia

kuweka mfumo mpya na taratibu zitakazorekebisha upungufu unaoonekana katika mfumo wa sasa wa utoaji leseni za kibiashara na usimamizi wake.

(d) **Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji na Utoaji Taarifa za Biashara:**

Mhe. Mwenyekiti**,** moja ya malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011-2012 ilikuwa ni kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa za kibiashara nchini kwa dhamira ya kukuza huduma za kibiashara (Business development services) ili kujenga misingi mizuri ya kuengeza uwezo wa uzalishaji, tija na ushindani hasa kwa wazalishaji wadogo wadogo na wakati. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kuwa Wizara yangu imeweza kukamilisha uwekaji wa mfumo huo kwa kutayarisha "*Domain*" ya wizara, "Database", mfumo wa mawasiliano ya ndani (LAN), na ukusanyaji wa takwimu muhimu za kibiashara na uzalishaji viwandani.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI:

Mhe. Mwenyekiti**,** majukumu makubwa ya Idara hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutathmini na kushauri mifumo na miundo ya kiutendaji kwa lengo la kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(ii) Kuandaa na kusimamia miundo ya utumishi kwa kada zinazosimamiwa moja kwa moja na Wizara;

(iii) Kutathmini mahitaji ya Watumishi katika Wizara na kuandaa mipango ya uajiri kwa ajili hiyo;

(iv) Kuandaa mipango ya mafunzo ya Wizara na kusimamia utekelezaji wake;

(v) Kutunza taarifa za kiutumishi kwa wafanyakazi wa Wizara;

(vi) Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi hasa ubora wa majengo, vifaa na usimamizi wake pamoja na utunzaji na uwekaji wa mali za Wizara kama vile majengo, mashine na raslimali nyenginezo za Wizara; na

(vii) Kuratibu utoaji wa huduma za uhasibu, ununuzi, utunzaji vifaa, ukaguzi wa ndani wa hesabu na ukondoeshaji wa masuala ya udhibiti wa ugonjwa wa UKIMWI na masuala ya jinsia.

Mhe. Mwenyekiti**,** utekelezaji wa malengo ya Idara kwa mwaka 2011 – 2012 ulikuwa kama ifuatavyo:-

Maendeleo ya Wafanyakazi:

Mhe. Mwenyekiti, muundo wa utumishi kwa kada ambazo zinasimamiwa na Wizara moja kwa moja umeandaliwa kwa mujibu wa elimu na uzoefu wa kazi walionao. Kwa taaluma nyengine ambazo zinasimamiwa na taasisi nyengine na ambapo wataalamu wa fani hizo wameajiriwa na

Wizara, miundo ya utumishi ya taaluma zao pamoja na uzoefu wao kwa kazi umetumika katika kuwapanga madaraja mbali mbali wanayostahiki.

Kwa upande wa ajira Mheshimiwa Spika, Idara ilifanya tathmini ya mahitaji na kubainika kuwa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi inahitaji jumla ya wafanyakazi 22 wa viwango vya elimu vya angalau Shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu au kiwango kinachofanana. Hata hivyo, kutokana na hali ya fedha kwa sasa, uajiri huo ingawa umekubalika, haukuweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa mafunzo ya wafanyakazi, Wizara yangu imechukuwa hatua mbali mbali za kuimarisha uwezo wa kiutendaji kwa watumishi wa ngazi mbali mbali. Hivi sasa wafanyakazi kumi na nne (14) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali na kugharimiwa na Wizara. Kadhalika, wafanyakazi kumi (10) wamepatiwa mafunzo ya ujuzi maalum kwa lengo la kuongeza tija ya utendaji. Mafunzo hayo yamefanyika katika nchi za China na India. Mafunzo hayo yalihusu mbinu za ukaguzi wa bidhaa, usalama wa chakula, ujasiriamali na masuala ya utumishi na uendeshaji raslimali watu.

Uimarishaji Mazingira ya Kazi:

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa uimarishaji wa mazingira ya kufanyia kazi, Idara iliendelea na ukarabati wa majengo yake mawili kati ya manne yaliyopo Unguja likiwemo jengo la Makao Makuu ya Wizara. Ukarabati huo bado unaendelea kwa majengo hayo mawili na kwamba kwa jengo la Makao Makuu ya Wizara utekelezaji wake umefikia hatua kubwa. Kwa upande wa jengo la Ofisi ya Wizara huko Pemba, Idara imeanza hatua za awali za kupata jengo kwa ajili ya Wizara. Hivi sasa Idara imeweza kupata eneo, kupimwa na hatua zinazoendelea hivi sasa ni kuandaa michoro na utayarishaji wa gharama za ujenzi. Kuhusu vitendea kazi, viliweza kupatikana kulingana na mpango wa manunuzi wa Wizara ambapo kwa ujumla Wizara imeweza kuendesha shughuli zake kwa ufanisi.

Maendeleo ya Jinsia na Udhibiti wa Maradhi ya UKIMWI:

Mhe. Mwenyekiti**,** katika kutekeleza lengo hili, Idara imeendelea kuchukua hatua za kuelimisha wafanyakazi masuala ya UKIMWI na Jinsia katika kazi za kila siku za Wizara. Aidha, Idara iliendesha semina moja (1) na imetayarisha vikao viwili vya kamati Tendaji ya UKIMWI na jinsia kwa ajili ya kutoa taarifa za utekelezaji wa masuala yanayohusiana na hayo.

IDARA YA BIASHARA NA UENDELEZAJI MASOKO:

Mhe. Mwenyekiti**,** utekelezaji wa malengo ya Idara ulikuwa kama ifuatavyo:-

Kuimarisha Mazingira ya Biashara:

Dhamira kubwa ya utekelezaji wa lengo hili, ilikuwa ni kuzifanyia mapitio sheria kuu za biashara nchini kwa lengo la kuzifanyia marekebisho na hata kuziandika upya ili ziendane na mazingira ya sasa ya kibiashara nchini na ulimwenguni. Kama nilivyoeleza

katika Hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2011 – 2012 kuwa Sheria hizo zimeandikwa upya na kwamba Sheria ya Leseni ilikuwa inaendelea kufanyiwa mapitio. Kwa ujumla rasimu zote za sheria hizo hivi sasa ziko tayari kwa kuzingatiwa na hatimaye kuwasilishwa mbele Baraza hili lako tukufu.

Ukaguzi wa Biashara:

Mhe. Mwenyekiti, Idara iliendelea na utekelezaji wa lengo la ukaguzi wa maeneo ya biashara kulingana na program za ukaguzi zilizopangwa kama ifuatavyo:-

a. Ukaguzi wa vituo vya mafuta, magari ya mafuta na matenki;
b. Ukaguzi wa mizani na vipimo;
c. Ukaguzi wa maduka ya kawaida na "Super Markets";na
d. Ukaguzi wa maghala na Bekari.

Matokeo ya ukaguzi huo Mhe. Mwenyekiti, ni kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 11** hapa chini.

Jadweli Nam. 11:

Ukaguzi wa Biashara:

Programu	Lengo 2011 – 2012	Utekelezaji	Asilimia ya Utekelezaji
1. Vituo vya Mafuta, Magari na Matenki	82	66	80
2. Mizani na Vipimo	3,000	2,152	75
3. Maduka ya Kawaida na Super Markets	3,005	2,769	92
4. Maghala na Bekari	800	192	24
Wastani wa utekelezaji wa ujumla:			**68**

Kwa ujumla utekelezaji wa lengo la ukaguzi ulifikia asilimia 68 ya lengo la jumla lililowekwa kwa mwaka 2011 – 2012.

Ada ya Ukaguzi:

Mhe. Mwenyekiti**,** Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS. 30.0 milioni kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kutokana na ada ya huduma za ukaguzi. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2012

Wizara imeweza kukusanya jumla ya TZS. 41.2 milioni ambazo ni sawa ongezeko la asilimia 37.2 ya lengo lililoekwa.

Kuratibu na Kuandaa Ushiriki wa Maonesho ya Biashara:

Mhe. Mwenyekiti**,** hili ni eneo jengine ambalo Idara ililifanyia kazi kwa lengo la kutafuta masoko ya ndani na nje ili kuwasaidia Wafanyabiashara na wazalishaji wadogo wadogo. Idara iliratibu ushiriki wa wafanyabiashara wa Zanzibar katika maonyesho yaliyofanyika ndani na nje ya Tanzania. Katika maonesho yaliyofanyika ndani ya Tanzania, Idara iliratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika maonesho mbali mbali ambapo bidhaa za viungo, madawa asilia, uchoraji wa hina, usindikaji wa chakula, samani zitokanazo na minazi zilioneshwa. Maonesho hayo ni kama yafuatayo:

- Maonesho ya Kimataifa ya Saba Saba wajasiriamali hamsini (50) walishiriki katika maonesho hayo
- Maonesho ya nane nane wajasiriamali wanane (8),
- Maonesho ya uhuru wajasiriamali kumi na mbili (12),
- maonesho ya Oman wajasirimali wanane (8),
- Maonesho ya Ujio wa "Prince Charles" wajasiriamali kumi (10),
- Maonesho katika Mkutano wa Sita wa Baraza la Biashara (ZBC) wajasiriamali ishirini (20); na
- Maonesho ya Wasyria ambapo wajasiriamali kumi (10) walishirikiana nao.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa maonesho ya nje ya Tanzania, Idara iliratibu ushiriki wa wajasiriamali kutoka Zanzibar katika maonesho ya Jua Kali yaliyofanyika Rwanda ambapo wajasiriamali sita (6) walishiriki, maonesho ya Korea 'EXPO 2012' ambapo miradi ya utalii, uvuvi, mazingira na uchoraji ilioneshwa. Katika maonesho hayo washiriki 6 kutoka Zanzibar walihudhuria na kugharamiwa na Serikali. Kadhalika kwa maonesho ya Japan 'JETRO' ambapo ZSTC ilishiriki, bidhaa za mafuta ya makonyo na mafuta mengine ya viungo (essential oils) vilioneshwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uimarishaji biashara za ndani na hasa Soko la Jumapili, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inaendelea na maandalizi ya taratibu za kuimarisha Soko hilo ambalo tayari limefunguliwa rasmi. Serikali tayari imeunda Kamati ya wadau mbali mbali kwa ajili ya kushughulikia uendelezaji wa soko hilo. Kamati hiyo pamoja na mambo mengine itasimamia mambo yafuatayo:

(i) Uainishaji wa Eneo (au maeneo) ikiwa eneo la sasa halitakuwa muafaka kuendeleza soko;
(ii) Usanifu wa Eneo pamoja na gharama za uendeshaji;
(iii) Kuainisha miundombinu na huduma zinazohitajika
(iv) Utaratibu wa Sheria itakayosimamia suala hili;
(v) Usimamizi wa uendeshaji na mambo mengine.

Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa:

Mhe. Mwenyekiti**,** katika kuimarisha usafirishaji bidhaa nje kuna umuhimu mkubwa wa bidhaa hizo kuonesha uasili wa bidhaa. Moja kati ya vikwazo vikubwa vilivyosababisha bidhaa za Tanzania ikiwa pamoja na Zanzibar kupenya katika masoko ya kimataifa ni kukosekana utambulisho wa uasili (Tracebility) wa bidhaa zake katika masoko ya Kimataifa. Hivi sasa bidhaa nyingi zinazozalishwa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, zinatumia namba hizo za utambulisho (barcodes) kutoka nje ya nchi, na hivyo kuzifanya bidhaa hizo zisiwe na uasili wa Zanzibar au Tanzania kutokana na kutumia namba za nchi nyengine.

Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi imeshaweza kupata namba ya kimataifa ya utambulisho (barcode) kwa bidhaa zinazozalishwa nchini. Namba ya utambulisho huo kwa bidhaa za Tanzania ni 620. Hivi sasa, Wizara kwa kushirikiana na ZNCCIA tayari imeshafungua tawi rasmi hapa Zanzibar pamoja na kununua vifaa maalum kwa ajili ya utoaji wa namba hizo. Kadhalika, kwa kazi hiyo na pia Wizara inaandaa mafunzo kwa maafisa husika watakaofanya kazi hiyo kazi hiyo ya utoaji wa nambari. Kwa upande wake, Wizara imegharimu ununuzi wa vifaa muhimu kwa ajili ya uanzishaji wa huduma hii hapa Zanzibar.

Majadiliano ya Kibiashara (Trade Negotiations):

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa lengo la kukuza na kuendeleza biashara hapa Zanzibar, Wizara imekuwa ikishiriki katika mikutano na majadiliano mbali mbali ya kiuchumi na biashara hasa mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini (SADC), Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (IOR-AC) na majadiliano ya Mkataba wa Ubia Uchumi (EPA) baina ya EU na EAC pamoja na mikutano ya biashara baina ya nchi na nchi kama vile India, China na nchi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza mashirikiano ya kikanda kwa maendeleo ya biashara na uchumi, Zanzibar imeshiriki mikutano mbali mbali ambayo pamoja na maeneo mengine ilizingatia masuala yafuatayo:-

- Ugumu wa kibiashara kutokana na vikwazo visivyo vya kiushuru (Non Tariffs Barriers - NTBs) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- Kuendelea na Majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Maendeleo baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya (Economic Partnership Agreements - EPA);
- Uanzishwaji wa Eneo huru la kibiashara baina ya Jumuiya za SADC, EAC na COMESA (SADC-EAC-COMESA Tripartite Free Trade Area);
- Mazingatio ya maombi ya Uturuki ya kuanzisha ushirikiano wa Kibiashara na Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- Majadiliano ya kibiashara baina Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani;

- Majadiliano ya Kibiashara baina Jumuiya ya Afrika Mashariki na India;
- Majadiliano ya Kibiashara baina Jumuiya ya Afrika Mashariki na China;
- Ombi la Rwanda la kuendelea na uagiziaji sukari; na
- Kuendelea na majadiliano kuhusu uanzishaji wa Eneo moja la Forodha (Single Customs Territory) katika EAC.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika Hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012 niligusia suala la mpango wa kukuza biashara kwa Tanzani (Trade Sector Development Programme –TSDP) ambapo Zanzibar ilitarajiwa kutekeleza miradi mitatu katika maeneo ya uwekaji wa madaraja ya hoteli za kitalii, mafunzo kuhusu malibunifu na kuanzisha kitengo cha uratibu. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Tanzania Bara imekamilisha maandalizi ya mpango wa utekelezaji wa programu hiyo (programme documents) kwa ajili ya kuwasilishwa kwa wafadhili. Mpango huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mhe. Mwenyekiti**,** ushiriki wa Zanzibar katika mikutano hiyo unaipa nafasi ya kuelewa fursa zilizomo katika mashirikiano hayo ya kiuchumi pamoja na kuwa mshiriki mzuri katika kuendeleza uchumi na biashara.

Urasimishaji Biashara na Rasilimali:

Mhe. Mwenyekiti**,** Serikali ya Jamhuriya Muungano wa Tanzania ilianzisha Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) katika mwaka 2005. Mpango huu ni sehemu ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) na Mkakati wa Kuondoa Umasikini Zanzibar (MKUZA) ambao unakusudia kuwawezesha walengwa kutumia rasilimali na biashara zao kujipatia mitaji, soko pana na fursa zingine zinazopatikana katika sekta rasmi na hivyo kupunguza umasikini wa kipato. Kwa upande wa Zanzibar, Mpango huu unaratibiwa na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni makubwa ya Mpango huu kama nilivyogusia hapo juu, ni kuwawezesha wafanyabiashara ndogo ndogo kuwa na uhai wa kisheria utaowawezesha kuwa na sifa tatu muhimu zifuatazo:-

(i) Kuwa na biashara iliyosajiliwa na iliyotenganishwa uendeshaji wake na mali binafsi;
(ii) Kuwa na hadhi ya kisheria (*legal states*) na kuendesha biashara katika soko pana zaidi; na
(iii) Kuwa na mfumo wa umiliki mali uliowazi na hivyo kuiwezesha mali hiyo kuhamishika kwenda kwenye soko lenye fursa bora zaidi na kuongezeka thamani.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango huu, Wizara iliweza kufanya utambuzi wa wafanyabiashara wadogo wadogo 500 katika Wilaya ya Magharibi na kuweza kuwapatia

mafunzo yanayohusiana na taratibu za kufanya biashara kwa mujibu wa Sheria, zikiwemo usajili wa biashara, ulipaji wa kodi, kuweka kumbukumbu za mahesabu na masuala ya bima.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA:

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo ya Wizara chini ya Idara hii ulikuwa kama ifuafuatavyo:

i. **Kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda:**

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa lengo hili ulihusisha maeneo yafuatayo:-

(i) Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda;
(ii) Kuchunguza vikwazo vya Maendelo ya Viwanda; na
(iii) Kutathmini mazingira ya uwekezaji katika Viwanda na mfumo wa vivutio katika Sekta ya Viwanda.

Kwa upande wa mapitio na matayarisho ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Wizara imeshaanza utekelezaji wake kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*) ambapo kazi hiyo inaendelea vizuri kwa kuandaa na kutoa mafunzo ya utayarishaji Sera kwa kikundi cha wataalamu wazalendo. Mwelekeo mzima wa uandaaji wa Sera hiyo umebainishwa na utalenga katika maeneo makubwa yafuatayo:

(i) Kubainisha majukumu ya Serikali na yale ya Sekta binafsi katika suala la uendelezaji viwanda nchini;
(ii) Kubainisha na kuweka mfumo wa vivutio kwa ajili ya maendeleo ya viwanda;
(iii) Kubainisha mfumo wa uendelezaji wa viwanda na biashara ndogo ndogo;
(iv) Upatikanaji mitaji kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na biashara ndogo ndogo;
(v) Ubunifu na utafiti (*innovation and research development*);
(vi) Ukuzaji wa teknolojia na utaalamu; na
(vii) Kubainisha masuala mengine muhimu kwa maendeleo ya viwanda nchini.

ii. **Kusimamia na kuratibu maendeleo ya viwanda vichache vilivyopo:**

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za Serikali za kuimarisha uwekezaji na uendelezaji wa viwanda viliopo, Wizara ilifanya ukaguzi kwa lengo la kubainisha changamoto za viwanda na kutoa usaidizi wa kitaalamu, kisera na mbinu za biashara kwa wazalishaji wadogo wadogo. Katika kipindi hichi, jumla ya viwanda na wazalishaji wadogo wadogo 132 walitembelewa na kufanyiwa ukaguzi.

Kama ilivyotarajiwa, Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi huo uligundua kuwepo changamoto nyingi zinazokabili sekta ya viwanda na wazalishaji wadogo wadogo zikiwemo:

(i) Ufungashaji duni wa bidhaa zinazozalishwa;
(ii) Ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na mbinu za masoko;
(iii) Ubora hafifu wa bidhaa zinazozalishwa na baadhi ya viwanda;

(iv) Ugumu wa upatikanaji wa mitaji; na
(v) Usalama duni kwa wafanyakazi katika mifumo ya uzalishaji kwa baadhi ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa ufungashaji bidhaa, Wizara yangu inaandaa utafiti wa suala hili kwa lengo la kutathmini mahitaji halisi ya vifungashio, gharama zake ili kuandaa utaratibu utakaowarahisishia wajasiriamali wa Zanzibar kupata vifungashio wanavyohitaji.

iii. **Ukuzaji Ujasiriamali:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ukuzaji wa ujasiliamali na uendeshaji wa mbinu za utafutaji masoko, zipo juhudi kubwa zilizoelezwa katika eneo hili kupitia mipango inayotekelezwa na Serikali na Sekta binafsi hasa kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar (*ZNCCIA*). Kupitia mpango wa kuwaendeleza wajasiriamali wadogo wadogo (*Entrepreneurship Development Programme*). Wizara yangu iliweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara wadogo wadogo 30 na pia kutoa usaidizi wa vifaa vya ukaushaji dagaa na ujenzi wa kiwanda cha utengenezaji sabuni cha Mpiki Miliki, kilichopo Wete Pemba. Kadhalika, Wizara yangu iliweza kuwapeleka wajasiriamali 6 nchini China kwa ziara za kimafunzo (*exposure visits*) kujifunza mbinu za uimarishaji wa ubora wa bidhaa zao.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi nyengine za kuwaendeleza wajasiriamali, zilichukuliwa kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashra, wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar (*ZNCCIA*) kwa kushirikiana na *Tanzania Private Sector Founadtion (TPSF*) ambapo ilianzisha na kutekeleza Pragramu maalum ya Fanikiwa Kibiashara (*Business Development Gateway Program - BDG*) kwa ajili hiyo. Chini ya program hii Wafanyabiashara na wajasiriamali wa Zanzibar wananufaika pia na mafunzo na uongezaji ujuzi kupitia mpango wa BDG. Kwa mwaka huu kwa mfano kiasi cha shilingi 594, 600,000 zitatolewa kama tuzo kwa wajasiriamali 208 chini ya Mpango mdogo wa Kuchambua Biashara (*Business Diagnostic Program - BDP*). Chini ya mipango midogo ya BDP na (*Business Plan Competition*) *BPC*, asasi 17 toka Zanzibar ni miongoni mwa washindi 400 waliopokea zawadi ya kiasi cha shilingi 47, 600, 000; na asasi 3 miongoni mwa asasi 100 bora nchini waliopata kiasi cha zawadi ya shilingi 16,800,000 na kufanya jumla ya zawadi miongoni mwa washindani miatano (500) bora kuwa shilingi 64,400, 000 kwa asasi za Zanzibar tu.

Pamoja na juhudi hizo, Mhe. Mwenyekiti, bado ipo changamoto kubwa ya kuendeleza ujasiriamali ili kuwawezesha wananchi kuzalisha kwa tija na hivyo kuwajengea uwezo wa kupambana na umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, Katika Hotuba yangu ya bajeti mwaka uliopita nililiarifu Baraza lako tukufu kuhusu kupiga hatua ya maendeleo katika juhudi zetu za kukuzaji ujasiriamali baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchangia TZS. 200.0 milioni kwa ajili ya uendelezaji ujasiriamali Zanzibar. Fedha hizo bado hazijapatikana na Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ili fedha hizo ziweze kuwaendeleza wajasiriamali katika masuala ya ununuzi wa vifaa, ufungashaji (*packaging*), utambulisho wa bidhaa (*barcodes*) mafunzo na mengineyo.

iv. **Mpangokazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya utafiti wa kuongeza thamani mazao (value chain study), na Sera ya Biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs):**

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua nyengine za kuendeleza na kukuza ujasiriamali, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*) ilifanya utafiti maalum wa kubainisha namna ya kuongeza thamani mazao ya kilimo (*value chain study)* pamoja na kutekeleza sera ya kukuza biashara za kati na ndogo ndogo (SMEs). Ili kutekeleza mapendekezo hayo ilihitajika kuandaliwa Mpango maalum kwa ajili hiyo. Mpango huo ulikuwa bado kuandaliwa kutokana na sababu mbali mbali kama vile uhaba wa fedha na utaalamu ili kusimamia utekelezaji wake. Hivi sasa Wizara inaendelea na utayarishaji wa Mpango huo wa utekelezaji kwa kushirikisha wadau mbali mbali.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa baadhi ya mapendekezo ya utafiti huo tayari yametekelezwa. Mapendekezo yaliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuzaji ujasiriamali;
(ii) Kuwepo kwa utambulisho wa bidhaa (barcodes); na
(iii) Uanzishaji wa Taasisi ya Viwango ya Zanzibar.

OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO – PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara katika kusimamia biashara, maendeleo ya viwanda na uendelezaji masoko kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa kazi zake katika maeneo hayo umeelezwa katika ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa Idara moja moja hapo juu.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA:

Taasisi Viwango ya Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uanzishwaji wa Taasisi ya Viwango ya Zanzibar, baada ya kutungwa kwa sheria ya viwango ya Zanzibar ya mwaka 2011 (*The Zanzibar Standarad Act*)Wizara imepatiwa majengo mawili katika maeneo ya Maruhubi ambayo yatatumika kwa ofisi ya chombo hichi. Wizara imetenga fungu la fedha kufanya matengenezo ya majengo hayo pamoja na ununuzi wa vifaa muhimu vya kuanzia kazi. Aidha, Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na hatua za uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa chombo hichi.

Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Vipimo ya Zanzibar, na Kamisheni ya Ushindani ya Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilijiwekea lengo la kuanzisha Mamlaka maalum kwa ajili ya kusimamia vyema Masuala ya Mizani na Vipimo pamoja na Masuala ya Ushindani katika biashara hapa Zanzibar. Kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka

2011 – 2012, mapendekezo ya rasimu ya Sheria hizo yamekamilika. Kadhalika, kama nilivyoeleza hapo awali katika Hotuba yangu hii kuwa mazingatio ya rasimu hizo yaliaghirishwa ili kupisha ukamilishaji wa mapitio ya Sheria ya Leseni na kuandaliwa kwa Sheria mpya ya usimamizi wa utoaji leseni za biashara nchini. Kama nilivyoeleza hapo awali, rasimu ya Sheria hiyo imeshakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria hizo mbili bado hazijafutwa na zinaendelea kutumika katika kusimamia biashara hapa Zanzibar. Majukumu makubwa ya Sheria hizo ni pamoja na:-

- Kufanya ukaguzi wa mezani ili kuhakikisha usahihi wake;
- Kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta;
- Ununuzi wa vifaa vya mezani;
- Kutoa Mafunzo kwa wafanyakazi;
- Kusimamia mwenendo wa biasharara na ushindani;
- Kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma; na
- Kuangamiza bidhaa zilizomalizika muda na zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Kwa sasa Mhe. Mwenyekiti, kazi zote hizo zinafaywa chini ya Idara ya Biashara ambayo ina vitengo maalum vya kusimamia Mizani na Vipimo pamoja na kumlinda Mtumiaji. Utekelezaji kamili umefafanuliwa katika maelezo ya Idara ya Biashara na Uendelezaji Masoko.

Baraza la Biashara la Zanzibar:
Mhe. Mwenyekiti, Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Baraza la Biashara ni kueka jukwaa la majadiliano baina ya sekta binafsi na sekata umma ili kujenga ukaribu katika utekelezaji wa mikakati ya maendeleo na kukabiliana na changamoto za maendeleo hayo kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho mkutano mmoja wa Baraza la Biashara (*ZBC*) umeandaliwa ambao ulijadili Mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Uhakika wa Chakula, Kufanya Kazi na Mashirika ya Kimarekani, Mazingira na Fursa za Uwekezaji Zanzibar pamoja na mada ya Utalii kwa Wote.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi za kawaida**,** Baraza liliendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa maagizo ya mkutano huo kutoka sekta na Wizara tofauti, kufanya mapitio ya sheria (*Legal Notice*) ili kuendana na mazingira ya sasa, kuendelea kufanya tathmini ya uwezekano wa kuanzisha Mabaraza ya mikoa na kufanya vikao saba (7) vya Kamati Tendaji.

MASHIRIKA YA SERIKALI:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inasimamia mashirika mawili ya biashara ambayo ni Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*), na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*).

SHIRIKA LA BISHARA LA TAIFA – ZSTC:

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Shirika hili yamefafanuliwa kwa undani zaidi katika Sheria yake mpya iliyopitishwa na Baraza lako tukufu mwaka 2011.

Biashara ya Karafuu:

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa biashara ya karafuu, katika msimu wa mwaka 2011-2012, serikali ilikadiria kununua tani 3,000 za karafuu kutoka kwa wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu baraza lako tukufu kwamba, tokea kuanza kwa msimu wa karafuu 2011 - 2012 hadi kufikia tarehe 18 Juni, 2012 Serikali imeshanunua jumla ya tani 4,822.8 za karafuu zenye thamani ya TZS. 72.1 bilioni sawa na aslimia 160.8 ya lengo iliyojiwekea. Katika ununuzi huo jumla ya tani 4,490.8 sawa na asilimia 93 zenye thamani ya TZS. 67.1 bilioni zimenunuliwa Kisiwani Pemba na tani 332 sawa na asilimia 7 zenye thamani ya TZS. 5.0 bilioni zimenunuliwa kutoka Unguja. Aidha, ZSTC ilishanunua tani 922.6 za Makonyo zenye thamani ya TZS. 1.38 bilioni kutoka kwa wakulima. Aidha, hadi siku ya tarehe 18 Juni 2012 ZSTC iliweza kuuza nje nchi karafuu tani 4,040.75 zenye thamani ya USD 52.057 milioni sawa na TZS 83.6 bilioni.

Mheshimiwa Spika; kwa upande wa usindikaji makonyo na mazao mengine, shirika limezalisha tani 41.7 za mafuta ya makonyo, mkaratusi madawa na manukato yenye thamani ya TZS. 1,675 milioni.

Biashara ya mwani:

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012, niligusia nia ya Wizara yangu kusimamia biashara ya mwani kwa kuandaa mfumo wa gharama na kuongeza thamani. Wizara ilitarajia *ZSTC* pia kusimamia biashara hii mbali na biashara ya karafuu. Hata hivyo, lengo hilo halikuweza kutekelezwa kutokana na Wizara kulifanyia mageuzi makubwa Shirika la *ZSTC* na kulipangia mikakati zao la Karafuu. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara na Uvuvi na Mifugo inatarajia kusimamia biashara ya mwani kwa sasa.

Mageuzi ya *ZSTC*:

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa mageuzi ya *ZSTC* ambayo ni sehemu ya Mkakati wa Kuendeleza Zao la Karafuu Zanzibar (*Zanzibar Cloves Development Strategy – ZCD*S), utekelezaji wake umeanza kama ifuatavyo:-

ii. Sheria mpya ya *ZSTC* imetayarishwa na kupata ridhaa ya vyombo vyote vya Serikali na Baraza la Wawakilishi na kwamba hivi sasa iko tayari kwa utekelezaji;

iii. Mpango wa mageuzi kwa ajili ya *ZSTC* nao umetayarishwa na tayari umeshaingizwa katika mfumo wa Serikali kwa kuzingatiwa na kuidhinishwa. Mpango huo wa Mageuzi utakuwa na Malengo kumi (10) na hatua za utekelezaji (*Activities*) 89. Jumla ya USD 12.34 milioni zitahitajika kwa ajili ya utekelezaji

wa Mpango huu kwa kipindi cha miaka kumi ijayo. Bajeti ya ZSTC kwa mwaka wa fedha 2012-2013 utazingatia pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa Mpango huo wa mageuzi

SHIRIKA LA MAGARI (MTC):

Kukamilisha taratibu za kulifunga (*wind up*) Shirika la Biashara la Magari (*MTC*):

Mhe. Mwenyekiti, kaama nilivyoeleza katika hutuba yangu ya mwaka 2011 – 2012 kwamba serikali imefikia uamuzi wa kulifunga Shirika la Magari (*MTC*) kutokana na shirika hilo kukosa nafasi ya kufanya biashara kwa ufanisi na kuwepo ushindani mkubwa kutoka sekta binafsi. Aidha, Shirika lina mtaji mdogo jambo ambalo limepelekea kushindwa kutekeleza kazi zake za kuagiza magari na vipando vyengine ipasavyo, na hivyo kutoa nafasi kubwa kwa sekta binafisi kuhodhi soko la biashara hiyo. Shirika kwa sasa linategemea zaidi malipo ya vibali, kodi za majengo na biashara ndogondogo katika kugharamia uendeshaji wa shirika.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kutekeleza lengo hili, Wizara ilitarajia kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kubainisha mali na madeni ya Shirika,
- Kutayarisha mafao ya wafanyakazi kwa kuzingatia ongezeko la mshahara,
- Kueleza wafanyanyakazi azma ya Serikali ya kulifunga Shirika kwa mujibu wa Sheria ya Kazi,
- Kutayarisha Hati ya Rais ya kulivunja Shirika na
- Kuteua mdhamini atakaekabidhiwa mali na madeni.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa utekelezaji wa malengo hayo, mali zinazojumuisha majengo, vifaa, vyombo vya usafiri na mali nyenginezo pamoja na madeni yao Shirika yameweza kubainishwa, mafao ya wafanyakazi yanaendelea kutayarishwa kwa kuzingatia mabadiliko ya mshahara yaliyofanywa hivi karibuni. Aidha, katika utekelezaji wa suala hili kunahitajika umakini mkubwa na kwamba, Serikali inazingatia taratibu zote za ustaafishaji wafanyakazi kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Sheria ya Kazi Nam. 11 ya Mwaka 2005 ikiwemo kuanzisha majadiliano na wafanyakazi juu ya dhamira ya hatua hiyo ya Serikali. Baada ya kukamilika kwa taratibu hizo Serikali itaendelea na taratibu nyengine za kuandaa Hati ya Rais ya kulivunja Shirika pamoja na kuteua mdhamini kama inavyoelekezwa na masharti ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002.

CHANGAMOTO:

Mhe. Mwenyekiti, Katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2011/2012 yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, zipo pia changamoto kadhaa ambazo ziliendelea kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyopangwa na ufanisi wa sekta ya biashara na maendeleo ya viwanda. Katika maelezo yangu ya bajeti kwa mwaka 2011-2012 nilitaja changamoto mbali mbali zinazokabili maendeleo ya

viwanda na uimarishaji masoko hapa Zanzibar. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Mwenendo wa biashara katika masoko ya kimataifa ambao kwa kiasi kikubwa umeendelea kutibuliwa na matokeo mbali mbali ya majanga ya kimaumbile ikiwemo ukame na mafuriko, matukio ya kisiasa na vita vinavyoendelea katika nchi za kiarabu na kuathiri bei za mafuta duniani, uharamia katika pembe ya Afrika, kasi ndogo ya kuimarika chumi za magharibi kunatokana na mtikisiko wa kifedha uliojitokeza hivi karibuni na athari zake kwa mwenendo wa bei za chakula katika soko la Zanzibar.

ii. Uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani wa bidhaa na udhaifu wa kutumia fursa za masoko ya kikanda kuongeza usafirishaji pamoja na thamani ya uzalishaji huo.

iii. Ari ndogo ya wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo, kujifunza mbinu mpya za kibiashara ili kujijengea uwezo wa kujitegemea wenyewe.

iv. Mwitiikio mdogo wa sekta binafsi kuwekeza katika viwanda na kuongeza pato la sekta hiyo. Kadhalika, utaalamu mdogo katika uendeshaji viwanda, mitaji, gharama za umeme na malighafi zimeendelea kuainishwa kama ni kikwazo katika maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar.

v. Mfumo na utekelezaji wa sheria za kodi ambao unaacha mwanya kwa bidhaa za nje ambazo pia huzalishwa nchini, kuingia na kuuzwa kwa bei za chini kuliko gharama halisi za kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini.

vi. Utayari na uwezo wa wafanyabiashara wa Zanzibar kuzitumia fursa za kibiashara zilizopo katika masoko ya Jumuiya za Kikanda kama vile *SADC* na *EAC*.

Kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, changamoto hizo bado zipo na zinaendelea kuwa na athari katika utekelezaji wa mikakati na malengo tunayojipangia.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012, sasa naomba kuelezea malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza kuwa malengo ya mwaka 2012/2013 yamewekwa kwa kuzingatia jukumu mahsusi la utekelezaji wa Dira 2020, Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA), Mkakati wa Kusafirisha bidhaa nje (*NES*), Maagizo maalum ya Serikali kwa Wizara, Mpango Mkakati wa Wizara na Maelekezo na Hotuba ya Rais katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi mwezi Novemba 2010. Hivyo, kurahisisha ufafanuzi wake, nitatoa maelezo ya malengo hayo kiidara.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*) kwa ajili ya ujenzi wa uwanja Maonesho ya Biashara ya Kimataifa;

ii. Kuanza utekelezaji wa mapendekezo ya Utafiti wa Kuifanya Zanzibar eneo tengefu la Uchumi (*SEZ*) kwa kuandaa Mpango wa Kazi (*Action Plan*) wa utekelezaji wake.

iii. Kukamilisha utungaji wa sheria mpya na Sera ya Biashara; mfumo mpya wa kisheria wa utoaji wa leseni za biashara; Sheria ya Mizani na Vipimo; na Sheria ya Ushindani na Kumlinda Mtumiaji.

iv. Uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa kuendeleza Zao la karafuu (*Cloves Development Strategy*) kwa:

   a. Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa Mageuzi ya *ZSTC*;
   b. Kukamilisha utungaji wa Sheria mpya ya Karafuu na mfuko wa Maendeleo yake;
   c. Kufuatilia uandaaji na uendeshaji wa sensa ya mikarafuu;
   d. Kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa kuongeza Thamani ya mauzo ya Karafuu kwa kutumia Tasnia za Malibunifu.

v. Kufanya utafiti kwa bidhaa zinazoweza kusafirishwa nje;

vi. Kuratibu Mkakati wa Usafirihaji bidhaa nje (*NES*); na

vii. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za biashara na viwanda kwa Kuimarishaji wa Kitengo cha Takwimu, na kuweka mfumo wa uwekaji taarifa za viwanda na uchambuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango Sera, na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 384.79 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,540.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo TZS 750.0 milioni ni mchango wa Serikali na TZS 790.0 milioni ni mchango wa wahisani.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuendelea na matengenezo ya majengo;

ii. Kuandaa michoro (*drawings*) pamoja na matayarisho ya gharama za ujenzi (BOQ) kwa ajili ya ofisi ya Pemba.

iii. Kuajiri wataalamu 17 wa Wizara pamoja na kuratibu ajira za wafanyakazi 5 wanaohitajika katika Baraza la Biashara;

iv. Kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya Zanzibar na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Tanzania Bara;

v. Kuendelea kusimamia mafunzo ya wafanyakazi 11 walioko masomoni na kupeleka wengine 3 kwa muda mrefu na 7 muda mfupi;

vi. Kuimarisha Kitengo cha Habari cha Wizara (*Information, Education and Communication –IEC*)

vii. Kuimarisha miundo ya utumishi (*scheme of Services*");

viii. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Ununuzi wa Wizara kwa bidhaa na huduma (*goods and services*);

ix. Kukondoesha masuala ya UKIMWI na jinsia katika mipango na shughuli za Wizara kwa kuelimisha wafanyakazi juu ya athari za ukimwi ili kuzuiya maambukizi mapya ya UKIMWI.

x. Kuendelea na taratibu za kulifunga Shirika la Magari kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya TZS 1,072.45 milioni kwa kazi za kawaida.

IDARA YA BIASHARA NA UENDELEZAJI MASOKO:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Biashara na Masoko inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuendelea kuzipatia fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar (*market research and product development*) ili kuziwezesha bidhaa hizo kupenya katika masoko ya nchi mbali mbali, kikanda (*EAC* na *SADC*) na kimataifa;

ii. Kujenga uwezo wa kitaalamu katika majadiliano, kushiriki mikutano na majadiliano ya kibiashara katika ngazi ya Kikanda na kimataifa, kuongeza juhudi za upatikanaji wa taarifa za biashara, na kuongeza uhamasishaji na ukuzaji biashara kwa kutumia mfumo wa ufuatiliaji bidhaa (*traceability and barcodes*);

iii. Kuendeleza kazi za uwekaji wa mfumo wa Kisheria, uendeshaji na usimamizi wa Soko la Jumapili na pamoja na uratibu uandaaji na usimamizi maonesho madogo madogo;

iv. Kuendelea na matayarisho ya Mkakati wa kukuza thamani ya mauzo ya bidhaa za viungo kwa kutumia Tasnia ya Malibunifu na kuendesha elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa "*branding*".

v. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ushindani na Vipimo ili kuhakikisha uwepo wa ushindani halalai wa biashara pamoja na kumlinda mtumiaji;

vi. Kukusanya ada ya TZS 60.0 milioni kutokana na huduma za ukaguzi utakaofanyika kupitia utekelezaji wa Sheria za Mizani na Vipimo na Sheria ya Kumlinda Mtumiaji; na

vii. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Urasimishaji biashara ambapo Idara utafanya utambuzi wa wafanyabiashara wadogo wadogo 500 katika Wilaya ya Wete huko Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Biashara na Uendelezaji Masoko iweze kutekeleza malengo yaliyowekwa, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 382.70 kwa kazi za kawaida, na TZS 487.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo TZS 250.0 milioni ni mchango wa Serikali na TZS 237.0 milioni ni mchango wa wahisani.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Maendeleo ya Viwanda inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kukuza ujasiriamali na maendeleo ya SMEs (*SME and Entreprenuership Development Programme*) kwa:-

- kutekelezaji wa Sera ya *SMEs*,
- kuendeleza mpango wa usindikaji mazao ya kilimo,
- kuboresha ubora wa bidhaa zinazozalishwa,
- kutoa mafunzo na usaidizi wa kitaalamu kwa wajasiriamali;

ii. Kuendelea na utayarishaji wa Sera mpya ya Viwanda;

iii. Kuweka mazingira mazuri kwa wajasiriamali, viwanda na Sera zake kwa

- Kuanzisha kituo cha maendeleo ya Viwanda;
- Kuendelea na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya miradi midogo midogo ya wajasiriamali;

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Maendeleo ya Viwanda iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS 273.23 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 200.0 milioni kwa kazi za maendeleo.

OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO – PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iliopo Pemba pia ina majukumu ya kusimamia shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba zikiwemo shughuli zote za utawala, kuimarisha mazingira bora kufanya biashara kwa upande wa Pemba, na kuratibu shughuli za wajasiriamali kisiwani humo.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi Kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 339.83 milioni kwa kazi za kawaida.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA:

Taasisi ya Viwango ya Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Viwango ya Zanzibar inakusudia kutekeleza shughuli zifuatayo:

i. Kufanya matengenezo ya majengo yake ya ofisi na maabara yaliyopo Maruhubi;
ii. Kufanya ununuzi wa vifaa vya maabara Kuanzisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar;
iii. Kuanza taratibu za kuajiri wafanyakazi na Mtendaji Mkuu wa Shirika;
iv. Kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar; na
v. Kutayarisha kanuni kwa ajili ya kutekeleza Sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ili Taasisi ya Viwango ya Zanzibar iweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 250.0 milioni na TZS 400.0 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo

Mamlaka ya Vipimo ya Zanzibar na Kamisheni ya Ushindani ya Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inakusudia kuanzisha vyombo ambavyo vitasimamia utekelezaji wa Sheria za vipimo na ushindani, baada ya kufanya mapitio ya Sheria ya Mezani na Vipimo ya mwaka 1983 pamoja na Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ya mwaka 1995. Vitengo vitaendelea kufanya kazi zifuatazo:

i. Kufanya uhakiki wa vipimo;
ii. Kufanya Ununuzi wa vifaa vya mezani;
iii. Utoaji wa Mafunzo kwa wafanyakazi;

iv. Kufanya ukaguzi wa mezani katika maduka na kuhakikisha usahihi wake;
v. Kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta;
vi. Kufanya tathmini ya uwekeaji wa mezani za elektroniki katika masoko ili kujua idadi ya bidhaa zinazozalishwa;
vii. Kusimamia Ushindani na Kumlinda mtumiaji, Mwenendo wa Biasharara na Mwenendo wa bei za bidhaa; na
viii. Kuangamiza bidhaa zilizomalizika muda na zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, ili utekelezaji wa masuala ya vipimo na ushindani hapa Zanzibar yaweze kutekelezwa kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 200.0 milioni kwa Taasisi ya Ushindani na ruzuku ya TZS 250.0 milioni kwa matumizi ya Taasisi ya Vipimo.

BARAZA LA BIASHARA LA ZANZIBAR (*ZBC*):

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Biashara la Zanzibar litatekeleza majukumu yafuatayo;

i. Kuanda mikutano miwili (2) ya Baraza la Biashara kwa lengo la kuendeleza jukwa la majadiliano;
ii. Kusimamia utumishi na uendeshaji wa *ZBC* ikiwemo malipo ya mishahara, ununuzi wa vifaa na samani pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wajumbe na wafanyakazi;
iii. Kusimamia vikao vya Kamati Tendaji ambapo kutakuwa na vikao vine kwa mwaka huu wa fedha;
iv. Kufanya tathmini ya haja ya kuanzisha mabaraza madogo madogo;
v. Kufuatilia utekelezaji wa maazimo ya mikutano; na
vi. Kuandaa makala juu ya masuala yanayojadiliwa katika Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Biashara la Zanzibar liweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 250.0 milioni kwa ajili ya Baraza hilo.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (*ZSTC*):

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) litatekeleza majukumu yafuatayo:

i. kununua karafuu tani 3500-4000 kwa msimu wa mwaka 2012/2013 na kuandaa mikakati ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi huo;
ii. kutekeleza mageuzi ya Shirika kwa mujibu wa Mkakati wa Mageuzi na hasa katika maeneo yafuatayo:
    a. kufanya *branding* ya karafuu;
    b. kufanya ukarabati wa baadhi ya vituo;
    c. kuajiri watalaamu 12 wapya;
    d. kufuatilia masoko ya karafuu.

iii. Kuimarisha biashara ya Karafuu katika soko la ndani, soko la utalii na masoko ya kikanda, pamoja na kuimarisha ufungashaji wa bidhaa za karafuu, makonyo na viungo vyengine.
iv. Kuendelea na taratibu za kupunguza wafanyakazi kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio ya wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, namshukuru Mhe. Spika, namshukuru Naibu Spika, nawashukuru Wenyeviti wote wawili na Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu, awajaalie viongozi wetu wa Baraza la Wawakilishi na wawakilishi wote afya njema, awajaalie ari ya kufanyakazi, awajaalie awaelekeze njia iliyonyooka ili Baraza lako tukufu lifanyekazi zake kwa uwadilifu mkubwa kama inavyofanya.

Mhe. Mwenyekiti, sinabudi kukiri vile vile kuwa mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2011/2012 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa Wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu ikiwa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na Kamati zake za kudumu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau mbali mbali kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo:-

(i) Jamhuri ya Watu wa China;
(ii) India;
(iii) Shirika la Kimataifa la Kusimamia Malibunifu (*World Intellectual Property Organisation – WIPO*);
(iv) Kituo cha Biashara cha Kimataifa (*International Trade Center – ITC*)
(v) Serikali ya Marekani;
(vi) Korea Kusini;
(vii) Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*);
(viii) Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*);
(ix) Benki ya Dunia (*World Bank*);
(x) Shirika la Biashara Duniani (*WTO*);
(xi) Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Secretariat*);
(xii) Jumuiya za Wafanyabiashara, Wenye Viwnda na Wakulima za Zanzibar na Tanzania Bara;
(xiii) Baraza la Biashara la Tanzania (*TNBC*); na
(xiv) Wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo na Wawekezaji wa Viwanda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza kwa dhati moyo wangu wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku na kunistahamilia maudhi yangu yote, licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali. Matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao, ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati, wadogo na Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali pamoja na bidhaa muhimu za nguo, vyakula, vyombo vya moto, vifaa vya ujenzi na kadhalika. Nawaomba waendelee kushirikiana na wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao. Aidha, nawaomba wafanyabiashara waekeze katika viwanda na biashara ya viungo (*spices*) kama vile mdalasini, manjano na viungo vyengine, kwani vinafaida kubwa na wala wasing'ang'anie upande mmoja tu katika kuendesha biashara na kuongeza ajira nchi mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati zinazotoka katika sakafu na vyumba vya moyo wangu kwa kwa wananchi wa Jimbo la Mtoni, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokuwa mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Vile vile nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee na ninaithamini sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima napenda nichukue fursa hii kumuombea dua Rais wetu kipenzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein Mwenyezi Mungu amjaalie maisha marefu, afya njema na *Inshaallah* aweze kutuongoza nchi yetu kwa salama na amani. *(Makofi)*

Vile vile nachukua fursa hii pia kumuombea dua Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad Mwenyezi Mungu ampe afya njema, amjaalie kila la heri aweze kumshauri Rais wetu vizuri katika kuendesha nchi yetu. *(Makofi)*

Pia nichukue fursa hii kumuombea dua Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi Mwenyezi Mungu amjaalie kila la heri ampe afya njema na maisha marefu aweze kutuongoza kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwaombea Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mwenyezi Mungu awajaalie umahiri mkubwa wa uongozi bora na waweze kutuongoza wananchi wote kwa umahiri mkubwa na *Inshaallah* asitokee tena waziri mwengine kujiuzulu baada ya huyu ambaye tayari ameshajiuzulu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwaombea dua Wawakilishi wote wa majimbo 50 waliochaguliwa na wananchi na wale ambao walioteuliwa Mwenyezi Mungu awajaalie kila la

heri waweze kushirikiana na serikali yetu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mwenyezi Mungu atujaalie kila la heri kwa Mwezi Mtukufu huu wa Ramadhani na Mwenyezi Mungu atakabali dua zetu *Inshaallah* aijaalie Zanzibar iwe nchi ya amani, nchi bora ya kiuchumi. *(Makofi)*

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake kama ilivyojipangia, naliomba Baraza lako Tukufu sasa liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 5,580 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kati ya fedha hizo shilingi 2,453.0 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida, shilingi 2,227.0 milioni kwa kazi za maendeleo na shilingi 900.0 milioni ruzuku kwa taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara. Jadweli Nam. 12 hapa chini linafafanua zaidi.

Maombi ya matumizi ya wizara kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa upande wa ukusanyaji wa mapato Wizara imepewa lengo la kukusanya shilingi 60.0 milioni.

Jadweli Nam 12: Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

2012-2013 (TZS. Milioni):

Vote Nam.	Idara	Kazi za Kawaida	Kazi za Maendeleo	Ruzuku
03:	Afisi Kuu Pemba	339.83	-	-
04:	Mipango, Sera na Utafiti	384.79	1,540.0	-
05:	Maendeleo ya Viwanda	273.23	200.0	-
06:	Biashara na uendelezaji Masoko	382.70	487.0	-
07:	Utumishi na Uendeshaji	1,072.45	-	-
	Baraza la Biashara	-	-	250.0
	Taasisi ya Ushindani	-	-	200.0
	Taasisi ya Viwango Zanzibar	-	-	250.0
	Taasisi ya Vipimo	-	-	200.0
	Jumla ndogo:	**2,453**	**2,227**	**900.0**
	Jumla Kuu:	**-**	**-**	**5,580.0**

Kiambatanisho Nam. 1

MALENGO YA MWAKA 2011/2012:

(i) Kuendelea kuimarisha mazingira bora ya ukuzaji biashara:

- kufanya mapitio makubwa mfumo wa utoaji leseni za biashara nchini ili kurahisisha uanzishwaji na ufanyaji biashara;

- Kuanza utekelezaji wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar;

- Kuwasilisha serikalini kwa mazingatio Sheria za Ushindani na Kumlinda Mtumiaji, Mizani na Vipimo na sheria ya Biashara pamoja na kuandaa utekelezaji wake.

(ii) Kuendeleza Eneo la Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya biashara kwa kutayarisha michoro ya matumizi ya ardhi (*Land Use Plan*), kutayarisha michoro ya kiufundi (*Structural and Architectural Design*) pamoja na kuatayarisha gharama za mradi (*Bill of Quantity*), na kuanzisha maeneo mengine ya maonesho madogo madogo na masoko ya Jumapili ili kuwakutanisha wazalishaji na wafanyabiashara wa ndani na wanunuzi.

(iii) Kukamilisha utafiti wa kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi makini kuhusu mkakati wake wa kuimarisha uchumi na uendelezaji viwanda wenye lengo la kuchangamsha biashara. Utafiti huo kama nilivyoeleza hapo awali, unakusudia kuigeuza Zanzibar kuwa eneo tengefu la uchumi (*SEZ*) kwa kuzingatia nafasi yake ya kuimarisha ushindani ndani ya soko la Afrika Mashariki na nchi za Jumuiya ya *SADC*.

(iv) Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha usafirishaji bidhaa (*Export Strategy*);

(v) Kuliimarisha Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) kwa kulifanyia mageuzi makubwa ya kisheria na muundo, ili liweze kusimamia vizuri uendelezaji wa zao la karafuu, biashara yake na kuweza kushindana katika soko;

(vi) Kuanzisha Mfuko maalum wa kuendeleza karafuu (*Clove Development Fund*);

(vii) Kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda kwa kufanya mapitio ya Sera ya viwanda, kuchunguza vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya viwanda Zanzibar, na kuweka mfumo mpya wa vivutio kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo hapa Zanzibar;

(viii) Kusimamia na kuratibu maendeleo ya viwanda vichache vilivyopo ili kuelewa matatizo yao na kutoa usaidizi wa kitaalamu, kisera na mbinu za biashara ili viweze kuendesha shughuli za uzalishaji kwa ufanisi;

(ix) Kuimarisha mashirikiano baina ya Sekta binafsi na Serikali (*PPP*) kwa kutoa fursa kubwa zaidi kwa sekta hiyo kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa nchi;

(x) Kuandaa mapendekezo ya matumizi mbadala ya kibiashara ya eneo la Bwawani na mpango wa uendelezaji wake;

(xi) Kuandaa mpango kazi wa taarifa ya utafiti kuhusu kuongeza thamani mazao (*value chain study*), na Sera ya Biashara ndogo ndogo na za kati (*SMEs*) kwa ajili ya utekelezaji;

(xii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Biashara ya Zanzibar ya mwaka 2006;

(xiii) Kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa na takwimu za biashara;

(xiv) Kuendeleza mazingira mazuri ya kazi na maendeleo ya wafanyakazi kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi;

(xv) Kupitia Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) Wizara imepanga kununua tani elfu tatu (3000 tons) za karafuu kwa thamani ya shilingi 30,000.00 milioni.

(xvi) Kukamilisha taratibu za kulifunga (*wind up*) Shirika la Biashara la Magari (*MTC*) katika msimu unaoanzia Julai, 2011.

(xvii) Kukusanya mapato ya shilingi 30.0 milioni.

Kiambatanisho Nam. 2

MUUNDO WA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne, mashirika mawili pamoja na Afisi Kuu – Pemba kama ifuatavyo:

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko;
- Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Afisi Kuu – Pemba;
- Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*); na
- Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*).

Hata hivyo muundo huo unatarajiwa kubadilika kulingana na mapitio ya sheria zilizopo pamoja na kutekeleza sheria mpya iliyotungwa ambazo zitapelekea uanzishwaji wa taasisi mpya. Taasisi zinazotegemewa kuanzishwa ni:-

i) Kamisheni ya Ushindani;
ii) Taasisi ya Viwango ya Zanzibar; na
iii) Wakala wa Mizani na Vipimo Zanzibar.

MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Wizara ina majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara;
- Kukuza mashirikiano kati ya sekta banafsi na sekta ya umma;
- Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;
- Kuwaimarisha na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogo ndogo;
- Kusimamia ubora wa huduma na bidhaa zinazouzwa nchini;
- Kutafuta masoko ndani na nje ya nchi kwa bidhaa za Zanzibar;
- Kuendeleza Viwanda viliopo;
- Kuweka mazingira mazuri yatakayoshajihisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda;
- Kuimarisha na kukuza viwanda vodogo vidogo;
- Kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini;
- Kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti na sera zinazohusiana na uimarishaji na uendelezaji wa sekta za biashara na viwanda;
- Kuendeleza mashirikiano ya biashara kinchi, kikanda na kimataifa; na
- Kuwaendeleza na kuwajengea mazingira mazuri wafanyakazi wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante hoja imekubaliwa. Sasa tutamkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ili aje atupate maoni ya kamati. Mhe. Makamu Mwenyekiti karibu. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo) napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia afya na uzima na kwa tawfiq yake tumeweza kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Ibada Tukufu ya Funga, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali hapa Barazani ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, pamoja na watendaji wake wote, kwa jitihada zake za kutekeleza majukumu yake kama inavyopasa.

Aidha, nichukuwe fursa hii pia kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano waliyonipa, michango na mawazo yao kwa Serikali kupitia Wizara hii kila Kamati ilipofanya kazi zake. Juhudi zao zimetuwezesha kufanya kazi vizuri, hata leo hii nikaweza kusimama hapa kwa niaba yao kuwasilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin — Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Moh'd Ali — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa — Mjumbe
4. Mhe. Rufai Said Rufai — Mjumbe

5. Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mjumbe
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma Mjumbe
7. Mhe. Raya Suleiman Hamad Mjumbe
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad Mjumbe
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed Katibu
10. Ndg. Khamis Hamad Haji Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya Sekta kuu za Uchumi wa Zanzibar ambazo ni Biashara, maendeleo ya Viwanda na masoko, Kuimarisha misingi ya ushindani wa kibiashara, ubora wa bidhaa na huduma zinazoingizwa katika soko la Zanzibar, kukuza ushirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kuhusu biashara na maendeleo yake.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011 mwenendo wa uchumi na biashara duniani uliendelea kuwa wa kuyumba. Kutokana na kuyumba huko, mchango wa biashara katika uchumi wa dunia nao umepunguwa kutoka asilimia 53.2% mwaka 2008 na kufikia asilimia 48.2% mwaka 2011.

Hali hii imetokana na athari za kuanguka kwa masoko ya fedha na hisa, athari za madeni kwa baadhi ya nchi zilizomo katika ukanda wa sarafu ya *Euro* pamoja na machafuko ya kisiasa yanayoendelea kuzikumba nchi za Mashariki ya Kati.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2011, usafirishaji wa bidhaa duniani, licha ya kuongezeka na kufikia dola 17.780 bilioni, nchi za Afrika zimekuwa na sehemu ndogo ya usafirishaji huo, ambapo zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya dola 597 bilioni za usafirishaji wote ambao ni sawa na asilimia 3 tu.

Kwa upande wa Zanzibar usafirishaji bidhaa nje ulifikia shilingi 61.261 milioni kwa mwaka 2011 kutoka shilingi 17.806 milioni kwa mwaka 2010. Usafirishaji wa kiwango hicho umechangiwa sana na usafirishaji wa zao la karafuu, ambao umesababishwa na kuhamasika kwa wakulima kutokana na kuimarika kwa bei, pembejeo na soko la uhakika.
Hata hivyo, kamati yangu imeona kuwa kiwango hicho cha usafirishaji nje bado si cha kuridhisha sana, jitihada kubwa zinatakiwa zifanywe katika kuongeza uzalishaji na usafirishaji nje wa bidhaa za kilimo na viwanda, pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya biashara badala ya kusafirisha mazao ghafi pekee.

Mhe. Mwenyekiti, kama tujuavyo, zao la karafuu ni nguzo kubwa ya kupata mapato ya fedha za kigeni kwa nchi yetu. Msimu wa mavuno uliopita (2011/12) ulikuwa wa mafanikio ambapo hadi kufikia mwezi Juni mwaka huu Serikali imefanikiwa kununuwa jumla ya tani 4.822 kwa jumla ya shilingi 72.1 bilioni, sawa na asilimia 160.8 ya lengo lililowekwa la kununuwa tani 3,000 tu.

Hatua hii kubwa imefikiwa baada ya Serikali kupandisha bei ya ununuzi na wakulima kuhamasika kuuza karafuu zao *ZSTC*. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kupandisha bei, pia inawapongeza wananchi kuitikia wito wa kuuza karafuu zao kwa Serikali na kutokweda kwenye sio isiyo ya halali.

Mhe. Mwenyekiti, ili mchango wa zao hili kwa uchumi wa nchi yetu uwe endelevu, kamati yangu inaiomba Serikali kufanya tathmini ya Soko la Kimataifa la Karafuu mapema kwa ajili ya msimu ujao, ili matarajio ya wakulima wetu wa karafuu yaongezeke kwa kutarajia bei nzuri zaidi na kuvuka mafanikio tuliyopata msimu uliopita.

Aidha, kamati inaiomba wizara kuharakisha mageuzi ya Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) kama yalivyowekwa katika sheria iliyopitishwa na Baraza hili. Sambamba na hilo, kamati yangu inakumbusha utekelezaji wa ile ahadi ya Mhe. Rais, wakati akifunga msimu wa mavuno ya karafuu kisiwani Pemba mwezi April mwaka huu, ya kutafuta hakimiliki na nembo ya ubora ya zao la karafuu (*Brand*), ili msimu ujao wa karafuu ukianza tuwe tayari tuna hakimiliki na nembo ya ubora wa zao letu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaomba kupata maelezo ya hatua zilizofikiwa kuhusu mkakati wa kuimarisha sekta ya mwani, mazao ya baharini na chumvi, ambayo katika bajeti iliyopita (2011/12) jumla ya shilingi 1,000.002 milioni zilitengwa kwa ajili hiyo. Aidha, kamati inaishauri Wizara kutazama upya hali ya soko la mwani, kwani wakulima wetu kama ilivyofanya kwa zao la karafuu, bado bei wanayoipata wakulima wetu ni ndogo, ambayo haijali kupanda na kushuka kwa bei ya soko duniani.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu bado inalia na mfumuko wa bei kwa bidhaa mbali mbali zikiwemo za chakula. Mfumuko wa bei ulipanda kwa wastani wa asilimia 14.7 kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kwa mwaka 2010. Hali hii siyo nzuri, ukiangalia hali za maisha ya wananchi wetu zipo chini na mfumuko wa bei kama huu unaathiri maisha yao kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa Serikali inamatarajio ya kupunguza kasi ya mfumuko huu wa bei kwa mwaka 2012 kufikia hadi asilimia 9.7 kutokana na kushuka kwa bei ya vyakula na mafuta duniani, pamoja na mategemeo ya kuongeza uzalishaji. Kamati yangu inaishauri wizara kuwa makini sana katika usimamizi wa uagiziaji wa bidhaa za lazima za chakula kama vile mchele, sukari na unga wa ngano, ambazo baadhi ya wafanyabiashara hupandisha bei kiholela kwa kutumia visingizio vya kuongezeka bei ya soko la dunia hata kwa ile "*stock*", ambayo ipo tayari katika soko, na ambayo haijaathiriwa na upandaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaendelea kuikumbusha Serikali kufikiria na kutilia mkazo hatua za kuanzisha viwanda kama ilivyokuwa zamani, ili kuweka urari wa ushindani wa soko na kupunguza kasi ya uagiziaji bidhaa kutoka nje ambazo huchangia kuyumbisha soko la bidhaa za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2012 kumekuwa na wimbi kubwa la wafanyabiashara kutumia vibaya fursa iliyotolewa na Serikali ya unafuu wa ushuru kwa bidhaa muhimu za chakula kama mchele, unga wa ngano na sukari, ambazo wanazihamisha kwenda nje ya Zanzibar. Kamati yangu inaipongeza Wizara ya Biashara kwa kuchukuwa hatua za kukamata na kurejesha kodi iliyosamehewa kwa wafanyabiashara hao wasiokuwa waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya Serikali kuweka unafuu huo wa ushuru katika bidhaa za chakula bado wananchi hawaoni tofauti yoyote ya unafuu huo, kwa vile bado bidhaa hizo zinaonekana kuwa ghali kutokana na vipato vya wananchi wetu wa kawaida kuwa vidogo.

Hata hivyo, kamati yangu inapendekeza Wizara kutilia mkazo hasa katika kipindi kama hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, bidhaa za chakula za lazima kama mchele, unga wa ngano, sukari na tende, kupunguzwa ushuru, ili wananchi waweze kuzimudu na watekeleze ibada ya funga bila dhiki.
Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda na Masoko ni muhimu katika ukuwaji wa uchumi, nchi nyingi zilizoendelea duniani zimewekeza katika uimarishaji wa sekta ya viwanda pamoja na kutanuwa wigo wa soko la ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa viwandani.

Kuna umuhimu mkubwa kwa nchi kuanza na sera ya viwanda angalau katika sekta ya uvuvi, kwa kuwa rasilimali ya bahari inapatikana kwetu tunaweza kuanza mikakati ya kuwa na viwanda vya uvuvi, ambavyo pia vinaweza kuwa ni sehemu kubwa ya ajira kwa wananchi wetu wengi katika ukanda huu wa pwani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaomba maelezo ya Serikali kuhusu Mgogoro wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, kumekuwa na taarifa kuwa Serikali imeunda Kamati tatu kushughulikia mgogoro huu, hadi hii leo hakuna hata kamati moja iliyotoa ripoti yake, kamati inauliza lini ripoti hizo zitatolewa.

Aidha, kamati yangu inaitahadharisha Serikali kuwa makini katika kufanya maamuzi kuhusu mkataba kati yake na mwekezaji wa Kiwanda hicho. Hatua yoyote isiyokuwa ya uangalifu ya kusitisha mkataba inaweza ikagharimu fedha za walipa kodi, iwapo Serikali itashitakiwa kama vile ilivyotokezea kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mkataba wa *TANESCO* na *DOWANS*.

Mhe. Mwenyekiti, Uendelezwaji wa maeneo huru ya Viwanda (*EPZ*) umekuwa ndoto, kamati yangu imesikitishwa na maelezo ya Mhe. Waziri katika hotuba yake kuhusu ukosefu wa miundombinu ya umeme, maji na barabara katika maeneo ya *EPZ* ya Fumba na Micheweni. Hali hii inatia shaka udhati wa Serikali wa kuendeleza maeneo ya uwekezaji katika Sekta ya Viwanda, kwani haiwezekani kuanzishwe maeneo huru ya viwanda ambayo yanasubiri wawekezaji yakiwa hayana kivutio chochote kwa uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida, nyumba husafishwa kwanza kabla ya kuja mgeni, usitegemee mgeni aje halafu yeye asafishe nyumba, hiyo haiwezekani. Serikali lazima iweke miundombinu katika maeneo hayo ya EPZ, ili wawekezaji wakija waikute na wavutike kuwekeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la elimu ya biashara na uzalishaji kwa wajasiriamali litiliwe mkazo na matokeo yake yaelezwe. Kwa mfano, kamati yangu ilipofanya ziara ya kutembelea Kiwanda cha Kukaushia Dagaa kilichopo Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja, ilikutana na dosari hii. Kiwanda hiki ni kizuri, kina nyenzo za uzalishaji za kisasa na wanakijiji wa hapo wanaokiendesha wamepata utaalamu wa kazi hiyo.

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, Kamati imewakuta wajasiriamali hao hawana taaluma ya kutosha ya biashara, hawana uongozi ulioimara, hali ambayo imepelekea mpaka kamati inawatembelea hawana hata usajili. Kamati yangu inaomba maelezo ya wizara, hatua gani zimefikiwa hadi sasa kusaidia kiwanda kile kuanza uzalishaji na kama tayari wemeshapatiwa usajili pamoja na mafunzo ya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Soko la Jumapili *(Sunday Market)* katika eneo la Michenzani, ambalo kwa kweli linawasaidia wafanyabiashara wetu wadogo kutangaza bidhaa zao. Hata hivyo, kamati yangu inaikumbusha Wizara, haitoshi tu kwa Soko lile la Jumapili kuwekwa mashamiana pekee yake, panahitajika na huduma za choo japo kidogo na unadhifu wa eneo kwa ujumla.

Sambamba na hilo, kuna umuhimu mkubwa kuwasaidia mitaji au ruzuku wajasiriamali hawa wadogo ambao ndiyo kwanza wanaanza uzalishaji. Kwani hata nchi za wenzetu waliondelea, huwasaidia mitaji na ruzuku wakulima na wajasiriamali wao, ndiyo maana uzalishaji wao unaongezeka na kuchangia maendeleo ya viwanda vyao.

Mhe. Mwenyekiti, hatua hizi tunaweza kuzifikia, iwapo Wizara itaharakisha kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Viwanda (*Zanzibar Industrial Development Policy*) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*) pamoja na ukamilishaji wa mpango kazi wa Sera ya Wazalishaji Wadogo na Kati (*SMEs*).

Mhe. Mwenyekiti, suala la utambuzi wa uasili wa bidhaa (*traceability*) nalo ni muhimu katika usafirishaji bidhaa nje ya nchi na kusaidia wazalishaji wetu kupenya katika Masoko ya Kimataifa. Bidhaa nyingi zinazozalishwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla hazina namba za utambuzi (*barcodes*) na badala yake zinatumia utambulisho kutoka nje ya nchi. Hali hii inapelekea kukosa mapato na utambulisho wa bidhaa zetu kimataifa na kurudisha nyuma juhudu za wazalishaji wetu wa ndani kupenya katika Masoko ya Kimataifa.
Mhe. Mwenyekiti, kwa vile tayari Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imeweza kupata nambari ya Kimataifa ya Utambulisho wa Bidhaa kwa Tanzania, ambayo ni 620. Kamati yangu inaishauri Serikali kuhakikisha taratibu za kufunguwa tawi hapa Zanzibar na matayarisho ya wafanyakazi na vifaa zinaanza mara moja. Aidha, kamati yangu inaishauri Wizara katika suala hili, ifikirie kutafuta namba ya utambulisho wa bidhaa kwa ajili ya Zanzibar na kwa bidhaa za Zanzibar peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba nizungumzie kwa kifupi kuhusu baadhi ya taasisi na mashirika zilizo chini ya wizara hii. Kamati yangu inataka kujuwa lini mpango wa kulifunga Shirika la Biashara la Magari (*MTC*) utakamilika, kwa vile katika hotuba hii Mhe. Waziri amerejea tena kama ilivyokuwa mwaka jana na hadithi ya mpango wa kulifunga shirika hili unaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusu Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*) imekuwa inachelewa kuanza kazi, ukizingatia kuwa umuhimu wa kuwepo kwake hivi sasa ni mkubwa. Wananchi wetu wamekuwa wakilalamikia bidhaa mbovu zilizo chini ya viwango zinazoingizwa nchini, hasa mafuta ambayo hivi sasa yamekuwa yakichakachuliwa na kusababisha uharibifu kwa vyombo vya moto na mitambo.

Kamati yangu inaiomba Wizara itowe ahadi katika Baraza hili ya lini itakamilisha uanzishwaji wa taasisi hii, ili kuwaondolea wananchi wetu hatari ya kutumia bidhaa zilizo chini ya kiwango.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na inawaomba wajumbe wako wajadili, waelekeze, wakosowe kwa nia ya kurekebisha, kuimarisha na hatimae kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante na sasa ni zamu ya wachangiaji na kwa siku yetu ya leo kwa Wizara hii tutaanza na mchangiaji wa kwanza Mhe. Asha Bakari Makame, atafuatiwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadaye Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mpenzi wetu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2012/2013. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake, ameipanga vizuri inafahamika, inaeleweka na imeeleza namna ya mapato yatakayokusanya, pia imeeleza namna ya matumizi aliyoyatumia kipindi kilichopita na matumizi ambayo anategemea kutumia katika kipindi hichi ikiwemo pamoja na malengo yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana, kwa sababu inashughulikia zaidi maeneo muhimu ya uchumi ikiwemo suala zima la biashara, viwanda lakini pia na upatikanaji wa masoko, kwa sababu masuala ya masoko ni muhimu, kwani unaweza kuwa na bidhaa na ukawa huna mahala pa kuuza au hata pale unapokuwa na pahala pa kuuza pengine hapana soko la uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, mchango katika hotuba hii ni mdogo sana na zaidi ukizingatia kwamba wizara hii iko katika zile Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ambayo sisi tunaisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda, ambayo ni sekta muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, tena ni sekta ambayo wizara ya Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ndiyo inayoisimamia. Kwa kweli sekta hii ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote, ni sekta ambayo uchumi wake unaonekana kwa haraka, pia nchi yoyote haiwezi kuendelea bila ya kuwa na viwanda.

Sasa suala hili la kuanzisha viwanda hapa Zanzibar imekuwa ni nyimbo, pamoja na kwamba tumekuwa na viwanda. Kwa mfano, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui anatueleze kwamba wanavyo viwanda. Lakini viwanda vilivyopo hapa kwetu Mhe. Mwenyekiti, bado havijakidhi haja ya

kuweza kuinua uchumi wa nchi hii. Kwa hivyo, mimi naona bado hatujaweka mkazo unaostahiki katika sekta hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema sekta hii bado tunaifanyia mzaha na wala hatuna ile *seriousness* ya kuona kwamba Sekta ya Viwanda hasa katika maeneo ya visiwa inaweza kutuvusha na kuweza kunyanyua uchumi wetu na kila mmoja akajua sasa Zanzibar imepiga hatua kiuchumi. Sekta ya Viwanda ni sekta ambayo inaajiri watu wengi, yaani ni sekta inayotoa ajira kwa wananchi katika maeneo yote na inabeba eneo kubwa sana la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na kwamba anayo mikakati pamoja na malengo ya muda mrefu kama alivyotueleza katika kunyanyua sekta hii. Lakini juhudi kubwa za Serikali zinahitajika, kama vile masuala ya vivutio katika eneo hili, kwa sababu wawekezaji wa viwanda hawawezi kuja tu kama hatujaweka miundombinu ya uhakika yenyewe vivutio kama ilivyo sera zetu kwamba sekta hii hivi sasa itashughulikiwa na watu binafsi.

Lakini wawekezaji wa viwanda hawawezi kuja hapa ikiwa hatuna yale maeneo muhimu ambayo yatawawezesha wao kuja kuwekeza viwanda vyao. Badala yake itakuwa wanakuja wanachukungulia, wanaangalia maeneo yetu, wanaondoka wanakwenda kuwekeza viwanda katika maeneo mengine.
Mimi niiyombe sana serikali kwa ujumla, Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Fedha, pamoja na serikali kwa ujumla, ione umuhimu wa jambo hili. Si suala la Mhe. Waziri wa Biashara peke yake ni suala la serikali kwa ujumla. Maeneo au vivutio vya uwekezaji katika viwanda inahitaji mambo mengi.

Mfano tunahitaji kuwa na umeme wa uhakika. Sasa hivi hatuna umeme wa uhakika Zanzibar. Umeme wetu tunategemea kutoka Tanzania Bara.

Hatuna barabara za kuridhisha katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda. Hatuna maji ya uhakika na hizi ndio *factor* ambazo wenzetu wanaotaka kuekeza wanaziangalia kuliko hata masoko yenyewe. Mtu anaweza kuwekeza kiwanda chake, akazalisha bidhaa zake, akatafuta masoko nje si lazima kutumia soko la ndani.

Tokea huko nyuma tulikuwa tunasikia barabara ile ya *ring road* kule Fumba, safari hii kwenye bajeti ya Miundombinu haikujitokeza kabisa. Suala la *ring road* limeishia wapi na mambo mengine kadhaa wa kadhaa. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa ujumla iwekeze zaidi katika maeneo ya viwanda, ikiwemo kupunguza au kutoa motisha kwa wawekezaji wa viwanda. Ili waweze kuvutika na kuja kuwekeza viwanda vyao hapa. Kwa hili tusitegemee tupate faida kwa wakati huu. Tunaweza tukawaita wakaja halafu baadae tukapata faida katika sekta hii. Hilo moja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie juu ya eneo moja ambalo Mhe. Waziri hapa amelizungumzia katika hotuba yake. Juu ya uhamishaji bidhaa za chakula muhimu kwenda nje ya Zanzibar. Ametueleza hapa kwenye hotuba yake, ukurasa wa 14. Ametueleza kwamba kumekuwa na wimbi la wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wamekuwa wakisafirisha bidhaa muhimu za chakula kwa mfano mchele, sukari na unga wa ngano. Wafanyabiashara hao huwa

wanazichukua bidhaa hizo wanazisafirisha kwa njia ya magendo kuzipeleka Tanzania Bara kwa madhumuni ya kupata faida kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mimi Mhe. Mwenyekiti nieleze *concern* yangu juu ya jambo hili. Wafanyabiashara mara nyingi huwa wanatafuta soko. Wanahangaika na wanapoona pahala panatija basi ni mahala ambapo wanakimbilia. Hatuwezi kuwazuia wafanyabiashara wasifanye jambo hilo. Pamoja na kwamba kuna sheria ambayo ametueleza kwamba kulikuwa na sheria ambayo ilikuwa inatumika wakati ule wa Bizanje ya kuzuia bidhaa zinazoingiwa na Bizanje hapa ili zisiweze kusafirishwa nje kwa kuzuia magendo. Lakini sheria ile sasa hivi imekuwa haifanyi kazi pamoja na kwamba ipo. Kwa sababu Shirika lile la Biashara la Bizanje halipo limefutwa, sasa hivi tunatumia wafanyabiashara binafsi kuagiza bidhaa zao kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, mimi *concern* yangu kwamba jambo hili pamoja na kwamba tunahisi lina adhari kwa Zanzibar kwamba huwenda likatupunguzia *demand* ile ya mchele katika visiwa vyetu. Mimi sifikirii hivyo. Mimi nadhani tuangalie zaidi athari ile ambayo inaweza ikaikuta Zanzibar hasa kiuchumi. Katika soko la *East Africa* kama ulivyotueleza kwamba tunatakiwa sisi katika bidhaa ya mchele tutoze kwa asilimia 75. Lakini sisi tumeomba serikali ya SMZ tupunguziwe ili tuweze kutoza kwa shilingi 12.5 kama ulivyoeleza, ili kuwapa nafuu wananchi wetu katika bidhaa hizi muhimu tatu, sukari, unga wa ngano na mchele.

Kwa mujibu wa maelezo uliyoyaeleza hapa unahisi kwamba kitendo cha wafanyabiashara kuchukua bidhaa hizo ambazo tayari zimeshatemshwa hapa na kupelekwa kule ni njia ya kujipatia faida kubwa kwa wafanyabiashara.
Mimi mawazo yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba tuwaruhusu wafanyabiashara wafanye biashara. Wafanyabiashara wa Zanzibar wanaotaka kupeleka biashara zao Tanzania Bara basi badala ya kulipa asilimia 12.5 basi walipe asilimia 25 kama ile inayotozwa Tanzania Bara. Wenzetu kule wao wapo kwenye asilimia 25, basi tuwaruhusu wafanyabiashara walipe asilimia 25 ya ile bidhaa ambayo wanaihitaji kupeleka Tanzania Bara. Badala ya kuwapiga adhabu maana sisi tunaona kama vile wanafanya magendo. Haya magendo yanakuja kutokana na hiyo adhabu kubwa ambayo tumeiweka. Lakini kama tutaweka asilimia 25 kwanza tutapata faida, wafanyabiashara wetu watafanya biashara na sisi tutapata faida nchi kwetu badala ya kupata asilimia 12.5 sasa tutakuwa tutapata asilimia 25 na wao watapata nafasi ya kufanya biashara na mapato yetu yataongezeka. Kuliko utaratibu huu ulivyo hivi sasa.

Nimuombe Mhe. Waziri pamoja na kwamba mnao utaratibu ambao mmejiwekea kwamba mtu tukimkamata mfanyabiashara alipe hivi, alipe hiki, alipe na adhabu hii. Mimi naona hili jambu tuliwache wazi kwa wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara. Mimi siamini kwamba tukiwaachia wafanyabiasha wakifanya biashara bidhaa ile ya mchele hapa itapungua. Bidhaa hizi zitaongezeka kwa sababu wao wataongeza zaidi. Kama wafanyabiashara walikuwa wananunua tani 100 au tani 200 kuleta hapa basi wataongeza *demand.* Wanajua wata- *supply* hapa na wata- *supply* Tanzania Bara na nchi yetu itafaidika kiuchumi. Wafanyabiashara wetu na wao wataongeza uchumi wao kwani biashara ni kuhangaika. Kwa hivyo tusiwape vikwazo wa kuwapiga penalti, tuongeze badala ya asilimia 12.5 basi iwe asilimia 25 kama ile inayotozwa kwa bidhaa zinazotozwa Tanzania Bara.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, pia kumekuwa kuna malalamiko kwa baadhi ya wafanyabiashara. Wale wanaokamatwa kwa njia ya magendo huwa hakuna utaratibu maalum wa hizo adhabu wanazopewa au malipo wanayopewa. Pamoja na kuwa wizara yako Mhe. Waziri umeweka utaratibu ambao wenyewe kiwizara ulikubaliana. Lakini kuna wafanyabiashara ambao wao wanalipishwa kadiri ya vile mlivyokubaliana. Lakini kuna wafanyabiashara wao wanapunguziwa. Wanalipa kiwango kidogo ya vile mlivyokusudia. Hii haikubaliki katika hali ya uongozi kwamba mwengine alipe kidogo, mwengine alipe kingi. Kumekuwa kuna malalamiko, nimuombe sana Mhe. Waziri tuweke usawa katika masuala haya. Tukikubaliana ilipwe asilimia hii kwa bidhaa hii, basi wote wale ambao watakamatwa kwa kuuza bidhaa hizi kwa njia ya magendo basi walipishwe vile ambavyo mmekubaliana.

La mwisho kuhusu Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC). Mhe. Mwenyekiti, Shirika hili la ZSTC ni Shirika letu ambalo tumeliunda kwa mujibu wa sheria. Sheria tumepitisha hapa, tumelipa mamlaka wake, majukumu yake, uongozi wake na mambo mengine mengi tu ambayo yapo kwa mujibu wa sheria. Lakini sasa Shirika hili Mhe. Mwenyekiti, limekuwa kama ni Idara ya Serikali. Hatujalipa nafasi yake kama Shirika, kwa kweli Mhe. Waziri hatulifanyii haki Shirika hili. Serikali tumekuwa tukiliingilia mno katika majukumu yake, hatulipi nafasi.

Shirika hili lina jukumu la kununua karafuu, lakini pia lina jukumu la kuuza karafuu, kwa mujibu wa taratibu tulilololiwekea. Katika suala zima la kuuza karafuu imekuwa Wizara ikiingia kila wakati, taratibu na kila kitu. Lakini hata kuuza karafuu nje tumekuwa tukiliingilia sana Shirika hili. Kwa kweli Wizara ni lazima iangalie utaratibu wa sheria.

Kama nilivyotangulia kusema kwamba shirika hili lipo kwa mujibu wa sheria na taratibu. Sisi Wizara kazi yetu ni kulisimamia hili Shirika, pale tutakapoona shirika linakwenda ovyo sasa ndipo sisi tutachukua *role* juu ya Shirika lile. Lakini tutakapokuwa tunaliingilia juu ya utendaji wake, litakapokwenda mchomo, lawama zitakuja kuwaangukia nyinyi Wizara. Kwa sababu kila kitu mnataka kuki – manage nyinyi wenyewe, masoko mnatafuta nyinyi wenyewe, manunuzi mnafanya nyinyi wenyewe. Hawa watu wa Shirika wafanyeje, wafanye kazi gani.

Mimi nimuombe sana Mhe. Waziri tuwaachie watu wa Shirika la ZSTC wafanye kazi zao. Mhe. Ismail Jussa ananambia tuwaachie watu wa Shirika hili wapumue ili wafanye shughuli zao wa Shirika, wapange mipango yao. Kuna taarifa kwamba hata bodi ya Shirika la ZSTC haipo, kuna Mwenyekiti tu ambaye ameteuliwa na Rais lakini hana wajumbe. Sasa bodi hiyo bodi gani, wajumbe wanateuliwa na Mhe. Waziri. Pengine Mheshimiwa pengine labda unachelea kuteuwa wajumbe pengine wakiteuliwa itabidi wafanye kazi zao. Lakini sio *fair* katika hali ya kidemokrasia lazima tufate utawala wa Sheria na Katiba ambazo tumejiwekea.

Bodi sheria imetungwa, bodi iwepo, isimamie Shirika pale ambapo wanahitaji msaada au Wizara mtawasaidia. Lakini isiwe sasa kila kitu tunafanya sisi Wizara. Au tubadilishe iwe Idara ya Serikali.

Kuna taarifa zisizo rasmi lakini Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho utatwambia. Kuna baadhi ya maofisa wako wamekwenda nje kutafuta soko la karafuu na kwa bahati wamelipata soko la kuuza karafuu. Wakatoa agizo kwamba zitayarishwe tani fulani zisafirishwe, lakini Wizara yako imezuia kuuzwa kwa hizo karafuu. Utakuja kutwambia ni kweli au si kweli.

Kama kuna sababu hizo zilizopelekea kuzuiliwa hizo karafuu ambazo tayari wale waliokwenda kutafuta masoko wameshakwenda basi uje utupe ukweli kwa sababu wewe ndio msimamizi na unafahamu juu ya jambo hili.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, juu ya kufungwa kwa masoko ya uuzaji wa karafuu. Tumetangaza kufunga masoko, lakini kinachoonekana bado wananchi wanazo karafuu ndani. Wanahitaji kuuza na sasa wananchi wanasikitika kwamba wanahitaji kuuza karafuu zao sasa hivi ili wapate fedha kwa ajili ya Ramadhani pamoja na Skukuu, lakini hawana pa kuuzia kwa sababuu masoko yamefungwa. Karafuu wanazo wanahitaji fedha wauze na sisi karafuu tunazihitaji lakini soko limefungwa.

Hapa kidogo panatupa shida. Tunapata shida sisi Wawakilishi wa wananchi juu ya utaratibu huu. Karafuu tunazihitaji, wananchi wanazo, wananchi wanataka kuuza karafuu zao ili waweze kupata mahitaji yao hasa katika mwezi huu wa Ramadhani na Skukuu, lakini hawajui wakauze wapi. Wananchi wale wakizichukua karafuu zile wakizipeleka Mombasa tutakuja kuwalaumu.

Wizara yako Mheshimiwa ambayo ndio inasimamia jambo hili ione umuhimu na kutafuta utaratibu mwengine badala ya kufunga moja kwa moja. Kuwa na utaratibu utakaowawezesha wale wenye karafuu zao waweze kwenda kuziuza ZSTC ili na sisi tupate karafuu na wao wapete fedha kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nitazungumzia kidogo mambo haya na kwa sababu hii Wizara iko chini ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, mchango wangu ni huo kwa Mheshimiwa Waziri, atusaidie ili tuone Wizara hii muhimu sana katika nchi hii inafanya shughuli zake vizuri kwa manufaa ya wananchi.

Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu Wizara hii ni yetu, tuichangie, tuijadili na hatimaye tumpitishie fedha ili Mhe. Waziri akaweze kutekeleza majukumu yake. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa afya sisi sote na kuendelea katika kikao chetu hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko, Alhajj Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, kaka angu, mwenzangu na tunatoka mbali sana.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba leo fani hii imenigusa na miye ndio niliyotoka nayo. Ningelipenda kumshauri kaka angu msikivu, ana hekma, ana busara, Mhe. Nassor. Kwa mpangilio wa makisio aliyotuletea kwenye Baraza hili la Wawakilishi na mimi nasema niko naye bega kwa bega katika masuala yote haya ambayo amekuwa ameyaelezea.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupitia wizara zinazohusika kama ya Biashara na Wizara ya Fedha kwa kuwafikiria Wazanzibari na Watanzania kwa jumla katika kuwaletea afueni katika masuala ya msamaha wa chakula uliotoka katika kipindi hichi cha miezi miwili.

Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Uzini kumshukuru Mhe. Rais, mpendwa wetu, mpenzi wetu kwa hili ambalo tunalokwenda nalo kwa kuitangaza ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuweza kutoa msamaha wa mchele 0%, unga wa ngano 0%, sukari 12.5% , na tende 0%.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara waliopata nafasi hii katika kuagizia chakula hichi napenda kuwashukuru nao ni akina Bombay Bazaar, Bopar, Turki, Simba Chai, na wote wafanyabiashara kwa njia moja au nyengine waliowezesha kufanikisha chakula kikawa kingi hapa Zanzibar yaani kwa maana ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na nafasi hii ningeliiyomba iendelee. Kwa kweli imewasaidia walaji katika afueni hii inayokuwa inatolewa.

Vile vile ningependa kuishauri Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda, ili kuondokana na zana potofu au kitu ambacho kinaleta hisia kwa wafanyabiashara. Barua imetoka tarehe 4 ya msamaha kwa wafanyabiashara wote aliyepelekewa Naibu Kamishna, lakini utekelezaji wake unaanza tarehe 5.

Napenda kumshauri Mhe. Waziri anapokaa na Wizara inayohusika hizi, nina imani kwamba lengo ilikuwa si kukomoana lakini kunaweza kuleta usumbufu kwa wafanyabiashara. Tarehe 3 Juni au tarehe 2 Juni, mfanyabiashara kaleta chakula hapa nchi ambavyo ni mchele, sukari, tende, unga wa ngano na akalipa, lakini baada ya siku mbili tatu ikatoka *exemption* ya kushtukizia. Ningeomba tuondokane na dhana mbaya, niya ni nzuri lakini ile *take over* yake. Nasema kufanya kosa si kosa kosa kurejea kosa. Lengo la serikali ni kuwahudumia wafanyabiashara wote ili wafanikiwe na kuwahudumia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Wito wangu kwa serikali na ushauri wangu kwa kaka angu Shekhe Nassor Mazrui, panapotoka suala la *exemption* basi itoke taarifa kwa umma kwa wafanyabiashara wote wadogo kwa wakubwa, kwamba serikali katika kipindi cha miezi mine ijayo tarehe fulani mpaka tarehe fulani chakula kitakuwa na msamaha kwa ajili ya walengwa kwa ajili ya wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, pamoja na Wizara zinazohusika kwamba tuwe waangalifu katika suala hili la msamaha na ni lengo zuri. Hili suala limefana na kwa kweli bidhaa hizi zimeweza kupata afueni.

Ushauri wangu wa pili kwa Mhe. Waziri wa Biashara ndugu yangu Nassor Mazrui, tunatoka mbali. Tunaambiwa wakati mwengine ukitaka kumchinja nyani usimtizame uso wake. Sisi wafanyabiashara nikiwemo pamoja na miye Raza pamoja na wenzangu. Tuwe waangalifu sana katika suala la chakula kwisha muda wake. Kwa kweli nataka kutoa wito kwako wewe Mhe. Waziri wa Biashara kwamba chakula tuwe waangalifu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuingia chakula ambacho kimekwisha muda wake na ukakifumbia macho Mhe. Waziri wa Biashara utakuwa unabeba jukumu mpaka yaumul Kiyama, tena hili tusilifanyie mzaha. Sisi sote ni binaadamu chakula kinapokuwa kimekwisha muda wake na tukaachilia wanaoathirika ni masikini za Mungu.

Mimi nataka kutoa wito hata ikiwa Raza kaleta chakula mimi mdogo wako, lakini Mhe. Mwenyekiti, namuomba Waziri wa Biashara na Viwanda suala hili ni suala nyeti amwambie tu samahani Raza rejesha chakula hichi. Kwa hivyo nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri awe muangalifu sana katika suala zima la vyakula vyetu vyote vilivyokwisha muda.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya uwezo wao mdogo nataka nikuhakikishie, lakini Wizara ya Biashara na Viwanda, kwa kupitia Waziri mwenyewe ambaye ndiye fani yake, ndio mfanyabiashara anatuelewa sote. Nina hakika jukumu hili anaweza akalifanya na Ishalla Mwenyezi Mungu atamsaidia. Pale atakapoona kuna uzito au shindikizo basi sisi wadogo zake tupo, ikiwa mwenzetu ataweka mawakili wawili sisi tutaweka mawakili ishirini kuhakikisha Wazanzibari wanapata chakula kilichokuwa hakijakwisha muda wake na ni chakula ambacho ndicho kinachohitajika kwa binaadamu kuweza kula.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu nije katika suala la biashara. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza katika Bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango suala la biashara. Mimi nataka kutoa ushauri kumwambia kwamba akae na Wizara zinazohusika nazo ni Wizara ya Makamo wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na yeye Mhe. Waziri wa Biashara na Masoko, pamoja angeliona kama kuna na wengine wanaweza kusaidia hili suala la soko.

Mimi nina ushahidi kwamba kuna bidhaa ambazo Zanzibar tunatakiwa tununue moja kwa moja. Lakini kwa sababu ya jina lile la Tanzania matokeo yake bidhaa hizi zinagharimu mara mbili au tatu mpaka kufika Zanzibar kwa mfano matairi na kuna biashara nyingi zipo. Sasa ningemshauri Mhe. Waziri kwamba suala la uchumi halimo ndani ya Muungano. Kwa hivyo ningeliomba katika masuala ya uchumi kwamba akae, wakutane na waziri anayehusika kwa upande wa Bara, wakae walijadili ili wawapelekee taarifa mabalozi wanaotuwakilisha sisi Tanzania nchi za nje na kutoa toleo maalum la kusema kwamba biashara ni uhuru kati ya Zanzibar na Bara katika suala zima la uchumi.

Namuomba Mhe. Waziri kwamba hili suala asilikalie na kuona kwamba wafanyabiashara wanaipata fursa hiyo. Kwa sababu kama tairi linazunguka wanaoathirika ni wenzetu wa daladala katika mazingira hayo. Ningelimuomba Mhe. Mwenyekiti, waziri angechukua hatua hii ambayo ingeweza kutusaidia sisi Wazanzibari kuongeza mapato. Vile vile kuwapunguzia gharama wale wanaoendesha gari kama daladala na magari ya michanga ndizo zinazotumika matairi haya ili kwa kuweza kusaidia.

Mhe. Waziri nataka nikuhakikishie sisi kama Zanzibar tunasema Tanzania ni nchi mbili huru zilizoungana kwa hivyo hapa hakuna Bwana. Kwa hivyo tunataka *fairness* katika Muungano wetu katika mambo ya uchumi. Lakini vile vile Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti vile vile nataka kumshauri Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti wakati mwengine wenzetu wafadhili Japan, Norway, Sweden, Marekani, Uingereza kutuletea chakula cha msaada kwa Tanzania kwa maana Zanzibar na Bara.

Mhe. Mwenyekiti chakula kile kinapofika Tanzania maana yake bandari ya Dar es Salaam, mara nyingi shara ya Zanzibar inaishia kwa watu wachache ushidi ninao, wanaofaidika chakula kile hakifiki Zanzibar, sasa Mhe. Waziri kwa sababu hili suala wanalielewa, ningelikuomba Mhe.

Mwenyekiti nimuombe Mhe. Waziri awe mwadilifu katika suala zima hili la chakula kije Zanzibar na wananchi wafaidike. Kwa hivyo utaratibu ule ambao unaokwenda wachache tu chakula cha Zanzibar kinamalizika kule kule watu wanatoa pesa kule kule, kinauzwa kule kule kwa kweli hatuwatendei haki wazanzibari wa Unguja na Pemba.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti katika kumalizia kwa jumla katika suala zima la biashara. Hivi karibuni kulikuwa na matatizo mengi katika masuala ya TRA biashara hizi za wafanya biashara wenzetu kwa hivyo mimi ningelishauri Mhe. Waziri kwamba hekma na busara na usikivu ziendelee. Mhe. Mwenyekiti ningemuomba Waziri wa Biashara anayehusika, wakae na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha ya Zanzibar, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kukaa na wenzetu kati ya Serikali na Serikali kuona usumbufu wa wafanyabiashara wenzetu ambao wanaohangaika katika masuala kupata riziki zao usumbufu huu unaondoka.

Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti matatizo ya biashara, matatizo ya muundo wetu huu wa muungano ni waandamizi tu wachache wakishakunywa kahawa sana huwa wanajisahau kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, wanaona kwamba ni jambo la kawaida. Kwa hivyo ningeliomba Mhe. Mwenyekiti kupitia kwa Mhe. Waziri wakaa na wenzake sisi wadogo zake tupo, uwezo wa hekima busara kuweza kumsaidia tunao ili kuona jinsi gani tunadumisha masuala ya biashara, lakini usumbufu kwa wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti hili linakuwa linaondoka kwenye taratibu.

Na mimi nawambia siku zote wafanyabiashara jamani Mhe. Mwenyekiti tuzungumzeni issue na term of reference, siku zote tukizungumza issue na term of reference hata wenzetu wakiwa bilioni moja sisi tukiwa watu watatu tutawashinda. Kwa hivyo wito wangu kwa wafanyabiashara tuwe waangalifu katika masuala yote ya biashara yote ya biashara katika kuzungumza matatizo yetu ambayo yanatukabili katika suala zima la biashara.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti niiombe Wizara ya Biashara na serikali kwa jumla suala la ukuaji wa viwanda. Nasema viwanda ndio uti wa mgongo wa nchi yetu kwa maana kwamba bila ya viwanda nchi haiwezi kuendelea. Kwa hivyo ningelipenda kutoa wito kwa wizara inayohusika suala la viwanda viweze kufanya kazi na kupewa insentive na naamini kwamba yakafanywa marekebisho kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, viwanda vinaweza kuleta maendeleo makubwa sana katika nchi yetu na hasa suala zima la ajira wafanyakazi, vijana wetu kupata ajira. Lakini vile vile katika soko letu kama tunavyojua historia ya Zanzibar ni biashara. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti ningetaka kutoa wito kwa wizara inayohusika isimamie hasa kwa wakulima wetu vile vile kuna wakati Mhe. Mwenyekiti ukenda marikiti matunda ya wakulima wetu utawaonea huruma hasa wakati wa msimu unapokuja wa machungwa, ndimu na vitu mbali mbali vya matunda wanavyokuwa wanaathirika wakulima. Hili linatia huruma sana, kwa hivyo mimi Mhe. Mwenyekiti ningelishauri kumpa ushauri wangu Mhe. Waziri wa Biashara kutizama njia gani ya kuweza kuwasaidia hawa wakulima wetu katika visiwa vya Unguja na Pemba, hasa msimu huu unapokuja wa embe, machungwa, ndimu, mabungo na mambo mengi ambayo tunaweza kuwasaidia jinsi gani ya kuweza wao wasiathirike. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti wanaoathirika sana katika matunda wanapokuwa katika msimu ni wakulima.

Utakuta mkulima kapalilia mti katunza shamba lake, kamaliza nguvu zake zote, njia za ndani hata gari la ng’ombe halipiti mpaka afikishe marikiti, pato analolipata yeye siku nyengine

chakula chake cha siku moja hakimfikishi kwa kile anachokuja kukiuza. Kwa hivyo mimi ninafikiri lengo letu sisi huku wawakilishi ni kuwasaidia walengwa na kuondosha kero za wananchi ambazo zinazowakabili ndipo tulipofika humu ndani Mhe. Mwenyekiti leo kuweza kuthubutu kwamba wananchi ndio waliotufikisha hapa kuweza kuwazungumzia maslahi yao binafsi.

Mimi vile vile Mhe. Mwenyekiti nimuombe Mhe. Waziri anayehusika kwamba hili wafanyabiashara wadogo wadogo wa mwani, wakulima na sehemu nyengine kama kutakuwa na utaratibu mzuri wa Wizara ya Biashara wa kuwasaidia hawa wafanyabiashara wadogo wadogo Mwenyekiti hawapati mikopo benki na hawana njia ya kupata benki. Wengine wanayo jitihada ya kuweza kukopa wakarejesha. Lakini kutokana na utaratibu wa dunia wa kibenki wa kuwezeshwa huchukua muda mkubwa.

Sasa mimi nataka nitoe changamoto kwa Mhe. Waziri wa Biashara, wafanyabiashara hao kama tuna hakika nao Mhe. Mwenyekiti mfano wa mwani, tunajua kwamba mfanyabiashara huyu msimu wake wa mwani ukulima wake una uhakika wa milioni kumi, basi serikali kupitia wizara inayohusika mimi ninamtegemea yeye Mhe. Waziri wa Biashara, kwa sababu namuona ni mtu msikivu, ana hekima ana busara na panapotokea jambo tunajadiliana. Mhe. Mwenyekiti nataka niseme mbele ya hadhara hii wakati mwengine huyu hutokezea matatizo tunakutana nyumbani kwake mimi, tunakaa ninamwambia Mhe. Waziri endelea na biashara kwake ninakwenda nakaa nae katika lengo lile lile la kuwasaidia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba na kuweka maslahi ya nchi mbele.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti suala hili langu mimi la biashara la kuwasaidia wakulima, kulima nina hakika wanapata katika msimu milioni kumi lakini anahitajia milioni mbili kununua dawa, kununua mambo madogo madogo ili yamuwezeshe bidhaa zake zile ziweze kufaidika zaidi na kupata nguvu hana na pahala pa kwenda kukopa hapana. Sasa yule mkulima tunaweza kuwaumiza sana, wakulima wapo wengi wana jitihada.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti natamka wazi mbele ya Baraza lako hili mimi kufika hapa nilipofika kama mfanyabiashara leo nikawa mwakilishi sijaambiwa na wazee wangu kwamba Raza nitakuja kuwa mwakilishi au mfanyabiashara ni jitihada ya wenzangu ndio iliyonifikisha hapa nilipofika. Sina nguvu ya kufikia hapa niliyofika na wananchi ndio walionifikisha hapa. Kwa hivyo kwa niaba ya familia yangu niko tayari kuwaazima Wizara ya Biashara chini ya Nassor Mazrui niko tayari hata kesho kuwasaidia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba wakulima wenye mifuko kama kuku, mwani na mengine niko tayari hata kesho Mhe. Waziri akinambia nikabidhi milioni mia mbili nitamkabidhi bila masharti kwa niaba ya familia yangu bila ya riba, bila ya chochote, ikafika mwaka anirejeshee cheque yangu kama nilivyompa. Lakini fedha hizi zilengwe kwa wahusika wakuu yaani nasema wakulima sisi ndio tulitoka kule. Tumetoka kwenye grass root tunawataka wakulima na wafanyabiashara wadogo watoke grass root ili wafike hapa tulipofika sisi.

Mhe. Mwenyekiti napenda Baraza lako tukufu na wananchi wa Jimbo la Uzini naunga mkono kwa niaba yangu na wananchi wote wa Uzini asilimia mia moja na kumi wa Bajeti na Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda kaka yangu Mheshimiwa pamoja na ungozi mzima aliokuwa nao kuwatakia maisha mema na ninaamini kwamba hayo tuliyoyatamka na haya

aliyoyazungumza ndani ya kitabu hiki amebeba jukumu na uongozi ni dhamana, uongozi ni hekima, uongozi ni halbadiri.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana wataala aliyetuwezesha hapa tukiwa hai tukiweza kupumua na tukiwa katika ramadhani ya 17, kubwa tuongezee bidii kumcha Mwenyezi Mungu. Vile vile nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sijakushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mawili matatu katika bajeti hii muhimu ya Wizara ya Biashara. Vile vile nataka niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mtoni kwa uzalendo wao, kwa umakini wao, kwa umahiri wao kwa kumchagua Mwakilishi mahiri kabisa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa vile hakuwafanya kosa, wamemuona mbali.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti nichangie katika ukurasa 48, Idara ya Maendeleo Viwanda. Mhe. Mwenyekiti kwanza nimpongeze kwa mpango wa kufanya mapitio ya sera ya maendeleo ya viwanda ikiwemo kuchunguza vikwazo vya maendeleo na viwanda na kutathmini mazingira ya uwekezaji katika viwanda, tatizo sio sera wala tatizo kubwa ni mipango madhubuti ya utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti tulikuwa tukijipanga si zote tulikuwa na maeneo huru hatukuona uhuru wake uko wapi, maeneo ya bandari hatukuyaona, wenzetu wa Bara wanaendelea kila leo kwa hivyo hatujafika pahali popote kwa maeneo hayo mpaka muda huu. Kama nchi ndogo kama hii Zanzibar inatakiwa na vipao mbele viwili au vitatu, lakini sioni utekelezaji wake. Kuna msemo unaosema shona koti kwa ukubwa wa kitambaa chako.

Muelekeo wa viwanda Mhe. Mwenyekiti unasikitisha viwanda vimekufa na watu wamepoteza ajira nyingi sitegemei kama tunaweza kufungua kiwanda kwa mujibu wa sera tunazokwenda nazo sasa Zanzibar. Kulikuwa na viwanda vidogo vidogo wengine wamevifungua wamevihamisha kutoka Tanzania Bara. Vijana wetu wamekosa ajira, serikali imekosa mapato kwa kuwa hapana umakini na ukizingatia zaidi umeme, umeme wenyewe tunautegemea kutoka Tanesco, kama hatujabuni mbinu nyengine za kuendeleza uchumi wetu hapa itakuwa bado mtihani wa kuja kumuweka muekezaji. Halafu hawa wawekezaji wakati mwengine wanabughudhiwa kupita kiasi, ikiwemo ZRB.

Nije katika Idara ya Biashara na Uendelezaji Masoko ukurasa 65. Mhe. Mwenyekiti katika biashara na masoko ni muhimu sana na bidhaa nyingi zinazotengenezwa Zanzibar package yake bado matatizo hasa ya wazalishaji wetu wa zanzibari, jambo ambalo linawasumbua sana kutokana na ubora wa bidhaa hizo. Lakini la kusikitisha hapa Mhe. Waziri kidogo nitahitaji maelezo, Zanzibar inanufaika vipi na soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati tunashindwa hata kuzalisha sindano. Hii si itakuwa si ndoto tu Mhe. Waziri?

Sehemu nyengine ninayotaka kuchangia Mhe. Mwenyekiti Shirika la Magari. Shirika la Magari limekufa na tusimtafute mchawi, mchawi ni serikali yenyewe. Leo serikali inataka kuagiza magari ipite mitaani kununua magari. Tuwaangalie wenzetu Tanzania Bara Mhe. Mwenyekiti

wana utaratibu mzuri wa kununua vitu vya serikali. Leo serikali yetu hapa ikitaka kununua gari basi ipite mitaani.

Ukaguzi wa biashara ukurasa wa 40 Mhe. Mwenyekiti, suala hili la mafuta siku zote nimekuwa nilipigia kelele kuelezwa msimamizi ni nani? Lakini jawabu yake haipatikani kuna vitengo vitatu hapa. Kuna magari yamekufa vibaya kutokana na kiwango cha mafuta yanayoleta Zanzibar. Kodi inakusanywa ZRB, ukenda huku unaambiwa wizara ya Ardhi Makaazi na Nishati, ukaja huku Wizara ya Biashara hebu hapa tupate ufafanuzi Mhe. Waziri nani msimamizi mkuu wa hii wizara ya Mafuta.

Utaratibu wa kuingiza mafuta mafuta sasa hivi hayapimwi tofauti na utawala wa awamu ya tano, palikuwa na mtaalam,u ikaja meli ya mafuta hapa kutoka Bara wakaja wakayapima mafuta yale hatukuwahi kusikia tatizo la mafuta kwa kipindi hicho cha awamu ya 5. Hapa Mhe. Mwenyekiti nitahitaji maelezo hili jengine Mhe. Mwenyekiti sikutumwa na wananchi wa Jimbo la Muyuni tu hili na wananchi wengi wamenituma juu ya suala hili. Shirika la Kusimamia viwango vya Ubora ikiwemo vyakula Zanzibar vilivyo standard, Mhe. Mwenyekiti imepitishwa sheria hii katika Baraza lako hili lakini utekelezaji wake bado unachechemea.

Wananchi wengi hivi sasa wameliwa manapata maradhi hasa stroke na hii inatokana na wataalam kusema, vyakula vimekuwa viki-expire. Mhe. Hamza alikuwa akizungumza siku zote hapa tumekuwa tukiongoza kupitisha sheria utekelezaji wake haupo, wananchi wetu wanyonge wanaumia. Hili Shirika la ZBS mpaka leo utekelezaji wake hatujauona sijui ofisi yake iko wapi, sijui lini itaanza kazi, sijui wataalam wangapi wameshapatikana mpaka muda huu Mhe. Waziri.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti nije katika suala la mchele. Hivi sasa wafanyabiashara wetu wamekuwa na kilio kikubwa cha mchele lakini sasa hivi mchele umekuwa hautoki, wafanyabiashara wetu wanaumia katika mzunguko wao. Sasa mchele utafika kuharibika hauna pa kupelekwa. Ingawa wamepata msamaha lakini wafikiriwe huku wenzetu huwa wanaekewa vipa umbele leo serikali haiwezi kukopesha. Leo tunajikamua wenyewe mchele ule unataka kuuzwa uzunguke iletwe sukari, sukali ile inataka kuzalishwa uletwe unga wa ngano. Lakini mchele umekuwa mwingi hawajapatiwa soko suala hili hapa pamekuwa na kizungumkuti Mhe. Mwenyekiti hawa ndio tunaowahitaji, kama tunafanyabiashara hapa tutakuja kupata mtihani. Hivyo vifungu vya kuja kupitisha hapa vya viburudishaji na vinywaji vitakuwa havipatikani bila ya kufanya biashara.

Leo tutizame wenzetu Dubai kuna Wachina wamewekekewa eneo mbali kabisa linaitwa Dragon market hawabughudhiwi wale watu, sasa hapa Mhe. Waziri tuwafikirie wafanyabiashara wanaitumikia nchi yao.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti nimepata kuuliza hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na baada ya kunihamisha eneo ambalo nimekwenda kutembea umenikumbusha, nimejisahau kama si eneo langu. Mhe. Mwenyekiti naomba nichukuwe nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea hotuba yake nzuri hotuba ambayo imejaa matakwimu ambayo ni ya kitaalam.

Mhe. Mwenyekiti nianze hoja yangu kwenye mapato na matumizi ya mwaka jana. Mhe. Waziri amekiri na ndivyo ilivyo mwaka jana tulimuidhinishia bilioni 2.7 kama fungu zima la wizara yake. Mhe. Mwenyekiti kwenye fedha hizo shilingi milioni mia tatu zilitengwa kwa ajili ya maendeleo na milioni mia mbili kama asilimia sitini na saba zilikuwa zimelengwa kwenye viwanda vidogo vidogo na vikundi vya ushirika. Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri anielimishe fedha hizi milioni mia mbili kama asilimia sitini na saba ya fungu la maendeleo zimewafikiaje walengwa kwa maana ya viwanda na vikundi vidogo vidogo vya ujasiri amali. Mtu wa kawaida kama mimi nikitaka kuiona hii shilingi milioni mia mbili nende nikaangalie wapi kwenye viwanda na kwa hao wajasiri mali wadogo wadogo ambao tunao kwenye maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti nachukua nafasi hii niyapongeze majimbo matatu kwa kukuwakusanya wananchi kwenye suala zima la ujasiri amali na Jimbo la kwanza ambalo limefanya katika hatua hiyo ni Jimbo la Mtoni Unguja. Mhe. Mwenyekiti viongozi wa Mtoni wamehamasika na kushajihisha wananchi kwa ajili ya kuandaa vikundi vidogo vidogo vya ujasiri amali ikiwa ni viwanda vidogo vidogo na uvuaji samaki. Sasa mimi kama mwakilishi ningetegemea fedha kama hizi zingewafikia watu wale kwa ajili ya kuleta maendeleo yao. Sasa Mhe. Waziri anambie fedha hizi zimeenda wapi ili mwananchi wa kawaida kama mimi niweze kuziona fedha ambazo zimetengwa shilingi milioni mia mbili kwa ajili ya viwanda na wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti hoja nyengine ni Idara ya Mipango na Sera, naomba kupata maelezo juu ya uuzaji wa magodown na kiwanja eneo la Mtoni Unguja karibu na kiwanda cha Bahresa. Mhe. Mwenyekiti pale pana maeneo ya serikali ambayo yako chini ya Wizara hii ikiwa ni eneo la kiwanja pamoja na magodown sasa nataka kujua je, wizara waliyauza kwa kiasi gani na kiasi gani kimeingia kwenye serikali kama mfuko wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti hoja nyengine ni malamiko ya wafanyabiashara kwenye ukurasa wa kumi paragraph ya kumi na sita, Mhe. Waziri ametuonesha bado ana dhamira ya kwenda kuzungumza kuhusu kero za wafanyabiashara. Mimi naendelea kusema kwamba hatuwezi mara zote kuidhinisha fedha kwa ajili ya mazungumzo ambayo hayana tija. Mhe. Mwenyekiti haiwezekani kwamba tumeshindwa kutatua kero miaka 48 baadae tuendelee kutenga fedha kuwapa wataalam wakazungumze makero ya biashara wakati hayana ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti mimi niwashauri sana wawakilishi wenzangu kwamba tusiruhusu tena kuidhinisha fedha kwa ajili ya kwenda kufanya mazungumzo kwa kisingizio cha kero za muungano jambo ambalo hakuna ufanisi. Mhe. Waziri anajua kwamba hivi sasa magari tu Dar es Salaam yapo zaidi 300 wafanyabiashara wa Zanzibar wamelipia ushuru halali, lakini wanaendelea kutozwa tena ushuru mara ya ile bei Zanzibar wametozwa. Mhe. Mwenyekiti mimi kwa ushauri wangu sioni msingi kabisa wa kwenda kuzungumza masuala ya kero hizi za muungano kero ambazo ufanisi wake hakuna na badala yake ni kufuja fedha za walipa kodi wanyonge wazanzibari ambao kwa kweli Mhe. Mwenyekiti wanazihitaji sana kwa mipango ya maendeleo na shughuli zao za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti hoja nyengine ni Shirika la Magari tumemsikiliza Mhe. Waziri kwamba kuna mpango wa kulifuta Shirika la Magari na bila shaka ni kwa hoja za kitaalam. Mhe. Mwenyekiti mimi niombe tu wizara kabla ya kuamua uamuzi huo, wafate sheria ile ya utumishi kukaa na wafanyakazi na watendaji wa lile shirika kuelimisha na kuelewana ili kuepusha migogoro huko baadae. Na baadae wizara ikiona kuna haja ya kulifuta kwa hoja za kitaalam Mhe. Mwenyekiti basi mimi sina pingamizi lifutwe kwa sababu bila shaka shirika linakuwa halizalishi kiasi hicho, lakini kufutwa maana yake tayari wamezungumza Wizara na wafanyakazi wa shirika lile ili kuondosha migogoro ambayo baadae inaweza kutokea.

Mhe. Mwenyekiti ZSTC Mhe. Salmin amezungumza kwamba hatujui hatima ya karafuu zilioko Pemba ambazo zinavunwa kwa nguvu na wakati huu mwezi wa ramadhan wananchi wanataka kupata fedha kwa ajili ya sikukuu. Lakini suala la bodi ya shirika Mhe. Waziri atwambie kwa nini Mhe. Rais ameteua mwenyekiti lakini hadi leo hatujaweza kuteua wajumbe wa bodi kwa ajili ya kusaidia ZSTC ili liweze kuwa shirika makini lenye kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti pia sisi kama ni wawakilishi tusingependa kusikia migongano baina ya watendaji wa wizara kwa kisingizio ya kutafuta bei za karafuu. Mimi imani yangu kwamba ikiwa kuna bei ya karafuu iliyotafutwa, basi itakuja wizarani kwa ajili ya kupata Baraka za wizara na hatimae serikali bila shaka itaamua kuuzwa kwa karafuu. Lakini hata bei ikiwa nzuri kiasi gani hatuwezi tu mtendaji mmoja akaamua kuuza karafuu, bila ya kupata Baraka ya wizara bila ya mashauriano na wizara nzima.

Mhe. Mwenyekiti nimalizie mchango wangu kwenye mafungu. Mhe. Mwenyekiti naomba Mhe. Waziri anisaidie fungu 0401 Idara ya Mipango na Sera kasma 220509 kuna ada ya ushauri. Mhe. Mwenyekiti bajeti ya mwaka jana 2011/2012 kulikuwa hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ushauri lakini bajeti hii wametenga milioni thathini na nane kwa ajili ya ushauri, anambie ushauri gani mwaka jana walioukosa na ukawaharibia kazi zao hata mara hii wakaamua kutenga milioni 38 kwa ajili ya ushauri. Mwaka jana kulikuwa hakuna pesa wizara imekwenda vizuri. Mara hii wanategemea kupata ushauri gani mzuri zaidi ili watenge fedha hii milioni 38. Mhe. Mwenyekiti hii fedha ni nyingi lazima tupate maelezo ya kina wanategemea kupata ushauri gani wa ziada kwa ajili ya kuendeleza Wizara yao.

Mhe. Mwenyekiti kasma nyengine ni kasma 220517 utayarishaji mpango wa bajeti. Mhe. Mwenyekiti mwaka jana kasma hii ilitengewa milioni nane laki tisa mara hii imetengenewa milioni 32. Mwaka jana bajeti tayari imetengwa na mimi nasema kwamba ni bajeti nzuri inaonesha kitabu kizuri kina wataalam sasa watwambie basi kwa nini wakaamua kuongeza fedha milioni 32 kwa ajili ya mpango wa bajeti, kipi kipya ambacho mara hii watakifanya ili tuweze kushawishika fedha hii tuwazidishie. Ni fedha nyingi ni mara nne ile ya mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti fungu jengine ambalo naomba ufafanuzi ni 0501 Idara ya Viwanda kasma 220601 ni ununuzi wa mapazia mazulia na makapet. Mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni mbili, mara hii ni milioni ishirini laki sita hamsini na moja, watwambie basi kuna kipi kilichoongezeka cha ziada ili kutoka milioni mbili mpaka ishirini wameamua kutenga kwa ajili ya kununua mapazia na makapet.

Idara nyengine ni Idara ya Biashara. Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti walitenga milioni hamsini na tano kwa ajili ya safari za ndani na nje mara hii wametenga milioni sabiini na moja. Mhe. Mwenyekiti nadhani sasa ni utandawazi unaweza ukaa kwako ukaona shughuli zote za kibiashara dunia nzima. Safari hizi ambazo zinatengewa milioni 71 Mhe. Waziri atusaidie tuangalie sera gani hawezi kuiona kwa mtandao ambao sasa hivi umeenea dunia nzima. Mwaka jana waemetia milioni 55 mara hii wameona kidogo wameamua kutia milioni 71 kwa ajili ya Idara ya Biashara kwa safari za ndani na nje ya Idara hii. Mhe. Waziri hapa pia anisaidie ili nishawishike kuidhinisha fungu hili kipi ambacho wanakusudia kukifatilia kwa milioni 71 zaidi ya mwaka jana milioni 55.

Mhe. Mwenyekiti, idara nyengine ni Idara ya Utumishi. Kuna kasma 211110 Posho Maalum. Mhe. Mwenyekiti, posho maalum hapa limepanda kwa shilingi 140,700,000/-, najua mshahara wa watumishi hawa ni shilingi 295 milioni lakini nusu yake ni posho maalum. Mhe. Waziri hebu tusaidie posho hili limepanda kiasi hiki kwa sababu ya nyongeza ya mshahara tuliyoipata au kuna kazi nyengine ya ziada ambayo mnakusudia kuifanya ili nusu ya mshahara ni sehemu ya posho maalum ya wizara hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi safari za ndani na nje ni shilingi 101 milioni. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imetengewa shilingi 101 milioni kwa ajili ya safari, Mhe Waziri nadhani utusaidie ni safari zipi za ziada ambazo unakusudia kuzifanya ndani ya idara hii ili Wazanzibari waone ufanisi wa wizara yako.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba Wazanzibari wanategemea wizara hii ni wizara ambayo inawagusa wananchi moja kwa moja, ni wizara ambayo inagusa maisha ya wananchi. Niungane mkono kabisa na Mhe. Mohamedraza Hassanali kwamba Mhe. Waziri asiruhusu kwa namna yoyote ile wafanyabiashara kuingiza chakula kibovu kwa kisingizio chochote kile. Kwa sababu hili litateketeza jamii yetu, litadumaza akili zetu na litasababisha maradhi kwa wananchi wetu.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akinijibu vizuri kwenye hoja zangu nitaunga mkono bajeti hii. Nakushukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuweza kutujaalia kuwa hai hadi leo hii na kufika katika Baraza hili kuweza kuzungumza lolote kuhusu Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Ama mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema Mtume Muhammad (S.A.W) nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri jinsi ya alivyowasilisha hoja yake, kwa kweli hoja yake kaiwasilisha vizuri mno na nimevutika zaidi Mhe. Mwenyekiti, kwa zile dua alizotuombea. Kwa kweli dua zake *Inshaallah* Mwenyezi Mungu azikubali, na ni matarajio yangu kwamba dua zake *biidhnillahi* zitatakabaliwa na pamoja na yote hayo nadhani Wajumbe wakitoka nje japo tuende watapata kutoka kwake. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naona niende moja kwa moja kwenye hoja.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa *introduction* ndogo juu ya hili zao la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, tangu zamani sasa na hapo baadae ni matarajio yangu kwamba zao la karafuu litaendelea kuwa muhimili wa uchumi katika visiwa hivi. Lakini hadi sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tunavyozungumza ni kwamba inaonekana kwamba serikali inanufaika zaidi na karafuu kulikoni mkulima, kwani hadi leo hii bado serikali inaendelea kuhodhi hili zao.

Mhe. Mwenyekiti, huku serikali ikiendelea kuhodhi hili zao wakulima wanaendelea kupata shida siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, wakati Wasukuma wanajisifu kwa kundi la ng'ombe walilonalo na kuondoa matatizo yao kupitia ng'ombe wao pale wanapokuwa na dhiki, wakati maprofesa mara nyingi hujinasibu kwa zile *lectures* wanazotoa katika Vyuo Vikuu pamoja na tafiti wanazofanya, wakati wafanyabiashara wanajinasibu na kujisifu kupitia misingi ya biashara zao, basi sisi Wapemba hujinasibu kwa mashina ya mikarafuu tuliyonayo pamoja na karafuu kavu tulizonazo katika majumba yetu.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha kwamba Msukuma hivi sasa akitokewa na shida tu anakwenda kuuza ng'ombe wake, Mfanyabiashara akitokewa na tatizo tu anaangalia *asset* zake anasukuma kidogo anapata fedha, lakini hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna sisi Wapemba ambao tunaweka karafuu zetu majumbani mwetu kwa ajili ya kuja kutufaa kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan hadi leo hii magunia ya karafuu yameganda ndani hatuna wa kumuuzia.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni unyanyasaji mkubwa, tatizo liko wapi, tatizo serikali haina pesa au tatizo ndio hilo kwamba hakuna soko? Ikiwa tatizo serikali haina pesa basi wapo watu ambao naamini na washaanza kujitokeza hapa, mambo ya kukopesha kopesha naamini wamo wengi basi ikakope serikali inunue karafuu. Hapa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali keshasema yeye uwezo wake na kuna Bakhressa na yeye, kuna nani, kuna na hata huyu rafiki yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaweza kukopesha ikiwa pesa za kununulia karafuu hamna basi kopeni kwa watu binafsi msituuwe na njaa Wapemba jamani.

Sasa ikiwa tatizo ni soko tujue, kwa sababu kama tatizo ni soko ondosheni wale KMKM pale Baharini wiki moja tu basi Wapemba wataliona soko lilipo, nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, ikiwa vyombo vya ulinzi vitaondoshwa barabarani kama nyinyi serikali hamlijui soko lilipo basi ondoshani vyombo vya ulinzi mle baharini basi Wapemba kutoka Mtambwe, kutoka Nyali, kutoka Vitongoji, watajua soko la karafuu lilipo msituuwe kwa njaa jamani. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni *introduction* ya hoja yangu.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi katika ukurasa wa 31 na 33 Mhe. Waziri amezungumzia juu ya kuwepo kwa Mfuko huu, ukurasa wa 31 nadhani Waziri amezungumzia azma ya serikali ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu. Mheshimiwa Mfuko huu ni muhimu sana, Mfuko huu kwa ajili ya Maendeleo ya Karafuu ni muhimu sana, kwa sababu naamini huu Mfuko utakapoanzishwa utaondoa matatizo mengi, wakulima wa karafuu tuna matatizo mengi.

Hivi sasa nyinyi serikali mnawaletea tu pale *ZSTC* kununua, lakini *the whole process* mpaka karafuu inakauka na kuletwa *ZSTC* kuna mambo mengi keshakutana nayo mkulima hapo. Hivi tunavyozungumza Mhe. Mwenyekiti, hakuna bima ya afya kwa yule anayeanguka mkarafuu, vitanda vya uangukaji mkarafuu kwa sababu mara nyingi tunapoanguka mikarafuu huwa tunaumia sehemu za migongo, lakini tukifika Hospitali ya Mnazi Mmoja vitanda vilivyopo ni

vile vile anavyolazwa aliyepasuliwa mshipa. Hakuna vitanda vya muangukaji mkarafuu. Sasa mimi nadhani Mfuko huu unaweza ukatatua tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko huu tunauhitaji sana nadhani na Mhe. Waziri katika hili tuko na wewe bega kwa bega katika hili. Kwa sababu huu unaweza ukatuweka salama pale ambapo mashamba yetu yanaungua kwa moto. Mhe. Mwenyekiti, hutokezea kipindi cha kaskazi ambapo kunakuwa na *natural fire*, moto tu unatokezea wa maumbile pale kwenye mashamba ukaona mashamba yameteketea, hapo yakishateketea mikarafuu 300, 500 utaona imeungua matokeo yake hapo atakuja Mhe. Rais na Waziri kuja kukuhani na baadae watakugaia pesa mbili tatu hao wameshaondoka wewe unaanza kuteketea kwa njaa. Lakini naamini utakapokuja Mfuko huu ukafanya kazi vizuri basi katika jambo moja litakalosaidia ni yule mkulima kuwezeshwa kuweza kurudisha upya shamba lake na hatimaye kujipatia kipato. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi tunaomba Mfuko huu na tunauhitaji sana na Inshaallah Mwenyezi Mungu ajaalie ufanikiwe kuwepo kwake.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kuhusu mkarafuu, juzi hapa niliwauliza jamaa wa kilimo lakini wakanijibu ndivyo sivyo, leo nataka nikuulize wewe Mhe. Waziri na wataalamu wako huko, mbali na mambo ya biashara nadhani mnaweza mka *study* au Zanzibar tunaweza tukapata *quality* na *quantitative cloves*, tunaweza tukapata hivihivi kwa kupitia utaalamu?

Kwa sababu niliwambia jamani mikarafuu ndio tunawauzia karafuu lakini mikarafuu haipandiki imeshakuwa mirefu mno, na ukiupanda leo utachukua miaka minne, mitano au sita lakini baada ya muda ushachonjoroka tena ushakuwa mrefu vile vile. Na wachumaji wakubwa wa karafuu ni wanawake, hawaiwezi tena mikarafuu na sisi wanaume tunalegalega miguu hii. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nauliza jambo moja hivi nyinyi serikali baada ya kuumiza kichwa kupitia wataalamu mmeshindwa kuleta *high breed* ya mkarafuu mwengine, ni ule ule aliouleta Saleh Buhamerel *Century* ya 16 hadi leo hii, wakati Mhe. Aboud Jumbe hapa Rais wa Pili yule mzee mimi nampongeza sana, jamani *old is gold* na kila linalofanywa na mkongwe musifikirie kwamba ni bara, mengine ni mazuri waigeni hawa wakongwe kina Mzee Mjumbe.

Mhe. Aboud Jumbe alikuja akauangalia mnazi ule wa *East African Tall* huu tulio nao hapa Zanzibar akauona kuwa mnazi huu kwa kweli wakwezi ni jamaa zake Mhe. Hija Hassan Hija pale hawauwezi tena. Sasa akaleta *high breed* kutoka Nigeria, ilikuja minazi kutoka Nigeria ingawa ina *short life span* lakini *production* yake inakuwa kubwa. Sasa pamoja na kwamba hizi *high breed* zina *short life span* lakini *production* inakuwa ni *very high* kama mtaishughulikia. Sasa Waheshimiwa tatizo liko wapi kwa mkarafuu jamani, hebu tuazimeni sisi serikali kidogo *back bencher* hapa muone tutakavyofanya vitu vyetu.

Waheshimiwa mimi nadhani ikiwa mtaumiza kichwa wataalamu vizuri basi tunaweza tukapata *high breed* ya mkarafuu na hata kina Mwasike pale sehemu za Mwambe akaweza kuupanda, lakini sasa hivi mikarafuu iliyoko mpaka uwe na pingu na hapo uje uanguke ndio mara nyingi tukianguka mikarafuu ya siku hizi hatutibiki tena na vigari vya walemavu hamtuletei bure inabidi mtu akishaanguka anunue kigari cha walemavu alimradi mashaka tu. Mimi nadhani mjiangalie upya serikali, mimi naamini tunao wataalamu wa kutosha kabisa wa kilimo, tunao maprofesa wengi Vyuo Vikuu, ikiwa mtaweza kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi tukaja

tukauona huu mkarafuu wetu jamani hatuwezi kupata *high breed*, inawezekana bwana elimu imeongezeka inawezekana sana, hilo ni jengine Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe naomba nikujulishe una dakika tano za ziada.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, katika huu huu mkarafuu katika hii *drying system*, ukaushaji. Ukaushaji mara moja niliuliza nikaambiwa hizi zinatakiwa zikauke kwa jua tu, tunakula hasara sisi siku za mvua kwa kuuza karafuu mpeta, jamani hebu fanyeni utaalamu ikiwa ni kwa jua basi fanyeni *mechanism* ya kuweza kuuchukua huu muangaza wa jua mkau-*store* halafu siku za masika mkafanya *radiation* ya kuzikausha hizi karafuu kusudi tukaepukana na mpeta wa mumo kwa mumo. Hilo jengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na hizi dakika tano ulizoniongeza naomba moja kwa moja sasa niende katika suala zima la ukurasa wa 32 na 35 ambapo Mhe. Waziri amezungumzia kuhusiana na suala zima la utaratibu wa kutoa leseni, waziri amezungumzia mfumo mpya wa utoaji leseni. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kama kuna suala zuri ni hili, mfumo uliopo sasa umepitwa na wakati sijui mnatumia vigezo gani katika kutoa leseni.

Katika MKUZA Mhe. Menyekiti, wewe utakumbuka hata Rais hapa naye alikuja akasema kwamba, kwenye MKUZA imesisitizwa kuwa wananchi wawezeshwe kusudi waweze kupunguza umasikini na kujiongezea kipato na wakati tunafungua Baraza hili Mhe. Rais alisisitiza serikali kuwahamasisha watu kujiongezea kipato na kupunguza umasikini. Lakini sasa hivi tatizo katika wizara yako Mhe. Waziri mfumo ulionao ni wa ubaguzi katika kutoa leseni, iweje wale jamaa wenye makontena pale wanajiita JUWEMADA pale Darajani, Jumuiya ya Wenye Makontena Darajani, tangu mwaka 2011 mpaka sasa hivi hawajapewa leseni wale, mtawaua wale watu kwa sababu huwezi kwenda nje.

Biashara wanazoziuza wale Mhe. Mwenyekiti, zote zinanunuliwa nje ya nchi, hizi nguo sisi hatuna viwanda vya nguo hapa lazima wale wasafiri na wakenda Wizara ya Mambo ya Nje kutaka *visa* wanaambiwa waoneshe leseni na leseni hamuwapi hiloni tatizo Mhe. Waziri. Ninachokwambia Mhe. Waziri wale pale JUWEMADA wana jumuia yao ina maduka 93, maduka haya ni kwamba kila duka lina mmiliki mmoja na wafanyakazi wawili, kwa hivyo kila duka limetoa ajira kwa watu watatu. Sasa ukiangalia hapa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba 93x3 ni sawa sawa na 279, yani pale Darajani yale makontena tu yameajiri watu 279. Sasa hawa hawapewi leseni wanachofanya ni kunyang'anywa, hununua fomu za kujaza kuomba leseni wakishajaza zikapita kwa Madiwani kupata baraka, zikishapita kwa Madiwani zikishafika *ZMC* pale kwenye mamlaka ya kupewa leseni hawapewi leseni, wakati *ZMC* hao hao kwa kila duka wanakusanya kila mwezi shilingi 9,500 huku hawawapi leseni. Halafu angalia kwa mwezi karibu shilingi 883,500 wanakusanya hawa ZMC wanataka nini tena hawa wanawanyang'anya wenzao hivi hivi kwa nini hawawapi leseni.

Mhe. Mwenyekiti, ni ubaguzi, hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa mimi napenda sana tena niendelee kusifu viongozi wetu wa nyuma hawa walituunganisha pamoja wale wanabaguliwa kwa nini. Wale jamaa walio na maduka pale Darajani na Makontena wanabaguliwa kwa nini, kwa sababu wako Mjini Magharibi au kwa sababu ni Wamakunduchi, au kwa sababu ni Watumbatu, au kwa sababu ni Wapemba, watupe hawa *ZMC* kwa nini hawawapi leseni.

Hii serikali yetu ni ya umoja wa kitaifa wazee wetu walijenga misingi Mzee Jumbe na Mzee Karume hapa ya umoja, Mzee Karume alikuwa hana Uunguja na Upemba yeye, hata ukiniangalia naomba nitoe mfano katika nyumba alizokuwa nazo nakusudia hawa mama wawili walitokea Pemba katika kuletwa Umoja wa Kitaifa Mzee Karume wake wawili amechukua Pemba; na Mzee Jumbe hivyo hivyo na yeye kaoa Pemba ili kuleta umoja wa kitaifa, sasa kwa nini wale wenye makontena mnawanyanyasa pale, ni tatizo? *Is this a Government of National Unity*? Tunatakiwa tulete *harmony within the isles, why* mnatukamua?

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani endelezeni misingi iliyosimikwa na Mzee Jumbe na Mzee Karume ili kuleta umoja wa kitaifa. Wale watu wa makontena pale Darajani ni Wazanzibari wana haki sawa na Wazanzibari wengine, iweje wao wakitaka leseni za maduka wasipate wakati waliopo Jongowe wanapata, walioko Kusini nao wanapata, walioko Vitongoji wanapata kwa nini wale tu? Naomba Mhe. Waziri utakapokuja unieleze kwa hili baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu naomba nikae chini.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini hoja hujaunga mkono bado.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Naunga mkono hoja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuwa katika hali ya uzima. Lakini pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia wizara ambayo ni nyeti. Nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri jinsi hotuba yake ilivyojipanga na akaeleza kinagaubaga mambo yote katika hotuba hii, na ni imani yangu kwamba hii wizara imepata mwenyewe. Sasa kikubwa nitachokiomba hapa ni watendaji kushirikiana na Mhe. Waziri. Kwa sababu yeye ni mwanasiasa, haidhuru na yeye mwingi kwenye mambo hayo ya biashara kwa sababu na yeye ni mfanyabiashara huko nyuma.

Lakini sasa nije moja kwa moja kwenye mada Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu cha Mhe. Waziri na mimi nitagusa kule kulikonigusa, kwanza nataka nimuulize Mhe. Waziri, na sitounga mkono hoja kama hajanieleza maelezo mazuri ambayo yataniridhisha. Kwanza, huu mchele kupelekwa Pemba, mchele una vikwazo vikubwa sana kwenye wizara yako Mhe. Waziri mpaka watu wakapata fursa ya mchele huu kuupeleka Pemba.

Sasa mimi najiuliza Mhe. Mwenyekiti, hata Pemba nako kunatakiwa kufanyiwe ushuru? Wafanyabiashara wanakuja hapa kwa ajili ya kuchukua mchele kuupeleka Pemba, lakini mchele huo niseme wanasumbuliwa kupita kiasi, hebu twambie Mhe. Waziri hao wanaofanya mambo hayo ni nani hasa, kama binadamu sote ni binadamu mchele kutoka hapa Unguja kwenda Pemba wasumbuliwe wafanyabiashara, na mtu akitoka Pemba akija hapa anajua mimi nitakwenda kukaa siku zangu mbili jahazi nitakayopakia au chombo chochote kile nitakachopakia anafanya kwa mintarafu ya mipango yake ya fedha ya matumizi anayojipangia. Uje unieleze kinagaubaga na kama hukunieleza *Wallahi* siipitishi bajeti wala siungi mkono. Maana tunaona sasa mambo mengine mnatufanyia sokomoko.

Nije katika suala zima la Shirika la *ZSTC.* Mhe. Waziri kitabu chako cha mwaka jana tulizungumza sana suala la Shirika la *ZSTC,* lakini pamoja na hayo tulipitisha sheria kwamba hili shirika tunalitaka liwe shirika madhubuti tena zuri lenye wataalamu, liwe dogo, lakini la kushangaza kuwa mpaka leo shirika hili bado ile sheria tuliyoipitisha humu haijafanyiwa kazi, uje unieleze kwa kina. Tunapitisha mambo yetu humu kwa mintarafu kutengeneza mambo yetu tuyaweke vizuri, ni sababu zipi.

Amesema Mhe. Salmin Awadh hapa kwamba hata bodi haijaundwa, kwa nini bodi haijaundwa na hili ni shirika ambalo kwetu sisi ni muhimu Mhe. Waziri kwa nini bodi haijaundwa mpaka leo mwaka huu. Hilo uje unieleze shirika hili lina wafanyakazi wangapi, kwa sababu sasa hivi kama tunavyojua fedha, mishahara imeongezeka na kama kuna watu ambao hawana kazi maalum kwa nini tuwalipe mishahara jamani, hebu hizo pesa tutafutieni tuzipeleke kwenye meli. Mhe. Waziri wa Fedha hapa anatafuta fedha tuzinyokoe nyokoe hizo tumuongezee tusiwe na muhali Mhe. Waziri, mficha uke hazai, Mwenyezi Mungu anisamehe na Ramadhani hii mficha uke hazai.

Sasa nije katika Shirika la Magari. Mimi nagusia yale mambo ambayo yanatufyonza tu hayatupi chochote. Shirika la Magari Mhe. Waziri tulisema hili shirika lifungwe kwa nini mpaka leo halijafungwa kuna matatizo gani? Kwa sababu badala ya kuuza linachuuza shirika haliuzi, mtu hatochukua baiskeli kwa watu wengine shirika hilo akaja akakaa pale akauza baiskeli tu au vespa za mtu akachukua pale akaja akauza, si shirika hilo ni hasara, badala ya kutia fedha linatoa fedha. Kwa sababu kwanza wao hawafanyi biashara wao wenyewe na wapo hapa wananisikia, shirika hili tulisema haliwezi kujiendesha lingeonesha mfano mzuri sisi tusingeagizishia magari kwengine tungekwenda kuchukua kwenye shirika letu, lakini leo utandawazi huu magari yamejaa tele shirika limekaa pale pale linauza baiskeli na vyarahani sijui kama vipo na vespa tena hivyo si vyao, maana yake wakope huko kisha waweke pale, jamani tutakwenda kweli! Hapa nitakuwa mgumu Mhe. Waziri, lazima tuwe *serious* na mambo yetu tusifanye mambo ambayo wananchi wakatushangaa.

Nimezungumza kuhusu mambo hayo manne lakini nakuja. Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika maonesho ya mwaka juzi maana yake huu si mwaka huu, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliwasaidia wajasiriamali shilingi milioni mia mbili, lakini pesa zile uje unieleze Mhe. Waziri zimekwenda wapi zipo, na kama zipo wamepewa wenyewe? kama hawajapewa ni kwa nini hawajapewa? Tuseme wajasiriamali wetu ni wengi lakini wangetizamwa wale ambao wanatoka hapa wakenda wakijituma kule Dar es Salaam kwenye Sabasaba. Nije nipate maelezo mazito kwa sababu wajasiriamali wengi ni akina mama na wanapata usumbufu mkubwa sana wanapotoka hapa kwenda Sabasaba, ni watu ambao wanakwenda kujichumia rizki na hiyo rizki hawaili peke yao na akina baba wanaila hiyo rizki. Kwa hivyo naomba maelezo ya kina.

Lakini jengine ninataka unieleze Mhe. Waziri sisi hapa wakati kipindi kilichopita tulikuwa na matatizo ya petroli. Tukasumbuka wakatunyanyasa sana wenye kampuni hii ya petroli. Hebu nieleze kama wewe ni Waziri wa Biashara, haiwezekani na siku ile nilimwambia Waziri wa Fedha, haiwezekani sisi hawa wafanyabiashara wetu hapa wakaagizishia petroli moja kwa moja huko inakatoka Mombasa, tukawa sisi wenyewe zile fedha tukaziingiza sisi wenyewe na yale mafuta yakapungua bei.

Maana yake kutoka hapa tukenda kuchukua Dar es Salaam yakija hapa yanawia uzito na fedha ni nyingi. Nakuomba ushirikiane na wizara husika na hasa wizara husika ninajua mimi ni Wizara ya Fedha ndio yenye mamlaka, mushauriane mukubaliane wafanyabiashara wetu waagize moja kwa moja mafuta huko Mombasa, tusinyanyaswe namna hii na wafanyabiashara wa mafuta hapa, wanatunyanyasa vibaya.

Nitoe indhari Mhe. Waziri wa Biashara kuna tatizo la kwamba mafuta yakipandishwa bei kule, huku wenye vituo vya mafuta raha mustarehe. Lakini yakiteremshwa bei kule huku wanatwambia mafuta hawana na sisi tunajua kwamba mafuta yamo. Tunasema mara hii wakitufanyia hivyo tutakuja kuiomba serikali vituo vya petroli vifungiwe.

Kila ambacho kinahisi kinatunyanyasa, akisema mafuta hana wafungiwe maana tunaopata shida na sisi. Mfanyabiashara hajivutii kwakem tu, mfanyabiashara lazima atizame na yule kwa sababu yeye si bwana, mteja ndio bwana lazima abembelezwe. Hilo ninakuomba Mhe. Waziri.

Lakini nije la mwisho kidogo hili. Mhe. Waziri ninajua viwanda vikubwa kwa sasa hivi, maana yake hiyo ni long term. Lakini kwa ninavyokujua wewe kwa sababu ni mfanyabiashara na umeshatemebelea ulimwengu mzima, imani yangu ni kuwa umeshautembelea ulimwengu. Kila nchi umeshakwenda kuangalia hapa ni nini, hapa ni biashara gani. Nakuomba Mhe. Waziri hebu wasaidie wale jamaa zangu wa Kipemba kwa kuwapelekea viwanda vidogo vidogo tu vya wajasiriamali kama vya bungo na hakuna kitu kizuri na kitamu kama juice ya bungo. Unashindwa Mhe. Waziri kuwapelekea vimashine vidogo vidogo tu wakaweza kufanya juice ya bungo, embe na bidhaa mbali mbali ambazo zipo Pemba, tunaweza tuka-preserve wananchi walioko kule wakaweza kuleta tija.

Na ndio maana ukaona jamaa zangu wanakuwatwike masusu ya maembe, ikifika msimu wa maembe masusu tele hapa sisi wenyewe tunashindwa kuyala, kwa sababu kule inakuwa hayana bei kwa wingi yanavyozaliwa na bunge ni hivyo hivyo. Hebu ninakuomba katika kipindi hiki cha mwaka huu ya bajeti hii, hebu onesha mfano japo mbili, tatu waweze kufaidika wananchi wa Pemba kwa matunda ambayo yaliyokuwepo kule. Sasa hivyo viwanda vyako vikubwa utajue mwenyewe huo mpango wa kupanga.

Lakini na la mwisho kabisa Mhe. Waziri tuna imani kubwa na wewe katika wizara hii, hebu onesha imani kwa wafanyabiashara, ninajua imani unayo kwa wafanyabiashara, hebu zungumza nao wafanyabiashara, baadhi ya mambo wawapunguzie wananchi bei. Serikali inajitajiti Mhe. Waziri kila inapoona kupunguza ushuru inapunguza lakini kwa nini wao hawawi na imani na wananchi wao, wakaweza kuwapunguzia angalau bei ndogo ndogo, vile vya kupunguza bei vikapunguzika. Unajua kwamba Ramadhani hii vitu vimepanda bei maradufu.

Maana yake huu ni mwezi Mtukufu wa kupata thawabu lakini takriban wafanyabiashara wengi wanajipotezea, kwa sababu sisi wengine huwa tunakwenda mwenyewe sokoni, mimi huwa ninakwenda nikaranda mwenyewe sokoni. Badala ya kuteremsha bei wanaona wakati huu ndio wa kuchuma. Si wakati wa kuchuma hivyo wanavyofikia wao, wakati huu ni wakati wa kuchuma thawabu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Ninawaomba wafanyabiashara, hizi siku zilizobakia wawasaidie wananchi kuwapunguzia bei bidhaa mbali mbali ili waweze kukimu na wao mahitaji yao.

Baada ya kusema hayo, siungi mkono mpaka uje unifafanulie maelezo yangu niliyoyaeleza, mambo ya kunyanyasana yameshapita, tusinyanyaswe. Baada ya kusema hayo siungi mkono hoja mpaka nitakapopata jawabu madhubuti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nikukumbusheni tu kwamba michango kwa ajili ya wizara hii tutamaliza leo na kesho itakuwa ni siku ya majumuisho kwa mujibu wa wakati wetu tulionao.

Sasa tunamkaribisha Mhe. Mussa Ali Hassan na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipatia uwezo wa kuweza kusimama hapa kwa kuchangia bajeti hii. Kwa hivyo sina budi nimshukuru allah hivi sasa kusimama nikiwa mzima wa afya.

Ninaanza kuchangia ukurasa wa 18 wa bajeti hii kuhusu masoko. Mhe. Mwenyekiti, kwamba ninasikitika sana kuwa nchi yetu kwa nini ikose viwanda wakati tuna ardhi kubwa na sehemu kubwa ya kuweza kuwa na viwanda, tukaweza kuwahakikishia wananchi wetu wanajitegemea kwa utendaji kazi.

Nikisema hivyo kwa muda wa miaka mingi ya nyuma nilifahamu Zanzibar ilikuwa na viwanda vingi sana vya kuweza kujitegemea. Viwanda hivyo hivi sasa nikajua kwamba havipo nchini. Naomba Waziri anifahamishe viwanda hivi vilisababishwa na nini kuweza kuondoka nchini na ikiwa havifanyi kazi, wakati na vijana wapo wa kutosha kuweza kufanya kazi katika viwanda vile.

Katika viwanda ambavyo ninavifahamu ambavyo vilivyokuwa vikizalisha na hivi sasa vipo lakini sijui vinazalisha nini. Kwa mfano Kiwanda cha Chakula cha Kuku. Nilikuwa ninakifahamu sana kiwanda kile na wafagaji walikuwa wanafaidika sana kuhusiana na kiwanda kile. Sasa ninashangaa sana kuona kiwanda kile kinaekwa vitu vyengine hakizalishi vile vitu ambavyo vinahitajika kuwepo pale.

Hivyo hivyo ninataka kujua hiki Kiwanda cha Chakula cha Kuku kinaendelea vipi, ni kiwanda cha serikali au kiwanda cha mtu binafsi. Kwa sababu hivi karibuni nilisikia tangazo kuwa kiwanda hiki kinanadiwa ili kiuzwe. Hivyo naomba kwa Mhe. Waziri anihakikishie kiwanda hiki kipo chini ya serikali ama kipo kiwanda cha mtu binafsi.

Vile vile Mhe. Waziri anieleze kuhusu mambo ya kilimo tunaenda katika sehemu gani. Kwa hivi sasa kuna biashara nyingi ambazo zinalimwa lakini hazitangazwi kama tunavyofaidika katika zao la karafuu. Wakulima wote wa Zanzibar hii wanakata miembe, minazi kwa ajili ya kupanda mikarafuu, sababu kubwa karafuu imepanda bei na unajua mkulima anapopanda mkarafuu

anavuna vipi na anauza vipi. Kwa hivyo kila mtu amepanga bajeti ya kwamba ahakikishe anapanda mikarafuu.

Kwa nini Mhe. Waziri usinieleze kwamba hizi species nyengine nazo unazitangaza bei zake hasa zile zinakaushwa kama vile karafuu. Nikitazama bidhaa za biashara za nchi za nje ambazo tunapata pesa za kigeni zipo nyingi hapa, kama tangawizi ambayo inahitajika sana huko nchi za nje. Tangawizi peke yake duniani iliyokuwa nzuri ni tangawizi ya hapa Zanzibar. Sasa ninashangaa kwa nini mpaka leo hujaweza kuitangaza tangawizi kwamba ni zao la kitaifa hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Mhe. Waziri hajaweza kunihakikishia bei ya pilipili hoho ikiwa imetangazwa kuwa ni zao la kitaifa hapa nchini wakati nchi za nje, hakuna nchi yoyote duniani inayozalisha pilipili hoho safi na nzuri kama hapa Zanzibar. Kwa vipi mpaka leo ukawa hajaweza kutangaza kuwa ni zao la kitaifa, tukahakikisha wananchi wetu wanapata biashara na faida kwa kila mmoja anaekeza kwenye zao la pilipili hoho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini mpaka leo Mhe. Waziri hujalitangaza zao la manjano ambalo Mkoa wa Kaskazini Unguja ni zao kubwa sana na linapata pesa za kigeni. Katika nchi za duniani zijasikia nchi ambayo inayozalisha manjano nzuri kama ya Zanzibar inatafutwa sana na mpaka leo hujaweza kulitangaza zao hili likawa ni zao la kitaifa.

Kwa kweli Mhe. Waziri ukija hapa unieleze sababu zipi mpaka leo ambazo hujaweza kutangaza mazao mengine, zaidi ya zao la karafuu tu ndilo ambalo umelipa kipa umbele au wewe mwenyewe zao hili umepanda huko nyumbani Pemba. Naomba Mhe. Mwenyekiti, zao la karafuu usilipe kipa umbele peke yake na vitu vyote uvipe umbele.

Kama mimi ninavyoomba ulipe umbele zao la mbaazi haina haja ya kuagiza kwa sababu katika jimbo langu ni zao pekee linalozalishwa kwa wingi hasa kwenye mwezi huu Ramadhani. Mimi nimekwenda katika maduka mengi kutafuta futari ya mbaazi unakuta mbaazi haziwivi. Lakini nenda Kikungwi ukahakikishe mbaazi zake ni original katika Zanzibar hii zinapatikana kwenye Jimbo langu la Mkoani. Kwa nini huwezi ukilipa kipa umbele Mhe. Waziri likawa zao hili linazalishwa katika jimbo langu na tukawa hatuagizii nchi za nje.

Mhe. Waziri ninataka uniambie kwamba hivi sasa mazao yote yanayopatikana Zanzibar tusiwe na haja ya kuagiza nchi za nje hasa kwa vile zao la chooko linaostawi sana katika Mkoa wangu wa Kusini Unguja, ni zao peke yake linalozalishwa kwa wingi kwenye sehemu za mawe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba unihakikishie katika dunia hii ni nchi gani inayozalisha mabungo kama si Zanzibar peke yake na ambazo linaingiza pesa za kigeni kwa wingi. Kwa nini zao hili tusilisafirishe nchi za nje tukapata pesa za kigeni, wakati watu wa nchi za nje wakija hapa Zanzibar, watalii wanakunywa sana juice ya bungo. Kwa nini zao hili tusilifanye ni zao la kitaifa tukahakikisha bungo hivi sasa linathamani sana na wananchi wetu wakaweza kupata pesa za kigeni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nchi ya Zanzibar sio nchi maskini na nchi tajiri kwa mazao yake yote. Vijana wetu haina haja ya kutafuta ajira serikalini kama Waziri atatangaza mazao haya kwa

kinagaunaga kwa kuwahakikishia bei zake. Ninahakikisha wananchi wote watarudi vijijini kuanza kulima na kuwa wajasiriamali wazuri. Ninahakikisha wananchi wa Kusini Makunduchi sote tunarudi kijiji kwenda kulima, vile vile wananchi wa Pemba wote watarudi Pemba kwenda kuhakikisha mabungo yanapatikana.

Hivyo wewe mwenyewe Mhe. Waziri ninahakikisha ndio unaosababisha mji huu kuwa na vurugu la vijana kwamba hawana kazi. Kama utatangaza mazao haya wananchi na vijana wote watarudi sehemu yao na kuacha vurugu pale mjini. Vurugu linasababishwa na vijana kwamba hawana kazi za kufanya, ndio utakuta wengi wanaamua kupewa shilingi tano ili wafanye vurugu mjini, wananchi wasikae vizuri, wafanyabiashara wasifanye biashara zao vizuri na wengi ni wala unga. *(Makofi).*

Hivyo wewe Mhe. Waziri naona ndio sababu kubwa kwamba hujaweza kutangaza biashara zetu ziwe za kitaifa na wananchi wetu waukoke na umaskini. Naomba Mhe. Waziri utakapofika hapa unihakikishie kwamba umeweza kutangaza bei hizi kinagaubaga ama ninaweka shilingi bajeti yako haitopita mpaka nihakikishe mazao haya umeyatangaza. *(Makofi).*

Kwa haya yote Mhe. Mwenyekiti, kwa leo nitaunga hoja hii asilimia zote mimi na wananchi wangu kama Waziri atanihakikishia kupanga bei ya mazao haya hadharani. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa kwa kuunga mkono kwa asilimia zote.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nizungumze machache kabisa katika kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza ninataka nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi kubwa na ngumu waliyopewa na taifa letu katika kuhakikisha kwamba wanaimarisha biashara katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme suala la biashara sio suala dogo; suala la biashara lina nyanja nyingi. Kimsingi kwa mazingira ya nchi yetu, yaani Zanzibar kwamba ni visiwa, ardhi yetu tuliyokuwa nayo ni ndogo. Kwa hivyo tunahitaji lazima tuwe na miundombinu ya kutosha ya kuimarisha biashara ili wananchi wetu waweze kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nianze kwanza katika suala zima la zao la karafuu. Kwanza tunaendelea kuipongeza serikali yetu, tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kuinua au kutangaza bei ya karafuu na mpaka hivi sasa wananchi wetu wanaendelea kufaidika. Lakini bado tunaomba Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mhe. Waziri, wizara iwe na mikakati ya kutosha.

Kwa kweli wananchi wetu wamepata moyo mkubwa sana baada ya bei ya karafuu kuongezeka. Lakini kitu ambacho kinachosikitisha hivi sasa tumeweza kupata taarifa kwamba karafuu watu zinabakia majumbani mwao. Sasa mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka nimuulize Mhe. Waziri suala dogo tu.

Mimi nimejaribu kuangalia sana vipindi vya maonesho ya sabasaba lakini vile vile nimeangalia na maonesho ya nanenane yale yaliyofanyika kule upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimejaribu kufuatilia sana taarifa za BOT wanazozitoa na wao hata jana nilikuwa nikiangalia usiku ninafikiri ilikuwa ikioneshwa katika TBC pamoja na ZBC, walielezea ni namna gani BOT wanavyotoa mitaji kwa mabenki kuyawezesha katika ili kuweza kuwahudumia wananchi.

Kama nilivyosema mwanzo, wenzetu hivi sasa wanawezesha zile taasisi ambazo zinazowea kutoa mikopo. Mfano kama jana walisema kwamba wanatoa mikopo kwa benki yoyote ambayo inayokusudia kutoa mikopo kwa wananchi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Sasa sijui kwa hapa kwetu katika zao la karafuu, pengine labda sisi tumekwama kwa upande wa serikali.

Lakini kwa kuwa BOT wao ndio regulator wa uchumi wetu lakini vile vile pale ambapo panapotokezea mtikisiko, wanajaribu kusaidia. Mtikisiko si lazima utokezee duniani, mtikisiko hata ukiwepo ndani kwamba kuna biashara unaitaka na fedha huna na biashara ile inauzika. Mimi ninafikiri hapa ndio maeneo ambayo ya kuweza kutusaidia.

Sasa sijui Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, umejaribu kuwa-approach vipi hawa wenzetu wa BOT ili kuona kama serikali imekwama kuwa na mtaji wa kuweza kununulia karafuu, basi angalau kuweza kutusaidia kutukopesha. Kwa sababu hili linalizungumza hata katika bajeti ya mwaka jana nilipozungumza Wizara ya Fedha, nilizungumzia kwamba BOT ilipotokezea mtikisiko wa uchumi duniani, basi waliweza kuyasaidia fedha bure kabisa mashirika na makampuni mbali mbali kwa upande wa Tanzania Bara.

Sasa hili vile vile nilikuwa naomba kwa Mhe. Waziri kama tumekwama kifedha ndio maana karafuu zimekwama, basi tuangalie taasisi za fedha ambazo zipo kwa mujibu wa Katiba na sheria ili ziweze kutusadia kukwamua wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapa hapa kwenye zao la karafuu. Kwanza tunashukuru kwa sheria ilivyofanyiwa marekebisho lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba unajua wananchi wetu inafika pahala wanakuwa hawajui wapi pa kwenda. Kuna mwananchi wetu mmoja tena kwa bahati yupo katika kijiji changu kule nilikozaliwa mimi kule Chaani. Yeye alipata ajali kwa bahati mbaya katika mkarafuu. Huyu alianguka tangu mwaka 2002. Kwa kweli amehangaika kila taasisi lakini amegonga ukuta. Hivi sasa yupo kitandani, hawezi kutembea, kila kitu afanye hapo hapo, asaidiwe hapo hapo.

Sasa ninaishukuru Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Kitengo chake cha Habari waliwahi kumfuatilia na wakarusha vipindi vyake hewani katika ZBC televisheni karibu mara mbili. Sasa mimi nimefarijika kwamba kuona kumeanzisha mfuko wa zao la karafuu.

Sasa basi huu mfuko mimi naomba uangalie uwezekano wa kuwasaidia hata na wale waliosaidia kuokoa hili zao la karafuu. Zamani mimi ninakumbuka tulikuwa tunafungiwa skuli tunakwenda kuokoa zao la karafuu. Sasa kuokoa zao la karafuu ina maana kuitikia wito wa taifa. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Waziri alau aje anisaidie ufafanuzi ajaribu kuwasilisiana na watendaji wake ili kuwasiliana na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kumuona yule afisa wa habari ili

kujua lile tatizo likoje na wao kama Wizara ya Biashara wanaweza wakamsaidia vipi mwananchi huyu.

Kwa sababu mukiweza kutoa kauli ya kuweza kumsaidia huyu, basi na ninaamini na wengine watavutiwa kuchuma hili zao la karafuu, sio kama watajiangusha kwa makusudi ili kuweza kupata msaada, lakini wanaamini kuwa pale itakapotokezea dharura yoyote basi serikali kupitia Wizara wataweza kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea ninakuja katika suala zima la wenzetu hawa waliokuwepo katika maeneo huru ya kiuchumi. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua sera ya maeneo huru ya kiuchumi wale wenzetu wanaruhusika kuingiza bidhaa nchini ambazo kwamba wanapata msamaha fulani wa kodi. Halafu wanaruhusiwa kuuza bidhaa zile ninafikiri asilimia 80 nje ya nchi na asilimia 20 wauze ndani ya soko.

Sasa nimepata malalamiko wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura ambao wapo katika soko la Saateni. Wao wanalalamika wanasema kwamba huyu muuzaji wa mitumba ambaye anaitwa Kampuni ya Savana; ninafikiri wapo Amani pale. Hawa kwa kweli wanakuwa kama na wao sio wafanyabiashara wakubwa ambao waliokuwepo katika maeneo huru.

Kwa sababu kama katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani, yaani ndani ya mwezi mmoja unaweza ukakuta bei ya bidhaa ile ile inaongezeka karibu mara matatu. Sasa hapa inaonekana kwamba hawa nao ni wachuuzi na sio wafanyabiashara ambao wapo katika maeneo huru.

Sasa nilikuwa naomba Mhe. Waziri hili suala hebu jaribu watume watendaji wako wafuatilie kwa karibu, wazungumze na wale wafanyabiashara wa mitumba, halafu wakae wazungumze na yule mwekezaji ili ajue kwamba yeye ameekwa pale kwa mujibu wa sheria za nchi na hizo nafuu zilizomfanya yeye aje awekeze pale kwa ajili ya kuwasaidia hawa wananchi wetu, asitufanyie udalali tena akajifanya kama na yeye yupo jua kali. Kwa hivyo hili nilikuwa nakuomba Mhe. Waziri hebu jaribu kulifuatilia ninajua watendaji wako wapo makini makini wananisikia wataweza kukusaidia ili kupata taarifa iliyokuwa sahihi zaidi.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri sasa hivi vijana wetu tunawasumbua sana hawajui leo wanaamka vipi na kesho wanaamka vipi katika masuala yao ya biashara. Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo moja kubwa hasa katika wafanyabiashara wa maeneo ya Saateni na Darajani.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu waliondolewa Darajani wakapelekwa soko la Saateni. Soko la Saateni limeboreshwa. Kuna wafanyabiashara pale wakajitolea katika utaratibu ninadhani wa BOT walivyokubaliana pengine na Baraza la Manispaa. Wamejenga pale maduka wame-invest pesa yao pale na hatujui ile pesa waliyo-invest pale kama aidha wamekopa kupitia benki au walitoa katika mifuko yao, kwa kutegemea kwamba ile biashara ndogo ndogo zitakuwepo katika soko la Saateni.

Matokezeo yake kwa kuwa tumeshindwa kuwadhibiti wale vijana; vijana wamerudi tena Darajani. Kwa hivyo matokeo yake ile milango sasa hivi kule Saateni imefungwa. Sasa wale wafanyabiashara wale wa Jua Kali ambao wapo Saateni sasa hivi wanalalamika. Wanatuuliza

Waheshimiwa hii serikali yetu ipo makini kiasi gani. Tulikuwepo Darajani mukatuhamisha, mumetuleta Saateni hapa tumeanza biashara na ilikuwa imeimarika vizuri. Serikali pale ilikuwa iimarishe nguvu zake.

Mimi ninakuomba sana Mhe. Waziri msaidie Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ili wananchi wetu waweze kujua hasa wanatakiwa wakae wapi na pale watakapokaa kweli vile facilities zitakuwepo na ile biashara yao itaweza kulindwa. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wanatwambia, mimi juzi nilikwenda pale wamelalamikia sana, wanasema mheshimiwa kama mutashindwa kudhibiti na sisi sote tutaondoka huku Saateni tutarudi tena Darajani.

Sasa wale waliokuwepo leo hapo Darajani pa kupita huna. Jee na wale wa Saateni wakirudi tena Darajani itakuwa vipi. Sasa mimi nilikuwa naomba serikali lazima tuwe na mikakati maalum ili wafanyabiashara wetu na vijana wetu, maana yake wakati mwengine tunalaumu wamerudi tena Darajani lakini wamerudi kwa sababu gani. Kuna sababu iliyowarudisha Darajani.

Sasa mimi ninadhani serikali yetu wakae na kwa kuwa hili tukimuachia Mkurugenzi wa Manispaa peke yake haliwezi. Mimi ninafikiri Waziri wa Biashara wewe ndio unaowasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na tunamshukuru Mhe. Mohamedraza ingawa kaondoka kenda jimboni hivi sasa. Kwa hivyo mimi ninadhani na zile shilingi milioni mia mbili mheshimiwa wala usiziache zifuate bwana, wafanyabiashara wanazitaka. Hata na mimi nina wafanyabiashara wangu wengine wanauza dagaa, kuni, tutapiga hodi kuja kuzifuata, eeh! bwana sadaka inaanza nyumbani na mimi na Mhe. Mohamedraza jirani na wewe ni jirani yangu pale, mimi ninaamini wananchi wetu wanaweza kufaidika.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninakuja mbele zaidi katika maeneo ya maenesho. Kwanza nimeshukuru kuona kwamba wizara yako imo katika jitihada ya kufungua maonesho. Mhe. Mwenyekiti, nchi kama Zanzibar ni nchi ambayo tokea asili ni kitovu cha biashara ni aibu kubwa mpaka leo kwamba hatuna maonesho ya kibiashara hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nyinyi munachukua pesa nyingi tunaziidhinisha, munakwenda nje katika masoko ya biashara, kwenda kuangalia kutangaza Zanzibar kwenye masoko ya utalii. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, tukianzisha hapa masoko yetu na wao wenzetu watakuja, na vile vile mutarusha katika website kuna maonesho ya biashara Zanzibar watakuja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa ninaona taabu sana kwamba maonesho ya sabasaba sisi tunakuwa katika bajeti. Mimi kuna kipindi niliwahi kutoroka nikenda Jumamosi na Jumapili lakini siku hizi Jumamosi na Jumapili, tulikuwa tumebanwa sana na vikao vya semina mbali mbali. Lakini kule Mhe. Mwenyekiti, unapata mtu kujifunza mambo mengi. Unajiuliza duu kumbe Tanzania tumefikia stage hii, kumbe biashara hii imefikia stage hii.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nina uwezo wa kwenda na kurudi lakini wafanyabiashara wengi wa Zanzibar hawana uwezo wa kwenda Dar es Saalam kwenda kwenye maonesho. Mimi ninaamini Mhe. Mwenyekiti, kama utaanzisha maonesho, tuanzishe kama alivyoanzisha ninafikiri wakati ule Dk. Salmin, hakusubiri mpaka akawa na miundombinu mikubwa sana nini, atleast tuanze. Wakija wafanyabiashara kutoka Bara na sehemu nyengine wakija kuonesha

bidhaa zao, ninaamini wananchi wetu wataweza kupata contact nzuri, wataweza kuwasilisiana vizuri.

Lakini vile vile na wale wafanyabiashara wa Zanzibar ambao mpaka sasa hivi tunashukuru wizara yako inaendelea kuwaenga enga, unawapeleka 50 basi na maonesho yakifanyika Zanzibar watakuja 200. Sasa leo 50 wanakwenda kule wanalalamika sijui tunakunywa uji, lakini maonesho yakiwepo na kwao, mimi nafikiri biashara itaweza kuimarika zaidi. Kwa hivyo, hili nilikuwa nakuomba sana Mhe. Waziri nimeona jitihada zako, naomba uendelee na moyo huo huo.

Lakini Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hayupo, mimi nadhani akupe nguvu. Mwenzangu Mhe. Salmini Awadh kazungumza vizuri sana. Wewe tumekupa mtihani, hii wizara yako inahitaji maeneo mengi yaimarike ili biashara iweze kuimarika. Huna bajeti ya kuimarisha biashara Zanzibar, lakini bajeti yako inakwenda kwa upande wa kilimo, tukiimarisha umwagiliaji maji, upande wa viwanja vya ndege tukiimarisha. Hapa nimeona katika kitabu chako, umeeleza mnataka kuboresha yale masuala ya kutaka kusafirisha maua, mboga mbona na vitu vingine. Lakini uwanja wa ndege wetu je, tunazo *coderoom* pale hatuna.

Sasa mimi nadhani hata katika mikakati ya huyo Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano aangalie wanapotanua huu uwanja wetu wa ndege, basi wajaribu kuweka na zile *coderoom*, kwa sababu maua yanalimwa shamba, yanatakiwa yakishatoka kule mpaka yakishafika mjini yawe katika hali yake ile ya kawaida. Lakini vile vile yakishafika hapa kama kuna *delay* ya ndege basi maua yanaweza yakanyauka. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Waziri haya ni katika maeneo ambayo yataweza kuwasaidia na hawa wakulima wetu wanaolima mboga mboga ambazo zitahitaji kusafirishwa kwenda nje hapo baadae. Lakini vile vile watakaotaka kusafirisha na maua.

Lakini pia nilikuwa nataka kukukumbusha Mhe. Waziri ahadi ya Mhe. Jakaya Kikwete. Mwenzangu alizungumza kwamba Dk. Jakaya Kikwete alikwishakutoa pesa. Lakini mimi ninavyojua alitoa ahadi. Sasa sijui ahadi ile imeshatekelezwa ya milioni 200, kwa sababu kwa kweli wafanyabiashara wetu bado wanaendelea kutuuliza kila siku. Unajua siku hizi wananchi wakisikia wizara fulani basi vibarua tayari, vipi pesa zetu. Sasa na hili ndio na wewe nilikuwa nakukumbusha tu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, katika kuimarisha biashara Zanzibar ni lazima tuimarishe bandari zetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba serikali, kwa kutegemea kwamba serikali yetu ifanye kila kitu *never. Never ever* hatuwezi, nchi za wenzetu tunashuhudia, serikali zao wanaandaa sera, wanaandaa taratibu, milango inakuwa wazi, wanaweka vivutio, ili wafanyabiashara waweze kuvutiwa.

Mhe. Mwenyekiti, bandari ya mpigaduri. Kama hatujaandaa utaratibu wa BOT, basi mimi naona tutachelewa sana. Serikali imeshakubali PPP, kwa nini mpaka leo tuko kimya. Kweli Mhe. Waziri mpaka leo huna maarifa ya kuweza kuwatafuta watu wa kuweza kujenga bandari, kwa kushirikiana na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Waziri wa Fedha, Uchumi na MIpango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, leo serikali yetu baada ya sisi kupiga kelele sana, serikali ilikuwa inasema haina uwezo wa kununua meli, Lakini baada ya kuona kwamba tumechachamaa, mmetoa tamko na sasa hivi mnatafuta meli. Sasa au unataka tuzuwie bajeti sasa hivi mpaka mtuambie kuwa mtamtafute PPP kutoka wapi, ili aje kujenga bandari. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hatutaki kila wizara tuisokote.

Tunatoa ushauri, lakini ushauri wetu huu tunaomba mawaziri watatu. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kushirikiana na jemedari mkuu Mhe. Rais wa Zanzibar, mimi naamini hebu tuandaeni utaratibu tuangalie ndani ya mwaka ujao hamuwezi kuja kutuambia kwamba tumeshapata mwekezaji yuko tayari kujenga a-*operate* halafu baadae akisharejesha gharama zake aweze ku-*transfer* ili tuweze kufaidika. Naamini kwa vichwa hivyo vilivyovitaja viko makini, tutaweza kufanikiwa katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo huru bado tunaendelea kuzungumza kwa mdomo hatujaimarisha, hebu tupelekeni barabara, hebu tupelekeni umeme na hebu tupelekeni maji kweli wawekezaji watashindwa kuja. Mhe. Mwenyekiti, mimi natoa mfano mmoja. Kuna mwekezaji mmoja hawa ndugu zetu wa Aghakhan ambao waliwahi kupewa eneo pale Bubwini katika maeneo ya Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji wale walikuwa wanataka kuekeza uwekezaji mkubwa, walikuwa wanataka kuwekeza katika ule uwanja wa gofu, lakini matokeo yake tulikubaliana kwamba serikali itapeleka barabara, umeme pamoja na miundombinu mingine, vitu hivyo vyote vilichelewa. Matokeo yake na yeye akaendelea kuchelewa, lakini baya zaidi tulimwambia mpaka Kambi ya Jeshi aondowe yeye.

Mhe. Mwenyekiti, walikwenda wakapigwa kichura kule walishika adabu yao. Sasa leo unapomwambia muwekezaji, halafu kuna mambo mengine ya kufanya serikali, akafanye yeye, matokeo yake lile eneo sasa hivi tunaambiwa pengine sijui kanyang'anywa au limepunguzwa. Tena akaambiwa kwamba hana uwezo wa kuekeza, kumbe kuna mambo ambayo ilikuwa ifanye serikali, tulimwachia afanye yeye. Sasa na haya maeneo mengine maeneo huru ya kiuchumi, mimi nadhani serikali iweze kusaidia.

Vile vile nakuja kwenye suala jengine la *small industry*. Mhe. Mwenyekiti wenzetu China kule, tulipokwenda sisi katika msafara wa mwanzo sisi ndio tuliofungua dimba. Wenzetu walituambia baada ya kila walivyokuwa wakifanya jitihada ya kulima wakaona wanashindwa kuiokoa jamii yao kuiondoa katika umaskini, kwa hivyo waliamua China kuigawa mapande, wakaigawa mafungu mafungu, wanaangalia katika eneo lenye umaskini mkubwa.

Kwa mfano hapa Zanzibar kama Micheweni au maeneo mengine, halafu lile eneo wanalitangaza kama *special economic zone*, yaani eneo lile wanaweka unafuu katika ushuru, unafuu katika kodi zote yaani kwenye umeme, maji na kila kitu. Matokeo yake wawekezaji wakaanza kuvutiwa wakaanza ku-*invest* pale na matokeo yake ajiri imetokezea. China sisi tulipokwenda walituambia wao hawakufungua nchi nzima, lakini wamefungua katika maeneo ambayo yaliyokumbwa na umaskini zaidi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Zanzibar mimi naweza nikasema kwamba tuna uwezo wa kuifungua Zanzibar yote ikawa *special economic zone*. Lakini vile vile Mhe. Spika, kuna vitu

ambavyo bado vinatukwaza, sera zetu za kiuchumi. Wenzetu China walituambia kwamba sera zetu za kiuchumi kama hamjazirekebisha na sera za Muungano katika uchumi, basi mtazungumza tu. Sasa mimi nilishangaa yuko China anatuambia vile, sisi wenyewe tuko hapa mpaka leo hatujajua kama kuna vitu gani tunatakiwa tuvirekebishe ili hizi sera zetu ziweze kutekelezeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nzuri kwa *nature*. Ulaya Mhe. Mwenyekiti, mimi nimetembelea baadhi ya nchi za Ulaya, Ulaya sio nzuri lakini inatengenezwa na inakuwa nzuri. Mfano mdogo tu tuangalie kwenye mahoteli yetu, ukiangalia Kampisk, Lagema pale na nyenginezo. Kwa hivyo, mimi nafikiri hebu tuangalieni, umizeni vichwa, wazee mliopewa dhamana ya uchumi katika nchi hii tunawaamini, hebu tusaidieni kidogo angalau kutuondoa hapa tulipo tuweze kusogea mbele kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kilimo cha *irrigation* nafikiri nimelizungumza sitaki nirejee, kwa sababu hili ni suala mtambuka. Vile vile katika suala zima la usafirishaji wa anga. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka kuna wakati Dk. Salmini wakati wa awamu ya tano, aliwahi kuzungumza na wenzetu wa Mauritius, hebu kafungueni tena yale mazungumzo. Mauritius nakumbuka hapa walitaka kuweka hapa *destination* yao katika suala zima la ndege zao zinapotoka London na kwengineko, ni lazima zituwe hapa na zinapotoka Mauritius zituwe hapa na Mauritius walitaka kuwekeza hapa Zanzibar na walitaka kuwekeza hapa mpaka hii *insurance company* yao waweke hapa, ili kwa sababu kutokana na *geographer* ya Mauritius wao walisema eneo lao ni dogo. Lakini Zanzibar vile vile pamoja na kuwa eneo lao ni dogo lakini ki-*geographer* wangeweza ku-*invest* wakaweka viwanda, ili wakauza katika soko la Afrika ya Mashariki na Kati, lakini na Afrika nzima na dunia.

Kwa hivyo, katika haya masuala ya kuvutia mashirika haya ya ndege kuja kutua hapa Zanzibar, hebu Mhe. Waziri mngejaribu kufanya safari na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, hizi safari tunazozihoji mafungu haya. Sasa mimi nawaambieni nendeni. Mimi kwa nyinyi nakuruhusuni nendeni, kwa sababu nyinyi mmekabidhiwa kutafuta uchumi wa nchi, nendeni katutafutieni hawa wafanyabiashara wakumbuke ili waje kutua Zanzibar. Kwa sababu hizi *transit* zitaweza kusaidia uwanja wetu. Mhe. Mwenyekiti, kama sasa hivi tunaboresha uwanja. Utaboresha uwanja lakini huna ndege za kutosha za kutua. Kwa hivyo, kwa kuwa tunaboresha uwanja basi tuboreshe na huduma za utoaji wa hizi ndege vile vile. Kwa hivyo, mimi nadhani mnaweza mkatusaidia sana.

Lakini vile vile..

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika suala zima la *export* ya biashara zetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwamba serikali imeanza kugutuka, kwamba kumbe tunaposafirisha bidhaa zetu, mfano kama karafuu ndani ya magunia na nyengine bila ya kuziboresha, kuzi-*add value*, kumbe tunawafaidisha madalali halafu serikali inakula hasara. Mimi hili nakupongezeni sana, kwa kweli kitengo chako cha Mipango na Utafiti kwa hapa nawapa *big up*, wamefanyakazi.

Kwa hivyo, isiwe waishie katika utafiti tu, watowe mwelekeo tunakwenda wapi ili kuzi- *add value* bidhaa zetu ili tusitowe faida kwa madalali zaidi kuliko kupata faida serikali yetu.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, uwekezaji bila ya umeme rahisi bado ni mtihani kwetu, bado tunaendelea kutegemea umeme kutoka kwa wenzetu upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano, sio mbaya kwa sababu wao ndio wanao. Lakini naamini serikali yetu kwa kuwa kuna kila dalili ya kwamba Zanzibar sio muda mrefu tutaruhusiwa kuanza kutumia au kuchimba mafuta pamoja na gesi, basi naamini umeme tutaweza kuupata kwa bei nafuu. Lakini kabla ya kufika huko, kwa sababu mambo haya tunategemea baada ya marekebisho ya katiba mwaka 2014, hili eneo naamini litakuwa huru kabisa na tutaweza kulitumia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi kuna wawekezaji wanataka kuweka umeme wa taka, umeme huu ambao utaweza kuwapunguzia mzigo wananchi katika kulipa umeme kwa bei kubwa. Vile vile italipunguzia mzigo Shirika la Umeme, kuna umeme huu wa takataka na wengine wameshafika Baraza la Manispaa. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri manispaa wale kazi yao kubwa ni usafi na mambo mengine, lakini mambo ya biashara zaidi yanawahusu nyinyi. Maafisa wako naomba wakutane na Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na Maafisa wa Manispaa, ili wajaribu kuangalia, hawa wawekezaji wanaotaka kuekeza katika sekta ya umeme, basi waweze kukaa na kuangalia ni namna gani kama kweli hizi takataka zitaweza kuzalisha umeme ili wananchi wetu na wao waweze kufaidika tuweze kupata umeme wa bei nafuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa mwisho nataka nizungumze suala la bidhaa feki, yaani bidhaa ambazo zimeshuka kiwango. Naipongeza sana bodi ya chakula, hivi sasa inafanyakazi nzuri, haina muhali na mtu, mtu anapoleta chakula kibovu anamuambia aidha akiondowe au akile mwenyewe.

Mimi nadhani Mhe. Waziri mwendo huu tunakwenda vizuri, lakini bado kuna eneo moja Mhe. Waziri hamjalifanyia kazi. Katika eneo la bidhaa, sitaki kusema zinatoka nchi gani, kwa sababu itakuwa kama ni fitna. Lakini kuna bidhaa mtu anajua hasa na anauliza hii inatoka wapi, kwa sababu anajua ile *quality* yake mara nyingi inakuja *quality* ya chini. Kwa hivyo, wananchi wetu maskini. Mwananchi maskini kanunua bidhaa dhaifu, tunamzidishia umaskini kwa sababu baada ya muda mchache bidhaa ile itakuwa imekufa inabidi akanunuwe nyengine, kwa hivyo umaskini unaongezeka.

Kwa hivyo, nilikuwa nawaomba vijana wako wa kitengo hiki cha kumlinda mlaji, baada ya kuangalia sasa hivi basi wafanyabiashara wameanza kuogopa, bidhaa mbovu wameanza kupunguza kuleta, lakini bado wafanyabiashara hasa wanaoleta vitu vya *hardware* na vitu vyengine bado zinaletwa bidhaa ambazo ziko chini ya kiwango, ambazo kwa mwananchi wa kawaida anaona ananunua rahisi, kumbe vile rahisi inashinda mpishi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwenzangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub na mimi nilikuwa nataka nikazie katika suala la ukaguzi wa vituo vya mafuta, lakini na mafuta. Mhe. Mwenyekiti, gari zetu zimeshaharibiwa sana katika kipindi kama hiki na bahati mbaya *engine* ikishaharibika mtu hana pa kwenda, inabidi sasa leo kwanza mtu gari yenyewe kakopa, anakatwa kwenye mshahara *engine* baada ya siku mbili tatu. ime- *collapse* kwa mafuta machafu, hana pa

kwenda. Tunaomba Mhe. Mwenyekiti, watu wako sasa hivi waingie zaidi katika ukaguzi wa vituo vya mafuta ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawapati hasara kiasi hicho.

La mwisho kabisa nataka niligusie kidogo, nitakuja kulimalizia siku ya bajeti ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana wananchi wetu wa Zanzibar, watusikilize sana tunavyozungumza. Tunavyozungumza matatizo ya Muungano sio kwamba hatuutaki Muungano. Muungano tunautaka, lakini kuna baadhi ya watu walikabidhiwa taasisi za kusimamia mambo ya Muungano, Mhe. Mwenyekiti, wanatufanyia kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, *TRA* ya Dar es Salaam, na mimi nawaomba sana wananchi wetu watakapochangia suala la katiba mpya waitie meno Baraza la Wawakilishi liweze kujadili mpaka na mambo ya Muungano ili tuweze kusimamia taasisi za Muungano. Kwa sababu hivi sasa kuna magari karibu 600 yako bandarini Dar es Salaam, ma-*document* yako. Mhe. Waziri kasema kuna watu ambao wameshalipa ushuru Zanzibar, wameshalipa ushuru mwengine Bara, lakini bado mtu anatakiwa alipe, kitu ambacho hakiingii akilini.

Mhe. Mwenyekiti, tumepata taarifa kwamba kuna baadhi ya watendaji wa TRA na wao wana *yard* zao za kuuzia magari, ndio maana wanawasumbua wafanyabiashara wa Zanzibar wasiingie katika soko la Dar es Salaam, ili wao waweze kuuza biashara zao. hawa wanahitaji kudhibitiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa kama alivyosema Mhe. Mohamedraza kwamba hii wizara yako ni kiuno cha uchumi wa taifa. Maana zamani tulikuwa tunasema uti wa mgongo, sasa uti wa mgongo uko juu, sasa kumbe ni kiuno. Sasa kama ni kiuno, kama kiuno hakifanyi kazi utakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi nakubaliana na ule usemi wa Mhe. Mohamedraza ingawa mliona kakosea, lakini kweli wizara yako ni kiuno cha uchumi wa nchi yetu, tunaomba sasa kiuno kiwe kizima ili uchumi wetu uendelee. Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa leo sijapiga ramsha yoyote, hii bajeti mimi naiunga mkono, ingawa nitakuja kupiga buti ndogo ndogo kwa maelezo, buti zangu zitakuwa sawa na kumpiga chura teke unamsaidia mwendo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na utendaji wake mzuri pamoja na watendaji wakuu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Halikadhalika, nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendesha vizuri Baraza hili tukufu kwa umahiri wako ulionao. Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mawazo yangu machache, lakini nianzie kwenye suala zima la uhamasishaji wa bidhaa za chakula na umuhimu kama vile sukari, mchele pamoja na unga ambapo Mhe. Salmin Awadh aliligusia kidogo. Kwenye sheria hii nambari 5 ya mwaka 1986 inayozungumzia masuala mazima ya vyakula muhimu ambavyo nimevitaja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili hususan katika hawa waliofanya biashara ambao huwa wanafanyabiashara kupeleka biashara zao katika maeneo ya Dar es Salaam na nje ya Zanzibar, ambapo kumekuwa na tatizo linalozungumzwa na wafanyabiashara wengi ambao

wanafanyabiashara hii ya mchele pamoja na sukari, hususan sukari na mchele. Kwa kweli ni tatizo hili kwa sababu inaikosesha Zanzibar mapato mengi.

Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake hapa Mhe. Waziri amesema kwamba *packet* 1,722 za mchele pamoja na *packet* 1,208 za sukari ambazo husafirishwa na wizara yake kuweza kuwashika wale ambao wanasafirisha biashara hizi kinyume cha sheria cha nambari 5 ya mwaka 1986. Mhe. Waziri kaeleza hapa, lakini ningemuomba wakati atakapokuja atueleze kuwa ni nani na nani ambao wamehusika na sakata hili zima la kusafirisha bidhaa hii ya mchele pamoja na sukari kinyume na kanuni ya sheria hii. Vile vile atueleze na majina yao ili tuwatambuwe, kwa sababu hawa hawaitendei mema Zanzibar. Wanajivutia upande wao kwa faida yao wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni wangapi na ni akina nani.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika sekta ya viwanda. Sekta ya viwanda ni sekta muhimu na ni sekta ambayo inawapatia vijana wetu ajira. Katika miaka ya 1980 viwanda vingi vilianzishwa hapa Zanzibar, viwanda vidogo vidogo vingi vilianzishwa na vijana wetu waliweza kupata ajira. Lakini katika miaka hii takriban 25 mpaka 30 viwanda vile vimepotea, viwanda vimekufa hakuna mwelekeo wowote. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wizara yake katika kuhakikisha kwamba tunaanzisha viwanda vyengine au kuviboresha vile viwanda vilivyokufa, ana mikakati gani na mipango gani ili kuhakikisha kwamba viwanda vile vilivyokufa vinafufuliwa na kuanzisha viwanda vingine na kuweza kuwashajihisha wawekezaji kuanzisha viwanda vidogo vidogo, ili vijana wetu waweze kupata ajira na serikali yetu kuweza kupata fedha za kuongezea katika mfuko wake wa bajeti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Shirika la Biashara la *ZSTC*. Shirika hili kwa kweli ni muhimu kuwepo, lakini bado mimi nasema naliunga mkono kuweza kufanyakazi zake. Mimi nakumbuka katika kipindi cha nyuma shirika hili lilikuwa na tawi kule Dubai, tulikwua tunapeleka karafuu zetu kule. Kwa hivyo, ningemuuliza Mhe. Waziri je, kituo kile cha karafuu kule Dubai bado kipo na kama kipo kinaendelea na uuzaji wa karafuu. Kwa sababu Mhe. Saleh kazungumza sana, katika kusikitika kwamba kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhan wananchi wetu wamekuwa wakiwekeza karafuu zao kwa ajili angalau ya kuendesha matumizi katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani. Wanawekeza karafuu zao wakifikia kipindi hiki waweze kuuza na kupata fedha kwa ajili ya matumizi ya Ramadhani pamoja na skukuu kwa watoto wao. Lakini imekuwa hakuna soko la kuweza kuuza karafuu zile.

Kwa hivyo, ningemuuliza Mhe. Waziri kwamba kituo kile cha kule Dubei bado kipo na kama kipo ni maendeleo gani ambayo yanaendelea katika kituo kile ambacho kipo kule Dubai.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima hili la biashara na mambo mengine madogo madogo ambayo tunasafirisha nje. Kataja hapa Mhe. Waziri mambo mawili matatu ambayo yanasafirishwa nje ili kuweza kuipatia fedha nchi yetu pamoja na kuweza kuongeza uchumi katika nchi yetu. Mimi nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja je, amejipanga vipi katika kuleta maendeleo kwenye nchi yetu. Bidhaa gani nyengine mbali na zile alizozitaja, kwa sababu kataja hapa usafirishaji wa kaseti zile za video, redio pamoja na mitumba sijui. Sasa hii mitumba imenishangaza kwa sababu hatuna nguo za kusafirisha mitumba, lakini hapa imo mitumba. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja ana mikakati gani na mipango gani hasa ya kuweza kuzalisha bidhaa

nyengine za kuweza kuuza nje ya nchi na kuweza kupata fedha kwa ajili ya kupata faida na katika kuongeza pato la serikali.

Baada ya kuzungumza hayo, na mimi nimepata kukohoa kidogo kueleza machache niliyonayo. Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi na wenzangu sote tukiwa hai, wazima wa afya na tukiendelea na shughuli zetu hapa, lakini pia tukiendela na mwezi mtukufu wa Ramashani. Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na wewe vile vile kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, katika orodha ya shukurani zangu nitakuwa sifanyi wajibu wangu ikiwa sikumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Mimi naweza kusema kama tuna mawaziri ambao tunajivunia tulionao katika serikali yetu basi mmoja ni Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Katika kipindi kifupi alichokaa yako mambo unayaona mabadiliko makubwa katika wizara hii ambayo anaiongoza. Wala tusizungumze mambo ya karafuu na mambo ya sera na shughuli zilizotuleta hapa. Hata ukiangalia mandhari ya jengo tu analoliongoza basi ameweza kulibadilisha.

Mhe. Mwenyekiti, tulifika kuona baadhi ya watu walihama kwenye jengo lile wakenda kutafuta vyumba katika mahoteli wakafanya ndio ofisi za wizara, kwa sababu tu wameitupa. Lakini Mhe. Waziri alipoingia amefanya marekebisho makubwa. Sasa ukimleta mwekezaji au mfanyabiashara ukimwambia unakwenda kuonana na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwenye jengo lile, angalau atasema hawa watu kweli wako *serious*.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nasema kuna mafanikio mengi ameyaleta katika kipindi hiki kifupi. Ameweza kudhibiti kwa kiasi kikubwa bei za vyakula. Hii ni sifa ambayo inapaswa tuipe serikali kwa kupitia kwa waziri huyu, kwa sababu mfumko wa bei katika nchi nyingi za Afrika ya Mashariki, lakini kwa Zanzibar bado inabakia kuwa ni wa chini kuliko nchi nyengine zote za Afrika ya Mashariki. Suala la karafuu kama nilivyosema kila mmoja kaligusa hapa, kuongezeka kwa bei kumewanufaisha sana wakulima. Kwa hivyo, nasema Mhe. Mwenyekiti, yako mafanikio ambayo yanaonekana wazi wazi. Kwa hilo Mhe. Nassor Ahemed Mazrui anahitaji kupongezwa na kupewa moyo kwamba aendelee na kazi hii nzuri ambayo ameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo niseme bado tuna changamoto kubwa sana ya kuweza kukuza sekta hizi mbili kubwa ambazo zinasimamiwa na wizara hii. Sekta ya biashara na sekta ya viwanda. Mhe. Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu mimi bado changamoto hizi zinaendelea kutukabili ikiwa hatukulikabili suala la msingi kabisa ambalo linakwamisha ukuaji wa sekta hizi mbili. Yale mafanikio ambayo nimeyataja ni mafanikio ambayo yanatokana na jitihada za ndani. Lakini ukuaji mkubwa wa sekta hizi Mhe. Mwenyekiti, kwa nchi ya kisiwa kama Zanzibar, utakuja tu tutakapoweza kuwa na udhibiti wetu wenyewe wa sera za msingi za uchumi, fedha, sarafu na kodi huo ndio ukweli Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kihistoria ni nchi ya biashara, ni kihistoria kabisa. Katika kitabu maarufu cha wasafiri wa Kigiriki *The Periplus of The Erythrean Sea* kilichoandikwa takriban

miaka 2500 iliyopita. Wasafiri hawa walipotembelea ukanda huu wa Afrika ya Mashariki mwambao huu, walisema wameikuta Zanzibar ikiwa tayari inafanya biashara na nchi za mbali, zikiwemo nchi za Bara Hindi, Bara Arabu na nchi za Mashariki ya mbali mpaka China. Hicho ni kilele cha ustaarabu cha kuonesha jinsi visiwa hivi historia yake ilivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tukidhibiti wenyewe masuala hayo niliyoyataja. Hivi sasa hatuyadhibiti. Mhe. Mwenyekiti, kuna wakati fulani niko masomoni Uingereza nakumbuka, lilitoka jarida maarufu sana la biashara duniani *economist.* Wengine wanalijua hapa kina Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wanapitia pitia. Kulikuwa na toleo maalum kuhusu historia ya duniani. Katika gamba la jarida lile, yaani *cover* lile la juu kulikuwa kuna ramani ya asili iliyokuwa ikionesha mzunguko wa biashara basi Zanzibar iko katikati katika jarida hilo Mhe. Mwenyekiti, huko ndiko tunakotoka.

Sasa sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tunapata matatizo na mimi nasema sera za msingi zilizoleta mabadiliko katika sekta hizi mbili ni zile ambazo tumewahi kuziasisi sisi wenyewe hapa. Lakini leo zote zimeachwa nyuma. Mhe. Mwenyekiti, suala la kufikiria kuwa na bandari huru Zanzibar ilikuwa ni miongoni mwa nchi za mwanzo katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki na hiyo ni historia yake, kwa sababu mwaka 1892 ukenda katika gazeti rasmi la serikali la Zanzibar lilishaitangaza Zanzibar kuwa ni bandari huru. Ilipokuja serikali ya awamu ya tano ikajaribu kutaka kulileta suala hili, lakini tukakwama kwa sababu hatudhibiti sera zetu za kodi.

Mhe. Mwenyekiti. Tulitangaza maeneo huru, *Free Economic Processing Zones*. Lakini mpaka leo tumeshindwa kufika popote kwa sababu tumekwamishwa, kwa sababu ili uwavutie wawekezaji waje hapa ni lazima uweke vivutio, vile vivutio vinakuja katika kupunguza kodi au kuziondosha, hatuna mamlaka hayo. Leo Mhe. Mwenyekiti, wenzetu waliotukwamisha Tanganyika, wao wameichukua sera ile wameanzisha. Juzi naangalia katika taarifa ya habari, wameanzisha maeneo yale ya *Free Economic Processing Zones* na wanawavuta sasa wawekezaji waende kwao baada ya sisi kutukwamisha hapa. Mhe. Mwenyekiti hatuwezi kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, tulitangaza hapa kuanzisha sera za *offshore banking* na *offshore companies*. Wakati huo Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alikuwa ni Rais wa chama cha wafanyabiashara Zanzibar, yaani Rais wa *Chamber of Commerce*. Zilikuwa sera za serikali ya awamu ya tano zile na kwa uchumi unaotegemea huduma kama Zanzibar, uchumi wa kisiwa, *service oriented economy*. Haya ndio mambo ambayo yangeivuta Zanzibar ikachechemua uchumi wake.

Lakini vile vile tulifika mpaka kuandaa rasimu ya sheria hapa, ikataka kuwasilishwa dakika za mwisho kuumeni wenye maamuzi wakazuwia, kwa hivyo sheria ile haikupitishwa mpaka leo tumekwama Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni mifano michache tu ninayosema kwamba hayo ndio ambayo yangechechemua ukuaji wa biashara Zanzibar na hata ukuaji wa viwanda. Mhe. Mwenyekiti, sisi sehemu kubwa ya usafirishaji bidhaa zetu ni bidhaa za mpito. Kama hatudhibiti wenyewe maamuzi ya sera zetu za uchumi, hatuwezi tukasonga mbele hata siku moja.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hata katika mfumo huu tulionao sasa, ingelikuwa kweli mnatukwamisha na mnasema tuko wamoja, kwa hivyo sera tunaamua kwa pamoja. Mbona vinapotokezea viwanda vikawa vinazalisha Zanzibar vinapotaka kuchukua bidhaa na kupeleka Bara halafu wenzetu wanavitoza kodi. Palikuja mwekezaji wa kiwanda cha sigara mnakumbuka nyote hapa, akajakuwekeza katika ubinafsishaji wa kiwanda cha sigara kile, akawa anazalisha sigara zikawa na soko zuri tu Bara pale. lakini wenzetu walipoona tunapata wakaweka mkakati pakapigwa tozo kubwa za kodi, kiwanda kile mwekezaji kikamshinda akakifunga na viwanda vingi. Ndio maana leo wametuulia kila kitu, ndugu zetu wa damu wanaotupenda sana, wametuulia kila kitu kwetu limebakia hili la biashara ya magari nalo pia wameamua kulimaliza kwa kulikata roho.

Mhe. Mwenyekiti, juzi katuambia mwenyewe Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko katika semina pale, kwamba kuna gari zisizopungua 500 pale bandarini Zanzibar zimetoka Zanzibar, zimeshalipiwa ushuru Zanzibar na mamlaka inayosimamia ushuru ni TRA ile ile moja, lakini zimekwamishwa wanataka wawatoze tena ushuru, hivi hawa ndugu zetu wanatupenda kweli tunavyoambiwa hawa. Kitu pekee kilichobakia angalau vijana wetu wanajitafutia rizki ni hicho nacho kinataka kuuliwa. Sio kwamba kinataka kuuliwa ndio kimeshauliwa maaana yake sasa hivi watu wamekwama Mhe. Mwenyekiti, hawauzi na mtaji wao walioekeza pale umekwama, wala hatujui itachukua muda gani. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi hata siku moja kuweza kusonga mbele katika mfumo wa sasa wa Muungano uliokuwepo hata siku moja Zanzibar haitosonga mbele Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nawaambia Wazanzibari hala hala mti na macho. Wasije kukubali kumezeshwa sera za vyama vyetu, ikiwa CUF au ikiwa CCM wakashindwa hata kuyafanyia maamuzi mambo haya yaliyotukwamisha tusisonge mbele kama nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema kama tunataka kuondoka hapa tulipo, kama tunataka kuwa na udhibiti wa sera zetu, basi ni lazima tuwe na mfumo mpya wa Muungano ambapo Zanzibar itakuwa na mamlaka kamili kitaifa, na kimataifa kusimamia kila chake chenyewe na Tanganyika wawe na lao, wawe na mamlaka kamili kitaifa na kimataifa wasimamie wenyewe na halafu pawepo na mashirikiano kwa kupitia Muungano wa Mkataba.

Mhe. Mwenyekiti, na hii nataka kuwawekea sawa msije mkasema anazungumza serikali ya mkataba, hakuna serikali ya mkataba, kuna Muungano wa Mkataba, tusimamiwe na kamisheni kama ilivyokuwa Ulaya inatosha kabisa, kila mtu akae na serikali yake na mamlaka yake kamili. Hatuwezi kila siku vijana wetu wanajihangaisha wanatafuta maisha, lakini kuna wenzetu wanawakwamisha. Halafu watakuja wengine hapa kwa unafiki wetu humu ndani watakuja kutuletea mfumo huu. Halafu tunakuwa na mdomo mrefu kuyakosoa haya, lakini tunataka kutafuta ufumbuzi dawa, basi humu humu ndani tunapigana vita Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tukafika. Wazanzibari wenyewe nashukuru wameamka hasa vijana wa kizazi kipya, nawaomba ukija mfumo huu wasimamie kwa ukamilifu Mhe. Mwenyekiti, ili kulidai hili ili Zanzibar iweze kufanya maamuzi yake mazito yatakayoweza kuifanya ikatoka hapa ilipofika ikakwamuka Mhe. Mwenyekiti, tukasonga mbele tukapumua.

Nikiondoka hapo naomba niseme kwamba tukiweza kufanya maamuzi hayo, ndipo Zanzibar tutakapoweza kukwamuka. Mhe. Mwenyekiti, Ulaya wameanzisha Umoja wa Ulaya, lakini

Uingereza ilifanya maamuzi baadhi ya mambo ikakataa kuyaingiza, kwa nini? Kwa sababu Jiji la London kwa maumbile yake ndicho Kituo Kikuu cha Fedha za Biashara kwa Ulaya. Vile vile na wao pamoja na kwamba wanazalisha lakini hadhi ya London inatokana na *service* wanazozitoa katika huduma za kiuchumi na kifedha.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ilipaswa iwe hivyo katika huu Ukanda wa Afrika ya Mashariki na huko tulikotoka ndivyo ilivyokuwa Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ninachosema hili ni muhimu sana katika kuifanya Zanzibar ikakwamuka kibiashara hapa ilipo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie moja hili katika masuala haya, ametutajia kwenye hotuba yake ukurasa wa 44 na 45 masuala ya Ushirikiano wa Kikanda. Nakuja pale pale amesema kwamba unatafutwa ushirikiano wa *SADC, COMESA* na Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

Swali langu ni kwamba amesema na sisi tunashiriki, je tunashiriki katika kufanya maamuzi ya kisera au ndio kama kawaida tunashirikishwa katika ngazi ya utaalamu, ambao wao wakifika kwenye maamuzi ya sera hawana maamuzi.

Sasa kama hana maamuzi katika ngazi ya sera, Zanzibar anaiamulia nani au anaiwakilisha nani katika maamuzi ya kisera, kwa sababu maeneo haya si ya Muungano tuna-*competing interest*, yaani tuna maslahi yanayopingana sisi na ndugu zetu wa Tanganyika. Mhe. Mwenyekiti, sasa wao wanapotuwakilisha kule sisi nani anasimamia maslahi ya Zanzibar katika maamuzi ya kisera kwenye Mahusiano haya ya Kikanda pamoja na Ushirikiano wa Kikanda.

Mhe. Mwenyekiti, nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu anakumbuka, kwani nakumbuka mpaka leo na wala sijasahau ilipoamua Tanzania kujitoa katika *COMESA*, ili ijiunge katika *SADC* na Mhe. Waziri wakati ndiye alikuwa Rais wa Chama cha Wafanyabiashara Zanzibar, naikumbuka mpaka leo *Press Conference* aliyofanya yeye akina Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali na wenzake kupinga maamuzi yale kwamba Zanzibar haitanufaika katika *SADC* kama ambavyo inanufaika kupitia *COMESA*, lakini maamuzi yanaamuliwa kuumeni.

Kwa kweli tunaambiwa kila siku Muungano huu ni ndoa na mimi huuliza mume nani na mke nani, siku hizi tunamjua maana yake mwenye maamuzi ndiye mume Mhe. Mwenyekiti, basi wakaamua wao. Sasa leo kunazungumzwa *tripartite*, kwamba *SADC, COMESA and East Africa*. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atusaidie katika kufanya maamuzi ya masuala haya hii mikutano, sisi maamuzi ya kisera anatuamulia nani Zanzibar nilikuwa naomba akija aje anisaidie.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri katika ukurasa wa 45 wa kitabu chake ameorodhesha mlolongo wa maeneo, ambayo Jumuia ya Afrika ya Mashariki kama *block* kwa umoja wake linafanya mazungumzo na nchi mbali mbali kubwa za kiuchumi bila shaka kutafuta maslahi ya kiuchumi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa nchi za wenzetu inawezekana kwa maumbile yao yalivyo wao wakafaidika na mfumo huu. Lakini mimi niulize kwa uchumi kama wa Zanzibar wa kisiwa unaotegemea kutoa huduma na biashara za mpito kwa sababu sisi hatuzalishi wenyewe hapa.

Hivyo, sisi tunategemea tutafaidika katika *negotiation* hizi, na kama hatufaidiki tunajiepusha vipi kuja kufungika na mapatano ya jumla kupitia *Block Negotiation ya East Africa Community*, ambayo Zanzibar itakuwa haina maslahi nayo, tunajilinda vipi katika hayo. Hili naomba pia Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie.

Vile vile naomba maelezo katika ukurasa wa 26 wa kitabu cha Hotuba ya Mhe. Waziri, ametuambia pale kwamba katika yale masuala ya kuweka Maonesho ya Kibiashara na kuendeleza eneo la Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya Kibiashara, ametuambia kwamba walishapeleka mradi huu uweze kudhaminiwa kupitia *BEST* na *UNDP*, inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Lakini wakasema imeshindwa kufanyika pamoja na wizara kufanya matayarisho yote, kwa sababu haikupata ufadhili. Nadhani hebu tuambiwe katika hii *BEST*, kwa sababu tuliwahi kupata taarifa kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwamba kuna baadhi ya miradi ya *BEST* ambayo ilikwama kwa sababu tu ndugu zetu wa damu wanaotupenda sana waliikwamisha.

Mhe. Mwenyekiti, wanatuambia mwaka wa fedha umekwisha wakati hao wafadhili wenyewe wanasema hapana mnaweza kuomba bado mwaka wa fedha haujamalizika. Ndio maana fedha hizi zikashindwa kupatikana na tuliwahi kupewa maelezo hayo baadhi yetu katika kamati Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja aniambie na hili kwa wizara yake lilikuwa hivyo hivyo ama lilikuwa tofauti, naomba akija anisaidie maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, haya nimeyazungumza kwa upana wake kwa sababu haya yanaathiri yote, yaani yanaathiri viwanda pamoja na ukuaji wa biashara Zanzibar, kwa sababu hatuna maamuzi yale ambayo tunahitaji kwa ajili ya maendeleo yetu.

Sasa niende *specifically* katika maeneo machache tu Mhe. Mwenyekiti. Katika suala la Sekta ya Viwanda na yale ya jumla tayari nimeshayazungumza, lakini kuna lile ambalo limezungumzwa hapa; kwamba ili tuweze kushajihisha ukuaji wa viwanda Zanzibar, basi lazima zile *factors* ambazo zinazopelekea watu kuvutika ziwepo. Kwa mfano, umeme wa uhakika, maji ya uhakika, miundombinu ya wazalishaji ambayo wanaweza kufanya kazi, mitaji na watu wetu kuwa na maarifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika haya umeme umezungumziwa sana na wala sitaki kuzungumzia, kwamba tunahitaji Zanzibar kuwa na umeme wetu ambao utatusaidia kuwa na umeme wa uhakika na kuwapa uhakika wawekezaji kuja kuwekeza Zanzibar, maji tunapambana na nafikiri tukipambana zaidi tunaweza kupata.

Lakini naomba nizungumzie hili la miundombinu, Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kukuza viwanda na biashara kama hatuna bandari ya uhakika. Na sisi historia yetu kama nilivyosema ni nchi ya biashara, lakini kwa bandari hii tuliyonayo haiwezi kufanya shughuli hiyo, kama unazungumzia biashara kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma amesema hapa na mimi nataka nimuunge mkono, kwamba kwa mikopo tunaona hali ilivyo, lakini unapewa *cost* kubwa, yaani huyo unayemkopa anakwambia uchukue mkandarasi wake.

Swali langu lipo kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, hivi katika Mfumo wa *Build Operate Transfer* na siku hizi kuna mpya unaoitwa *Build Finance Operate Transfer (BFOT)*, hivi tunashindwa kupata mwekezaji akaingia katika eneo hili.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, wapo wafanyabiashara wakubwa ambao tayari wameshawahi kunitajia hili, na sasa mimi niwambie ikiwa Mawaziri wameshindwa basi labda watuteue mimi na Mhe. Hamza Hassan Juma tuchakarike na twende tukawatafutie sasa huyu mwekezaji mkubwa atakayekuja kujenga bandari kwa msingi wa *BFOT*.

Lakini mimi siamini kama watu wataweka maslahi yao pembeni na ikiwa tunatafuta *commission* zetu, basi tutaendelea kutafuta mwaka mzima hatupati. Isipokuwa mimi naamini kama kweli tutaweka maslahi ya nchi mbele, basi naamini tunaweza kumpata mwekezaji wa maana na akakubali kujenga hapa na akajilipa fedha zake, baadaye akaikabidhi nchi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi kile kipindi ambacho anajilipa uwekezaji wake, tunafaidika katika kuongeza *volume* ya biashara pamoja na uwekezaji katika nchi na wala si lazima tupate moja kwa moja katika kipindi kile kutokana na mapato ya bandari na yale tumuachie ajilipe mpaka amalize.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tutapata ukuaji wa *volume*, yaani kiwango cha biashara, uwekezaji pamoja na ajira zitakazotolewa ndani ya nchi haya yote yataongezeka na haya ni *returns* pia yanaongeza mapato katika serikali na mzunguko utakua. Mhe. Mwenyekiti, nasema hebu hili tuliangalie tena hili nalisema kwa sababu, naona umesogelea *microphone* naomba unigaie muda wako kidogo nimalizie Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuongeza dakika tano za ziada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli haya ninayasema kwa sababu si hili tu, mimi nahisi tuna tatizo katika kufanya maamuzi kwenye serikali yetu na wala si suala la kwamba hakuna watu wa kuwekeza, isipokuwa tunalo tatizo la urasimu katika kufanya maamuzi yetu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa mfano, alikuja mwekezaji ambaye alitaka kujenga Kiwanda cha Saruji hapa tukatishana hapa kuhusu mazingira. Hivi Mhe. Mwenyekiti, tunajali sisi dunia nzima na wala hakuna nchi ya kisiwa yenye Kiwanda cha Saruji. Sasa kama tuna *failure* zetu katika *management*, basi tusikatae uwekezaji, isipokuwa sisi tuimarishe *management* yetu katika suala la ku-*preserve environment*.

Mhe. Mwenyekiti, walipopewa pendekezo hilo mawaziri walikwenda Kisiwa cha Langkawi Malaysia hawa na kama sikosei Mhe. Waziri mwenyewe alikuwemo katika safari hiyo. Kwa kweli Kisiwa cha Langkawi ni kidogo kuliko Zanzibar kinaingiza watalii wengi kuliko Zanzibar, lakini kinapendeza kwa mandhari ya kijani, kwa sababu wamesimamia vizuri tena wanacho kiwanda cha saruji ndani yake.

Lakini kwa *technology* ya kisasa hakitoi vumbi wala moshi na lile eneo walilowekeza limewekwa uhakika kuweza kuwa linarejesha hali yake kila linapomaliza, na dhima hii si ya serikali ni dhima ya wale waliowekeza Kiwanda cha Saruji.

Sasa leo sisi tunakataa, hivi ni nchi gani itakayoendelea ikawa haizalishi saruji yake wenyewe, kwa sababu nchi inataka kujenga kwamba na utangojea saruji ya kuagizia kila siku Mhe. Mwenyekiti, pia kuna ajira. Kwa hivyo, mimi ndio ninasema mara nyengine tusitafute *short cut answers* kwa maswali magumu, kwamba kutaharibika mazingira na wala tusiruhusu viwanda, kwa maana hiyo tutakuwa haturuhusu kiwanda hata kimoja Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuhofia mazingira katika nchi hii.

Suala ni vipi watendaji wetu wanafanyakazi kazi yao ya kusimamia sheria na tukisimamia sheria tutapata viwanda, tutajenga na tutatunza mazingira yako Mhe. Mwenyekiti. Kwa hiyo, nasema tunalo tatizo katika maamuzi Mhe. Mwenyekiti na katika kusimamia mambo yetu. *(Makofi)*

Vile vile kuna miradi mingine mikubwa wanaijua serikali wenyewe hapa, kwamba wamekuja wawekezaji wa maana Mhe. Mwenyekiti wanataka kuwekeza *over hundred million dollars* katika *project* zimekwama mpaka leo, kwa sababu serikali inashindwa kufanya maamuzi, hivi mpaka lini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hii mukikwamisha serikali hamfanyi maamuzi Mhe. Mwenyekiti wakikwamisha hawa wanatukwamishia ajira, mapato katika nchi yetu pamoja na ukuaji wa uchumi katika nchi yetu na kwa nini tuendelee kusubiri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwa haraka dakika chache zilizobakia kwenye Sekta ya Biashara. Mimi nataka kuiomba serikali, tena namuomba sana Mhe. Waziri hili mbali ya zile *factors* alizotutajia katika ukurasa wa 35 kwenye kitabu chake pamoja na maeneo mengine yanayokwamisha biashara.

Nadhani ni vyema akaiangalia na ile ripoti Mhe. Waziri kuhusu *Doing Business in Zanzibar 2010,* serikali imeomba msaada wa *World Bank* wamefanya *research* na wamekuja na *report* nzuri kabisa. Kwanza mimi nimefurahi kwamba Zanzibar imeingia katika orodha ya nchi ambazo zina *Report* yake yenyewe ya *Doing Business*, kwa sababu *Doing Business in the World* ni mfumo ambao kila nchi inakuwa na *report* yake.

Sasa mule wameonesha maeneo na wala sitaki kuyataja hapa kwa sababu sina muda, wameonesha maeneo ambayo Zanzibar yanawakwaza isiweze kusonga mbele kibiashara. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ayatizame maeneo yale na ashauriane na wenzake huko BLM, kwamba yepi yanayokwamisha na zichukuliwe hatua, ili kufanya sisi tuweze kusonga mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka Mhe. Waziri amezungumza suala la kuangalia ubora wa bidhaa naomba nimalizie hili kwa haraka. Mhe. Mwenyekiti, bado mimi namwambia Bodi yake ya Ukaguzi inahitaji ifanye kazi ya ziada, kwa sababu bado bidhaa ambazo hazifai zinaingia, na mimi namuomba mara kwa mara atembelee pale Marikiti maeneo ya Zakaria pale, akatizame wale wanaomwaga vyakula vyao chini pale akavitizame vile tarehe zake za kumalizika muda wake.

Kwa kweli wanajitahidi Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, lakini bado tuna tatizo. Sasa sijui baina ya hii yake yeye na ile ya Ukaguzi maana yake huu muingiliano wa majukumu wakati mwengine unakuwa unachanganya huu, nani wanaohusika pale watusaidie halafu watutajie, ili wananchi wetu wasiweze kuathirika katika mchele na mambo mengine.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Shirika la *ZSTC*. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atusaidie kuna nini *ZSTC*, anaye Meneja Mkuu Mhe. Waziri, anaye Meneja Masoko, kwa nini huyu Meneja wa Masoko hapewi ruhusa ya kufanya kazi yake na kila kitu amedhibiti Meneja Mkuu.

Kwa mfano, kuna safari za kwenda kutafuta masoko anakwenda Meneja Mkuu na Meneja Masoko anaachwa, hasa Meneja Masoko amewekwa wa kazi gani pale analipwa mshahara bure, naomba Mhe. Waziri aje atusaidie. Vile vile kama anakwenda aje atusaidie ile ofisi iliopo pale Dubai inafanya kazi gani? Kwa sababu kama inabidi musafiri mwende mukatafute masoko basi nafikiri ile ofisi musiilipie kodi mkatubebesha mzigo bure, bora muifunge tujue moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme na mimi naungana na Mhe. Hija Hassan Hija sitaki kupoteza muda tena, basi yale mafungu aliyoyaombea maelezo na mimi nayaombea maelezo. Mhe. Waziri wizara yako ukijumlisha fungu la safari kwa ujumla wake idara zote kuna shilingi 307,089,000/=.

Lakini yale mengine Mhe. Waziri wa Fedha tayari ameshatuahidi kwamba anayafanyia hesabu ya jumla jumla na wala sitaki kuyahoji, isipokuwa kuna maeneo machache tu ambayo ninataka kwa haraka Mhe. Mwenyekiti, nje ya yale ya kawaida ambayo tumeshazoea kuyahoji, naomba akija Mhe. Waziri atusaidie maelezo.

Kwanza katika idara ya Mipango Sera na Utafiti katika Fungu la Gharama za Vifaa na Huduma za Mawasiliano kuna ununuzi wa Kanda za Kurikodia na Santuri shilingi milioni 10,500,000/=. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anisaide Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wanarikodi santuri gani kule, ili na sisi tuweze kujua. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kuhusu utayarishaji wa mpango wa Bajeti kuna shilingi milioni 32,000,000/= ni fedha nyingi sana.

Pia ukiondoa yale maeneo ya jumla Mhe. Mwenyekiti, niliyoyataja pale katika Idara ya Utumishi kuna Fungu la Posho la Mazingira ya Hatari (*Risk*), na hili nimeliona katika wizara hii tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja anisaidie maelezo yake.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwenye mafungu haya kuna Fungu la Ruzuku la Kamisheni ya Kusimamia Ushindani wa Biashara na Fungu la Mamlaka ya Mizani na Vipimo. Mhe. Mwenyekiti, haya katika hotuba yake mwenyewe Mhe. Waziri alionesha kwamba hata utendaji kazi wa taasisi hizi bado haujaimarika. Sasa kwa nini tuendelee kuidhinisha shilingi milioni 200 au 250 kila mwaka wakati utendaji kazi wenyewe wa taasisi hizi ni wa mashaka makubwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naunga mkono hoja hii, lakini naomba maelezo kwa yale maeneo ambayo nimeyaombea maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunivumilia na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mhe. Salim Abdalla Hamad, tujitahidi kuzingatia muda na baadaye atafuata Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi fupi ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukurani za dhati kwa kupata nafasi hii. Pili kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake kwa namna alivyoisoma na tumeifahamu vizuri, na pia kwa mara ya mwanzo kupata mtu aliyeomba dua kama ile tokea wakubwa wetu wa serikali mpaka kwa wananchi Mwenyezi Mungu aijaalie dua hii iwe maqbuli. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kuhusu suala la karafuu. Lakini kabla sijaanza kidogo tumesikia Waheshimiwa Wajumbe wenzetu wamechangia hapa na kumtaka Mhe. Waziri ashughulikie ununuzi wa hizi karafuu uwe endelevu, ili karafuu zisisafirishwe kwa njia ya magendo na imetajwa hapa katika majimbo yanayosafirisha majimbo ni Jimbo la Mtambwe na leo ni mara ya pili.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa hili naomba kutoa taarifa rasmi na tunajua sisi hatutoi taarifa mpaka tufanye utafiti, ni kuwa wananchi wa Jimbo la Mtambwe ni wenye kuipenda sana serikali yao, na wameiunga mkono kwa kupambana na watu wanaouza karafuu kwa magendo ambao si watu wa Mtambwe na wameunga mkono kwa kupeleka karafuu zao vituoni.

Kwa hivyo, naamini kwa msimu uliopita wa karafuu ikiwa si wa mwanzo katika majimbo bora yaliyouza karafuu kwa wingi ni Jimbo la Mtambwe, kwa kutumia vituo vya zamani, vipya vilivyojengwa na mpaka vya muda na vyote vilikuwa kila siku vikinunua karafuu kupita kiasi nashukuru kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mtambwe ni jimbo lililokuwa linapakana sana na bahari, ina maana kama kuna magendo kwenye bahari si lazima yawe ya watu wa Mtambwe kwa hili nawatetea sana. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia pamoja na kuwa Shirika hili la *ZSTC* lilikadiria kununua karafuu tani 3,000/= tu katika msimu uliopita. Lakini badala yake limenunua tani 4,822.8 na imetumia jumla ya fedha za Tanzania bilioni 72 na milioni 100. Vile vile shirika hili limeuza tani 4,040.75 za karafuu kwa jumla ya fedha za Tanzania bilioni 83 na milioni 600. Pamoja na kuwa imenunua karafuu kwa asilimia 80 ya bei ya Soko la Dunia kwa kuwaonea wakulima huruma, basi shirika hili limeingiza jumla ya faida bilioni 11 na milioni 500.

Sasa kutokana na karafuu walizonunua kutoka kwa wakulima na karafuu walizouziwa, nashukuru tuna ziada ya tani 7,801.05, ambayo kama zikiuziwa kwa bei ya hiyo iliyouzwa karafuu zilizopita itakuwa ni shilingi bilioni zisizopungua 16 na milioni 160, hii ni faida kuwa sana pamoja na huruma kubwa ya shirika hili kuwaonea wananchi kwa kuwanunulia karafuu zao kwa bei ya juu na naomba iendelee hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, shirika limejidhatiti kuimarisha zao hili la karafuu. Kwa hivyo, kuna mambo mengi ya kufanya, kwa sababu hili zao ni la kudumu na hivyo kuna mambo ni lazima yatekelezwe yawe endelevu, ili huko usoni iwe shirika linaingiza faida kila wakati karafuu zinapozaliwa.

Kwanza naomba sana kwa vile Zanzibar kuna mikarafuu mingi tu, lakini kuna mingine ni mizuri mashada yake ni makubwa na mingine mashada yake ni madogo tunaita mbili mbili kule Pemba. Kwa hiyo, shirika liimarishe zao hili la karafuu kwa kuiendeleza mikarafuu iliopo na kuwahamasisha hao wananchi kwamba hao wakulima kuishughulikia mikarafuu yao ipasavyo. Vile vile na kupanda mbegu zile za asili ambazo ni nzuri pia kuendeleza katika miche ya kutosha, ili mikarafuu iweze kupandwa kwa wingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, ili zao hili liwe endelevu wakulima wetu wa karafuu wakati wanapovuna karafuu, kwa sababu ya mikarafuu ilivyokuwa ni mikubwa huwa wanafanya mtindo ambao ni wa hatari sana wa kuikata sana mikarafuu. Kwa mfano, kuna wengine wanakata matawi makubwa sana, na wengine kwa bahati mbaya wanaukata wote mzima kwa kupunguza kazi.

Kwa hivyo, naomba shirika lijitahidi sana kuwaelimisha wakulima wa karafuu pamoja na wachumaji wa karafuu, kuwa ukataji huu unasababisha mikarafuu yetu kufa kwa wingi na ni hasara kwa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka kabla ya Mapinduzi niko katika darasa la sita katika msimu kama huu magazeti yalikuwa yakieleza hasa "*Pruning of the Clove Trees is Strike Prohibited*", yaani ukataji wa matawi ya mikarafuu unakatazwa moja kwa moja, lakini sisi tunauendeleza na wala sijaona hatua za kimsingi zinazochukuliwa. Kwa hivyo, naomba pia na hili wizara itilie maanani.

Jambo jengine wizara waliloshuhudia katika msimu wa karafuu uliopita ni upungufu wa vituo, kwa sababu hapo mwanzo karafuu ilikuwa hazishughulikiwi ipasavyo, kwa hivyo vituo vimekuwa ni kidogo na wamepata hasara kubwa sana ya kujenga vituo vipya na imebidi waazime baadhi ya maghala kwa kuweka vituo vya kudumu. Kwa hiyo, kwa kuimarisha ununuzi wa zao hili la karafuu, moja ni kupeleka huduma karibu na wananchi.

Kwa maana hiyo, naomba kwa mule ambamo wizara iliona iko haja ya kujenga vituo kutokana na wananchi walivyoitikia kuuza karafuu zao kwa serikali, basi wajitahidi vituo vile vijengwe na mule walimokuwa wakitumia vituo vya muda pia namo munahitaji kujengwa vituo. Pamoja na suala la ukarabati wa vituo ambavyo vimezeeka hili ni jambo la lazima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nijiulize katika maelezo yao ya wizara hii Mhe. Waziri amesema kwamba kuna utaratibu wa kupunguza watu kutokana na sheria ilivyo na watu wenyewe ni wafanyakazi wa wizara hii.

Kwa kweli mimi naelewa kuwa kila mwaka wanapunguzwa, lakini inapotokea ununuzi wa karafuu, basi wizara inabidi kuajiri watu kutoka wizara nyengine kwa ajili ya ununuzi wa karafuu, na watu wale huwa *special* kwa ajili ya kununua karafuu, kwa bahati mbaya huona pia ni msimu wao wa kuwakata wananchi kwa manufaa yao binafsi.

Sasa suala hili la kuwapunguza wafanyakazi, lakini wakaajiri watu wa wizara nyengine, sijui Mhe. Waziri hapa atanieleza vipi wakati watu wapya hawa wanakuja na mikakati ya kuwa wakiondoka waondoke na chochote, kwa hiyo wanatuumiza sana tunaouza karafuu zetu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba karafuu hizi zijazo wizara imejipangia kununua tani 3,000 mpaka 4,000. Kwa msimu uliopita walijipangia kununua tani 3,000 na wakapata 4,822 kama nilivyosema. Je, kama Mwenyezi Mungu akitujaalia zikazaliwa karafuu na ikawa zipo za kutosha kuliko hizo tani 4,000 na hizo nyengine ni vipi zitabakia tu majumbani.

Kwa hivyo, ushauri wangu hapa kwa vile serikali ndio kwanza inatafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa karafuu, basi wangeliweka kuanzia tani 3,000 mpaka 5,000, ili tusije kukwamwa hapo njiani.

Vile vile naona nitumie fursa hii kwa kutoa pongezi kwa Benki yetu ya Watu wa Zanzibar kwa namna walivyounga mkono ununuzi wa karafuu katika hali ambayo Mhe. Waziri anaielewa yeye mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la biashara ya mwani. Mimi hofu zangu ni kuwa *ZSTC*, walikuwa wakishughulikia karafuu, makome, mwani pamoja na biashara nyengine, yaani ilikuwa *totally* ikijishughulisha na biashara. Kwa kweli mimi nilifarajika katika kitabu kilichopita kuona kuwa wizara iliazimia kulishughulikia zao hili la mwani na wakulima wafaidike kama wanavyofaidika watu wa karafuu.

Lakini kitabu chetu cha leo kimesema kwa sababu kuna muundo mpya na shughuli nyingi za wizara hii kwenye Shirika la *ZSTC*, kwa hiyo kazi hii hawataweza kuishughulikia ipasavyo; na badala yake watashirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kushughulikia zao la mwani.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa fikra zangu binafsi naona hakuna wizara inayoweza kuwasaidia wakulima wa mwani isipokuwa ni wizara hii, kwa nini waliweza kwenye karafuu na wasiweze kwenye mwani? *(Makofi)*

Kwa hivyo, pamoja na kazi kubwa waliyonayo na sababu walizozieleza, lakini naomba msimamo uwe pale pale, kwa vile wakulima wa mwani ni wengi tena ni mama zetu na wanapata tabu sana na bei tunajua ni ndogo kwa sababu mwani biashara imekuwa huria kwa kila anayetaka kununua.

Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara ifanye kila inavyowezekana iwashughulikie hawa wakulima wetu, ili wafaidike na bidhaa hii kama wanavyofaidika wakulima wa karafuu.

Halafu kitabu kimeeleza kuwa wanafanya utafiti ni mazao gani yanayoweza kusafirishwa nchi za nje. Mhe. Mwenyekiti, kwa hili mimi niseme kuwa Zanzibar kama nilivyosema wizara iliyopita ni kwamba Mwenyezi Mungu amejaalia kila aina ya mazao hapa yanapatikana. Kwa mfano, kuna pilipili manga, mdalasini pamoja na *spices* zote zina soko duniani, pia tukija kwenye matunda, kama vile embe, mafenesi, mananasi, mabungo, mapapai na mengi mengineyo yote yana soko. *(Makofi)*

Lakini kuna utaratibu ambao mimi mwenyewe unanishangaza Mhe. Mwenyekiti, sisi tunazalisha hapa lakini hata hichi kinachozalishwa lazima tukitumie. Mhe. Mwenyekiti, kuna huu mpango wa biashara uliopo mara zote unaingiliwa na biashara kutoka nje ya Zanzibar tokea mali ya wakulima mpaka mali ya viwanda. Kwa maana hii matokeo yake ni kuwa biashara zetu zimeanguka moja kwa moja.

Kwa mfano, kuna wafugaji wengi sana hapa wa kuku na ilikuwa sisi kuku tusafirishe kupeleka nje, lakini wanakaa mpaka wanakufa kwa maradhi wanakosa soko kwa sababu ya Paja Nono, yaani kuku wanaotoka nje na dawa kwa sababu bei ni ndogo, basi tunakwenda huko na kuwaua wakulima wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunazo nazi nyingi sana lakini kumeingia biashara ya nazi kutoka nje bei ni ndogo na hizi zetu hapa inakuwa zinaanguka soko, pia watu wanalima mboga mboga na kila kitu. Sasa sisi wenyewe imeshatujaa katika fikra cha nje ndicho bora. Kwa hivyo, mimi naona kwanza tuwe na msimamo wa kutunza kilicho chetu na baadaye tuangalie kwa wenzetu.

Kwa maana hiyo, naiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ifanye kila inavyowezekana kwa kujuana na wakulima na wafugaji wapange mambo ya soko, thamani na kadhalika na ikiwa kuna *package* mambo mengine yafanywe. Lakini tuone kwanza tunashughulikia vitu vyetu wenyewe na baadaye ndio tunashughulikia kutoka nje.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, hii ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, mara tu baada ya Mapinduzi kulijengwa viwanda vingi sana tena vya maana. Kwa mfano, kulikuwa na Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Sigara, Kiwanda cha Sukari pamoja na Viwanda Vidogo Vidogo na kama sikosei mpaka Kiwanda cha Nguo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yale yalikuwa ni maendeleo makubwa ya Wazanzibari yaliyowekwa na viongozi wetu waliopita. Sasa leo viwanda vyote vimekufa na wala hakuna kimoja kinachofanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wito wangu kwa wizara ni kufanya utafiti wa kina kujua kwa nini viwanda hivi vikafa tokea uendeshaji wake ndani ya nchi na halafu uwiano na masoko kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vyovyote vile inafika wakati lazima na sisi tuwe na viwanda vyetu ambavyo vitakuwa endelevu na wala hatutegemei sana malighafi kutoka nje. Kwa mfano,

hakuna sababu ya kutokuwa na Kiwanda cha Kusindikia Minofu ya Samaki kutokana na bahari ilivyotuzunguka pamoja na samaki wengi tulionao, isipokuwa ni mpango mzuri wa kuuweka na kuona kuwa hili tumeanzisha.

Vile vile kwa matunda yote tuliyonayo ya kila aina na mengine ni ya mwitu tena yanayosifika dunia nzima mabungo, hakuna sababu kuwa hatuna hata kiwanda cha kusindikia matunda yetu hapa tukapata malighafi hapa, na kadhalika na badala yake ikawa tunaagiza nje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa mambo mawili madogo tu, tena nakuomba unipe nafasi ya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda na wengine wawahi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuwaeleza wananchi wetu, serikali kwa makusudi imeondoa kodi kwa vitu muhimu kama vile chakula kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa nchi hii. Kwa kweli serikali inajua umasikini tulionao na ndio ikaondoa ushuru wa mambo kama hayo, ili tuuziwe kwa bei rahisi tuweze kufaidika.

Kwa hiyo, nawaomba wazanzibari wenzangu wasiitumie fursa hii ya kupata chakula ambacho cha kutusaidia sisi wenyewe, na badala yake tukakisafirisha kwa kukipeleka nje kwa ajili ya kutafuta bei kubwa, yaani ikawa tunaua sisi kwa sisi kwa wachache kufaidika kwa bei kubwa. Kwa maana hiyo, hili naomba tulipige vita kwa vyovyote vile, lazima tuheshimu azma ya serikali kuondoa ushuru ule. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka kuna baadhi ya viwanda vimefunguliwa vya wananchi kama vile Mtambwe ninacho Kiwanda cha Sabuni na Mhe. Waziri anakijua na hivi sasa kinazalisha kwa wingi, lakini kwa bahati mbaya hakijakuwa na utaalamu wa *package*, hivyo bidhaa zao ni nyingi lakini faida si kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akifuatilie kile kiwanda na baada ya kukifuatilia akisaidie, ili lengo lililokusudiwa liweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kumuuliza tu Mhe. Waziri, kwamba Mhe. Waziri alitumia fedha nyingi sana kutengeneza barabara kwa kufanya *gridding*, ili karafuu zikauzwe vituoni na barabara zile Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hawakuzishughulikia na mvua zinakuja na karafuu zinazaliwa tena na tutahitaji hasara mpya. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuona kuwa ile kazi waliyoifanya haikupotea bure kwa manufaa yetu? *(Makofi)*

Mwisho ni swali kwa Mhe. Waziri hivyo sisi hatuwezi kwenda bila ya *TRA*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, shukurani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hujaunga mkono hoja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimesahau kutokana na usomaji mzuri uliotangulia na uzito wa kitabu kilivyo na azma zake kwa maslahi ya wananchi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Anayefuata sasa Mhe. Fatma Mbarouk Said tunamuomba azingatie muda na baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache katika Hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake hii kwa muda muafaka na pia niwashukuru watendaji wake kwa kumuandalia bajeti yake hii.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, niseme jambo lolote ni lazima liwe na mkakati. Wizara hii ya Biashara, ni wizara muhimu ambayo kama ilivyotafsirika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Biashara ni kama inavyojulikana kama biashara ni kuuza na kununua, na viwanda ni viwanda ambavyo vitakuwa vinasindika na yale yanayosindikwa yanahitaji kuuzwa.

Zanzibar kihistoria au kimaumbile ni visiwa ambavyo vinazalisha matunda mengi tu na mpaka hivi sasa tukitizama bado matunda yanakuja kwa msimu yanakuwa mengi, lakini baadaye matunda yale inakuwa wale wakulima hawafaidiki ipasavyo. Kwa mfano, msimu wa machungwa, basi machungwa yanakuwa mengi na ingekuwa serikali ina viwanda basi tungeweza kusindika na tukauza nchi za nje, lakini hilo halipo. Vile vile kama tungekuwa na viwanda tungepata ajira kwa vijana wetu pia na hilo halipo.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa tano Mhe. Waziri ameelezwa kwamba kwa mwaka 2011 mwenendo wa Uchumi na Biashara Duniani uliendelea kuwa wa kuyumba licha ya juhudi kubwa za kufufua kutokanana na athari za kuanguka kwa masoko ya fedha, hisa na athari za madeni zilizojichomoza kutokana na ule Mtikisiko wa Uchumi wa Ulimwengu. Kwa kweli hili haliwezi kuepukika, kwa sababu kama sisi Zanzibar tukiwa ni sehemu ya ulimwengu hili ni lazima litatokea.

Lakini serikali nayo ina jukumu la kuchukua juhudi, ili kuona kwamba tatizo hili kwa hapa ndani sijui Mhe. Waziri nimuulize kwa hapa ndani alichukua hatua gani, ili kukabiliana na matatizo kama haya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende ukurasa wa 8 kuhusu hali ya kibiashara Zanzibar. Mhe. Waziri ameeleza kwamba kwa upande wa Zanzibar na kama ilivyoarifiwa katika bajeti ni kuwa usafirishaji wa bidhaa ulifikia milioni 261.4.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atuambie ni bidhaa za aina gani, kwa sababu hapa tunavyojua ni zao la karafuu ndio zao kubwa la biashara na wala hakuna chengine tunachokijua na mwani pia nayo. Lakini labda kutakuwa na bidhaa nyengine zaidi, kwa sababu tunaweza kuwajuilisha wananchi wetu ambao wanaotusikiliza hivi sasa wakajua ni bidhaa gani ambazo tunazisafirisha na sisi kama Wawakilishi tunayo haja ya kujua ni bidhaa gani nyengine.

Kwa hivyo, hatuwezi kusema kitu kwa kuwafahamisha wananchi wetu ambao wametuchagua kuja katika Baraza hili, basi wajue ni biashara za aina gani, ili na wao wajue sasa namna gani vya kujipanga ikiwa na serikali ndiyo yenye jukumu hilo la kuwasaidia wakulima mbali mbali kama vile wakulima wakubwa na hasa wale wadogo.

Nikiondoka hapo sasa naomba niende ukurasa wa 9 kuhusu suala la Mwenendo wa Biashara wa mwaka 2007/2011 ametuonesha jaduweli lake ni hili hapa na ndio hiyo ambayo tayari nimeshaizungumza kwamba ni kujua ni bidhaa za aina gani, kwa sababu tumeona tu ni usafirishaji, uagiziaji na *amount* ambazo zimeandikwa hapo kwa mujibu wa miaka.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala la usafirishaji wa bidhaa kwenda na kutoka Tanzania Bara. Kwa kweli mimi inanipa *headache* kidogo sijui bidhaa hizi ni zipi, kwa sababu bado hatujakuwa na tukitoa karafuu na mwani hatujakuwa na biashara nyengine za kusafirisha ni bidhaa ambazo tunazipata kutoka nje, kama vile mchele.

Lakini inasikitisha baada ya kuingia hapa na pengine wafanyabiashara wanapata punguzo la ushuru, baadaye wanazitoa bidhaa hizi na kuzipeleka nje. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linasikitisha na lazima kama wizara basi ichukue juhudi maalum, kwa ajili ya kuweka mikakati.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba biashara ni kitu ambacho ni huru. Sasa wao wafanyabiashara wafanye na nimpongeze mfanyabiashara mmoja ambaye ni Bakharessa. Kwa mfano, ukitizama maeneo mengi ya Afrika anafanya biashara zake, tena anavyo viwanda vyake katika maeneo mbali mbali. Sasa na hawa wafanyabiashara wawe wakweli, wanaleta biashara Zanzibar wanapunguziwa ushuru na halafu biashara ile wanaipeleka kule.

Vile vile wao waone kwamba ni wazalendo wa nchi hii, hivyo ni lazima zile biashara wakipata wao watusaidie zaidi Zanzibar na kwa sababu hivi sasa naona kwamba Sekta hii ya Masula ya Biashara, kama serikali mambo ya uagiziaji kwa upande mwengine umepungua na zote wamewaachia wafanyabiashara na wala si jambo baya kwa lengo la kuisaidia serikali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kama serikali nayo ilitakiwa ichukue juhudi ya kuagizishia chakula na kikawa labda kwenye Maghala ya Akiba, ili pale linapotokea balaa lolote la ukame, hasa hivi sasa tukisema kwamba tuko katika haya mabadiliko ya tabia ya nchi na wala hatuna serikali kama serikali ikasema ina Maghala yake ya Akiba.

Kwa hivyo, niseme kwamba serikali bado ichukue juhudi hii, na hawa wafanyabiashara wanaochukua bidhaa kuingiza hapa na halafu wakazitoa ingawaje Mhe. Waziri amesema kwamba ameshirikiana na vyombo mbali mbali vya ulinzi.

Lakini hapa inazidisha tatizo kwa sababu hawa watu wa vyombo vya ulinzi na wao ni binadamu na wao kila siku matatizo mbali mbali tunayaona yanayojitokeza kwamba kuna kuwa na rushwa pale inaongezeka kwa sababu ya umasikini. Kwa maana hiyo, hapa kila siku tutajikuta kwamba wananchi wetu walio masikini zaidi wanadhalilika, kwa sababu hii nimepata taarifa kwamba SUMA pale anauza sukari tena kwa bei ya chini ya shilingi 1,400/= kwa kilo moja. Sasa yeye anao utaratibu gani na anapata wapi vitu hivi?

Kwa hiyo, ni lazima kwamba serikali iwabane hawa watu na wala si vibaya kufanya biashara pale unapoona unapata, isipokuwa wawe wakweli au serikali iwaandalie tena mwenye kutaka kutoa tena biashara basi awe analipa kiasi fulani, ili aweze kutoa, kwa sababu biashara ni kitu

cha uwazi na kitu cha haki. Mhe. Mwenyekiti, tunataka na wafanyabiashara wetu wapate, basi lazima wawe wakweli tena wawazi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kwa mchango huo kwa sababu wenzangu wameshachangia maeneo mbali mbali na kusema kwamba muda pia unatukwaza kwamba kesho tunataka tufanye majumuisho. Kwa hivyo, niseme kwamba naishia hapo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Sasa anayefuata ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Hemed Khamis na baadaye Mhe. Subeit Khamis Faki na tumalizie na Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Kwanza na mimi sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama mpaka kufikia hatua hii kuweza kuchangia hotuba hii. Pili nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameifafanua vizuri na kila mmoja ameifahamu.

Lakini baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaunga mkono hoja kabla sijamaliza hotuba yangu, ili nisije nikasau naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze na *Sunday Market*. Kwa kweli soko hili linahitaji kuimarishwa, kwa sababu soko hili watu wengi hutembelea pale na hata watu kutoka sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kuliimarisha soko hili na kutafutiwa sehemu ambayo ni nzuri kwa ajili ya kujenga majengo mapya au mazuri ya kuweza kuweka soko letu.

Pili nije katika Kiwanda cha Sukari. Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nilisikia kuna migogoro ya kiwanda hichi na kwa bahati na mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi hapo nyuma, nilishawahi kutembelea katika kiwanda kile, lakini kuhusu migogoro ya kiwanda hichi serikali haina budi kushughulikia migogoro inayotokea katika viwanda na wawekezaji kwa jumla, ili kuepuka wawekezaji na wananchi kutoelewana.

Vile vile serikali ina lengo la kumnyang'anya mwekezaji huyu. Lakini naomba kuuliza Mhe. Mwenyekiti kwamba serikali imejipanga vipi kutokana na mwekezaji huyu kwa kumnyang'anya kiwanda hichi.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningeomba kwamba mwekezaji huyu apewe muda wa kiasi cha mwaka mmoja, ili aweze kujiimarisha au aweze kutekeleza zile ahadi zake za pale, kwa sababu inaonesha dalili kwamba mwekezaji huyu hivi sasa tayari anaweza kukifufua hichi kiwanda kwa ajili ya kuendeleza shughuli zake pale.

Hata hivyo, serikali inahitaji kumsaidia mwekezaji huyu katika uvamizi wa mashamba yale.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije katika Shirika la *ZSTC*. Mhe. Mwenyekiti, mimi naliomba shirika hili lisisimamishe huduma zake za ununuzi wa karafuu, kwa sababu watu wetu wengi ni masikini ambao huweka fedha mkononi na kuzitumia haraka kuliko kuweka hakiba ya mazao yao nyumbani mwao, kwani wengi wanaweka mazao yao nyumbani.

Kwa mfano, karafuu inaweza kufika wakati mtu akawa hana cha kutumia, basi mtu yule hutoka na kwenda kuuza karafuu zake, kwa ajili ya kupata mahitaji yake pamoja na watoto wake, hususan kipindi hichi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, wapo ambao tuseme wanazo karafuu zao ndani na hivi sasa tayari wameshakwenda kuziuza, ili kusaidiana na watoto wake kwa ajili ya kupata Sikukuu kwa Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Kwa hivyo, naliomba shirika hili lisisimamishe huduma hizi, kwa sababu shirika ni duka, ambalo watu wengi huenda kuuza mazao yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nije katika Shirika la Magari. Kwa kweli mwenzangu Mhe. Asha Bakari Makame amesema shirika hili lifutwe. Lakini pamoja na kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi, shirika hili Mhe. Mwenyekiti mimi nisingesema lifutwe wakati shirika hili linakwenda kwa faida na wala haliendi kwa hasara.

Pia Shirika hili linalipa kodi na wala halitegemei ruzuku za serikali, wakati ambapo yapo mashirika mengine hayatoi kodi na bado Mhe. Mwenyekiti hayajafungiwa, kwa nini Shirika hili la Serikali lifungiwe, kwa nini serikali isitumie shirika hili wakati kila siku serikali inanunua vyombo vya moto na kuweza kulipa shirika hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uangukaji mikarafuu na hapa kidogo naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kwamba amewategemeza vipi waangukaji wa mikarafuu, ili kwa kuwalipa waangukaji wale wa mikarafuu.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu wafanyabiashara wa Jua Kali. Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara wa Jua Kali ni watoto wetu pamoja na ndugu zetu ambao wote pale wamejiajiri, hasa vile kwa serikali haina ajira, lakini watoto wetu pale wamejiajiri kwa kuweza kufanya biashara zao na kuweza kuendeleza huduma zao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awapunguzie kodi wafanyabiashara wale hususan wa Jua Kali na Pindamgongo, kwa sababu kama unavyojua wanaweza kukaa pale kutwa nzima baadhi wakauza na wengine hawauzi na ikifika mwisho wa mwezi mtu kama yule anataka alipe kodi. Mhe Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri awapunguzie kodi wafanyabiashara wetu, ili waweze kujiendeleza vizuri.

Sasa naomba nije kwenye ukurasa wa 55.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Sasa naomba nije kwenye ukurasa wa 54 na Mhe. Waziri alisema kwamba kuna bidhaa hizi ambazo zimeangamizwa, kufanya ukaguzi wa mizani, halafu kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta.

Lakini kwanza naomba nianze na hii ya kuangamiza bidhaa zilizomalizika muda wake na zisizofaa kwa muda wa matumizi ya binadamu. Hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri ni bidhaa ngapi ambazo zimegundulikana kupitiwa na muda wake? Bidhaa ngapi na zipi ambazo zimeangamizwa na wizara imechukua hatua gani, ili kuwadhibiti watu kama hao?

Jambo jengine ni kuhusu kufanya ukaguzi wa mizani. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri ni mizani ngapi ambazo zimegundulikana hazina usahihi wa vipimo vyake na serikali imechukua hatua gani?

Mwisho kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri ni sheli ngapi ambazo zimefanyiwa ukaguzi na kuonekana kuwa hazina matatizo ya mafuta, kwa sababu kuna sheli nyengine watu wengi huwa wanazikimbia kutokana na matatizo ya mafuta. Je, nimuulize Mhe. Waziri ni sheli ngapi ambazo wamefanya utafiti wa mafuta?

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Sasa anayefuata ni Mhe. Suleiman Hemed Khamis jitahidi usirejee mada na zingatia wakati na baadaye Mhe. Subeit Khamis Faki na mwisho Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kuweza kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba Zanzibar ni mjumuisho wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba. Lakini Mwenyezi Mungu ametujaalia kwamba ametupa bahati katika bahari yetu iliyotuzunguka katika visiwa vyetu hivi viwili kwa kuweza kupata rasilimali ndani yake, na rasilimali nyingi sana zinapatikana katika bahari. Katika kuzitafuta zile rasilimali nyengine tunazipata lakini kwa kiwango kidogo sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tuseme tu kwamba bahari ni tajiri sana na ina rasilimali nyingi ndani yake ambazo zinaweza kupatikana mambo ya johari, mafuta, gesi asilia, wanaweza kupatikana chaza ambapo ndani yake inaweza kupatikana lulu, madondo, *gunda fish*, vibenza pamoja na mwani. Kwa kweli hizi ni rasilimali ambazo tayari zimo katika bahari ingawa ugunduzi wake unakwenda kidogo kidogo. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo kitu ambacho kinajitokeza nimwambie Mhe. Waziri katika rasilimali ya bahari ni mwani, ambao ndio uliochukua namba. Vile vile nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba wanawake wanastahiki kupewa kipaumbele, kwamba wanawake katika visiwa viwili hivi ndio wanaozalisha mwani kwa wingi kabisa.

Kwa hivyo, hii biashara ya mwani ndio inayotupa mwelekeo wa maendeleo yetu ya uchumi katika nchi yetu, wao ni watendaji na ni wanawake wanaopoteza muda wao mwingi sana katika bahari kwa ajili ya uzalishaji wa mwani. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri awashughulikie sana hawa wanawake na awape kipaumbele kutokana na juhudi na bidii ya kuitanguliza biashara hii ya mwani.

Kwa kweli hii inaelekea kama ni sehemu ya ajira kwa wanawake, ambapo wanawake hapa wanafaidika katika zao hili na wanapata mapato ya kila mmoja, pia ni sehemu ya uchumi na nchi inafaidika katika uchumi huu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba wanawake katika jitihada zao wameweza kuzalisha kwa wingi kabisa mwani, lakini utaona pia imepita hata bei ya tani ya karafuu inayozalishwa ndani ya Zanzibar. Utaona mwani uko mbele ambao unaweza kuzalisha hata tani 10 mpaka 12 za mwani ukilinganisha na tani 4,000 za karafuu. Kwa hivyo, ni stahili yao washughulikiwe kama wanavyoshughulikiwa wengine wapewe vipaumbele na iangaliwe kwamba usafirishaji unaelekea utakuwa mzuri baadaye siku za mbele.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba hawa wanawake awasaidie katika kupata elimu ya ukaushaji wa huu mwani wao. Vile vile kwa sababu uzalishaji wao unaonesha unakuwa ni duni sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aweze kuwashughulikia ili liwe zao bora na linaweza kupata soko.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ukaushaji wa mwani, wanahitaji kupata elimu ya kutosha na pia zao lenyewe lina tabu kulishughulikia na bei zao ziko chini. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri aangalie gharama za uzalishaji wa zao la mwani pamoja na usafirishaji wa zao hilo.

Vile vile tuangalie tunaozalisha tunazalisha malighafi, na hii ndio tunayoiuza, kwa sababu ni kawaida yetu wazanzibari tunapozalisha malighafi tunauza. Kwa mfano, hapa Zanzibar tunazo karafuu kwa wingi, pia tunauza malighafi, yaani mpaka leo tumeshindwa kuisarifu tukaweza kutoa; ambapo karafuu ile tukiiuza kwa wenzetu wanazalisha na tunanunua mazao yao kwa njia ya *dollars* fedha nyingi sana.

Sasa na hapa tunazalisha mwani kwa wingi lakini tunauza malighafi je, unaonaje Mhe. Waziri kutokana na mwani huu, ambao unaozalishwa na wananchi wetu ukaweza kupata bei ya soko iliyokuwa kubwa, kwamba kwa kuanzia tunauza malighafi, lakini baadaye tuwe na mbinu na njia ya kuweza kuzalisha hii malighafi bidhaa nyengine. Kwa mfano, kama tunavyozalisha karafuu kwa kutoa mafuta na mwani kwa kuweza kuzalisha na kuweza kutoa bidhaa nyengine kwa zao la mwani.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili hapa. Je, kuna hatua zozote zile zilizochukuliwa katika mfumo wa gharama (*costal structural*) kwa uzalishaji na usafirishaji wa zao la mwani? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili ambalo napenda nimuulize Mhe. Waziri ni mafanikio gani ambayo yamepatikana baada ya kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Viwanda la Umoja wa Mataifa *UNIDO* katika kuongeza thamani ya uzalishaji wa mwani? Haya maswali yangu mawili.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye sehemu ya pili kuhusu Shirika la MTC. Kwa kweli shirika hili tulikuwa nalo muda mrefu, ambalo lilikuwa *Motor Trade Corporation*, ambapo biashara yake ilikuwa ni magari pamoja na vespa. Mhe. Mwenyekiti, muda mrefu biashara hii imekufa na hii inaonesha kwamba mtaji wao ni mdogo, na kutokana na *competition* iliopo Zanzibar Shirika la *MTC* haliwezi kuingia ndani ya vita vilivyopo vya biashara hii ya magari.

Mhe. Waziri nafikiri unaelewa kwamba hivi sasa *Show rooms* kwa hapa Zanzibar zipo kwa wingi, yaani kila *conner* ya Zanzibar kuna *Showroom*, yaani aina mbali mbali za magari pamoja

na vespa zimejaa tele. Kwa hivyo, kwa muda mrefu hivi sasa hili shirika linakuwa linaitia hasara serikali. Kwa maana hiyo, mimi ningeliona Mhe. Waziri kuanzia bajeti ya mwaka jana ambapo ulisema utalifunga shirika hili na bado hatua hii haijajulikana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizokwamisha kwamba hili shirika linaendelea kuishi bila ya mpangilio wowote, yaani halina maendeleo yoyote kwamba halizalishi, watu wamekaa na wala hawajui nini cha kufanya.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, awape maamuzi moja wapo, na ijulikane na huko kushindwa kwao wameshindwa na kitu gani, kwa sababu wao inavyoonesha kinadharia kwamba ushindani wa biashara umewashinda. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeweza kusema labda pengine umewashinda kwa sababu uwezo mdogo wa kifedha, kwa nini wizara hii inashindwa kuchukua hatua mpaka hivi sasa kutokana na hayo ambayo tayari nimeshayaeleza.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu zao la karafuu na hii ni *national crop* ya *Zanzibar*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wananchi wamefaidika kwa muda mrefu, lakini utaona kufaidika kwao bado wao wenyewe alitaka suala hili la zao la karafuu waweze kubinafsishiwa, lakini imeshindikana kubinafsishwa na imeonekana ni kama zao la kitaifa. Kwa kweli Zanzibar ilikuwa inategemea uchumi wake kutokana na zao la karafuu, baada ya kuanguka zao la karafuu ikaingia katika suala la utalii, ndio sasa inategemea utalii, yaani biashara ya utalii.

Hata hivyo hivi sasa kwa sababu ya kupewa wananchi muamko fedha za kutosha katika kuzalisha, kwa hiyo yameonekana maendeleo na bado Shirika hili la *ZSTC* linaendelea kuwa na zao hili la karafuu. Lakini mimi naomba kusema Mhe. Waziri kwamba zao hili la karafuu ambalo liko chini ya dhamana ya *ZSTC* huoni kwamba hawa ni watu wawili wako pamoja *ZSTC* pamoja na wakulima wako bega kwa bega, kwa nini basi yale wakulima wanayoyataka hawapewi.

Kwa mfano, inafika wakati wa kutaka kusafisha mashamba yao basi waweze kupewa mikopo ya kuweza kufanya usafi wa mashamba yao, kwa sababu zao hili linasaidia.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, tulizungumza hapa kwamba zao hili la karafuu linataka lifanyiwe *branding,* na tulizungumza kipindi kilichopita na imeshindikana kufanya *branding* na unajua tukikosa kufanya *branding* tukalitambulisha kwa mataifa yote kwamba tunalo suala hili, basi suala lile na kufanya biashara ya magendo inaweza kuendelea na kila mtu anaweza kuwa tajiri wa karafuu zetu.

Kwa mfano, Kenya ilijifanya yeye ana mamlaka ya kuuza karafuu, wakati karafuu Kenya hana na karafuu ziko Zanzibar. Lakini kwa sababu sisi hatuna *branding* ya karafuu zetu ina maana kila mtu atakuwa ni bwana mkubwa na atakuwa yeye ni bosi wa karafuu zetu. Kwa hivyo,

namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, achukue hatua za haraka, ili *branding* ya karafuu zetu iweze kusaidia na uuzaji kiholela wa karafuu upotee.

Jambo la mwisho ambalo namalizia Mhe. Mwenyekiti, *the last thing I want to talk.*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tuzingatie muda na wengine wawahi.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Sekta ya Viwanda Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu hapa tulikuwa na Sekta ya Viwanda. Sekta ambayo iliyokuwa inatuendesha hapa Zanzibar, yaani sekta ambayo tulikuwa tunaendeshwa kwa vizuri kabisa. Kwa mfano, tulikuwa na Kiwanda cha Sabuni, Kiwanda cha Sukari, Kiwanda cha Maziwa, Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha *Juice*, Kiwanda cha Sigara pamoja na mambo mengi tu.

Vile vile vimeingia Viwanda vyengine Vidogo Vidogo kama vile uzalishaji wa mafuta, matunda, sabuni kwa kiwango kidogo, soda. Kwa kweli hali hii inaonesha uzalishaji uko dhaifu kidogo, ingawa hii ni ajira na inawasaidia watu kuweza kupata kazi. Lakini sasa tuone kwamba viwanda vyetu vya ndani uzalishaji wake ni mdogo sana na wala hauwezi kufanikisha maendeleo makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunategemea katika Sekta hii ya Viwanda tungetegemea tuwapate wawekezaji, ambao wataweza kutusaidia katika Sekta hii ya Viwanda, watakapokuja hawa na ikiwa njia zipo safi, maeneo yetu ambayo ni huru yako safi kabisa katika masuala matatu, maji, barabara na umeme ni kitu cha uhakika tunakipata.

Kwa maana hiyo, naamini uzalishaji utakaofanywa katika viwanda vikubwa na *Industrial Revolution* unaelewa sawa sawa Mhe. Mwenyekiti, imewapa watu maendeleo na sisi kwa nini tukose mambo ya uzalishaji wa viwanda. Kwa mfano, tunaona Japan kitu kinachowasaidia ni viwanda vidogo vidogo pamoja na vile vikubwa.

Lakini sisi Zanzibar mpaka leo hivi sasa hatujawa na msimamo wa viwanda vya aina yoyote na wala hatuwezi tukajisifu kwamba Zanzibar kama tunavyo viwanda, kwa sababu viwanda vilivyopo bado ni *very small scale* ya viwanda vyetu na uzalishaji wao ni mdogo. Kwa hivyo, kwa jitihada zako tukuombe basi utusaidie angalau wawekezaji waje waweze kuwekeza Zanzibar kwenye viwanda vikubwa vikubwa na sisi tuweze kuzalisha badala ya kuagiza mambo kutoka nje, tuone malighafi tunaweza kuipata.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa watu wetu wa ndani katika viwanda vyetu vya ndani wanashindwa kuzalisha kutokana na kukosa malighafi. Kwa hiyo, tukipata wawekezaji wataweza kuleta malighafi na bila ya shaka viwanda vitaendelea na uchumi utapatikana na wananchi watafaidika kwa ajira na nchi itafaidika kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Sasa anayefuatia ni Mhe. Subeit Khamis Faki kwa kuzingatia muda na baadaye Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niseme maneno machache kabisa kuhusu hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu biashara hii ya zao la karafuu. Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kutokana na zao hili la karafuu kwa kuwaongezea bei wananchi wetu na wakafaidika. Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kutokana na suala hili pamoja na kufaidika na nyongeza hii ya bei lakini hivi karibuni kuna watu walikuwa wanapiga kelele kutokana na kwamba ununuzi wa karafuu walikuwa wameufunga.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kutokana na kipindi tunachoingia hichi cha Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani na hasa ukizingatia kwamba watu wanategemea sana Sikukuu, basi nimuombe kwamba waboreshe yale maduka au sehemu za kununulia karafuu ziboreshwe, ili wananchi waondokane na kupata dhiki na hasa ukiangalia kwamba ni kipindi cha kujipatia Sikukuu wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kukuza hii biashara nimuombe Mhe. Waziri aangalie kama biashara ya zao la mwani ni zao moja ambalo limepata changamoto kubwa ya wananchi wetu kuliitikia. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kama upo uwezekano basi kwa nini hili Shirika la *ZSTC* wasiwe wanunuzi wa zao la mwani, kwa sababu wao wakiwa wanunuzi wanaweza kuboresha soko na kuangalia zaidi utafutaji wa soko, ili wananchi wetu waweze kufaidika, kwa sababu zao hili limeitikiwa na wananchi kwa wingi sana, yaani Unguja na Pemba linazalishwa kwa wingi.

Kwa maana hiyo, ili wananchi wetu wafaidike, basi namshauri Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aangalie uwezekano Shirika la *ZSTC* waone kama kuna haja ya kununua kwa sababu watawakuzia zaidi wananchi wetu bei, kwa sababu kutakuwa na ushindani wa ununuzi na wananchi wetu watapata faida zaidi. Kwa hiyo, namshauri Mhe. Waziri angaalie zaidi kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo nataka nizungumze Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita hapa tulizungumza sana kuhusu suala la hili la biashara ya mchele pamoja na biashara nyengine muhimu kwa jinsi zilivyokuwa zimepanda bei kwa haraka, ingawaje hivi sasa kidogo ule upandaji wa mara kwa mara umepungua kidogo.

Lakini tulimuomba Mhe. Waziri kwamba serikali inakuwa ni wasaidizi wa wananchi, kwa maana hiyo tulitaka kama wawe na Ghala za Akiba kwa ajili ya kuweka akiba pale inapokuwa biashara hii imepanda zaidi basi vile vyakula vilivyomo kwenye maghala ya vyakula kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, kwa sababu siku zote serikali ndio inakuwa kiunganishi cha kuwasaidia wananchi.

Kwa hiyo, nilitaka Mhe. Waziri wakati atakapokuja anieleze, kwa sababu suala hili tayari tumeshalizungumza tokea bajeti iliyopita na tulipiga kelele sana, hivyo anieleze kwamba je sasa wamefikia hatua gani kuhusu suala hili la ujengaji wa maghala ya akiba kwa ajili ya wananchi wetu. Hilo ni swali moja.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nizungumze kuhusiana na maeneo huru. Kwa kweli suala hili tumeshalizungumza sana na tumeshapiga kelele sana na Mhe. Hamza Hassan Juma amelizungumza, na mimi kila bajeti inayokuja nazungumza, kwamba tumetenga maeneo ambayo ni maeneo huru ya uwekezaji.

Lakini mara nyingi mimi huwa ninasema kwamba sadaka siku sote huanzia nyumbani, yaani unaanza kutoa sadaka wewe nyumbani mwako, ili na wengine wakija watoe sadaka, sasa leo nyumbani hujatoa sadaka na unakwenda kutoa kule mbeleni, haiwezekani lazima sadaka ianze pale nyumbani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kila mara nazungumza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lazima itoe hiyo sadaka kwanza ndio waombe serikali nyengine kwa ajili ya kuja kutoa sadaka. Kwa maana hiyo, ni sawa na kusema kila siku nasema uwekezaji serikali ianze kuwekeza yenyewe katika yale maeneo huru, ili na wawekezaji wengine wafuate, lakini serikali au mwekezaji yeyote wa nchi nyengine atakapopelekwa akifika kule ni machaka tu na wala hawezi kuwekeza. Hivyo ianze kuwekeza serikali yetu kwanza, hebu serikali ijitutumue iende kuwekeza na baadaye hawa wengine wafuatie.

Sasa mwekezaji akija hakuna maji kama anavyosema Mhe. Mjumbe mmoja hapa kwamba hakuna barabara wala umeme, yaani hakuna kitu chochote cha kuwekeza ni mapori tu watawekeza vipi, na wala hawezi kustahamili mwekezaji akakubali na kwenda kuwekeza.

Kwa hivyo, serikali ni vyema ikaanza yenyewe kwanza na itoe sadaka hiyo kwanza na halafu wengine ndio wafuatie, kwa sababu bila ya kuwekeza hiyo kwanza hawezi kwenda mtu na kuwekeza. Hilo ni suala jengine.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nizungumze ni kuhusu suala hili la biashara na viwanda. Nadhani ni kusema kwamba kwa sababu kila mukija munatuambia kuwa Zanzibar kuna viwanda vingi. Lakini viwanda vyenyewe vinavyoonekana ni viwanda vipi, hivi mtu anatengeneza mchi mmoja wa sabuni ndio mnakiita kiwanda, mtu mmoja anakamua mafuta ya nazi kwa chicha zile lakini ni kiwanda chake mwenyewe ndio mnakiita kiwanda na wala hivyo sivyo viwanda tunavyovitaka sisi Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunataka viwanda tuone kama kuna viwanda Zanzibar vya kuzalisha pamoja na kusafirisha bidhaa katika nchi nyengine, lakini leo kuna kiwanda mtu anatengeneza mchi wa sabuni anakuja kumuuzia Mhe. Ismail Jussa Ladhu mchi mmoja mnasema ni kiwanda na wala hicho si kiwanda. Vile vile kuna bekari mtu anazalisha mkate mmoja wa kumpa Mhe. Abdalla kwa ajili ya kula tunasema ni kiwanda na wala hivi havijawa ni viwanda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama serikali imekusudia kukuza viwanda Zanzibar, basi hebu tuwekeni na mufanye tuone kama kweli viwanda angalau viweze kubeba wananchi wetu waweze kupata ajira angalau 100, yaani kila kiwanda kiweze kuajiri wananchi 100 au 50. Lakini kiwanda cha kufanya mche mmoja wa sabuni si viwanda hivyo muheshimiwa.

Pili ninalotaka nilizungumze ni suala la kiwanda kilichopo Mahonda. Hivi kiwanda kile cha Mahonda kinatoa faida gani kwa wanachi wa Zanzibar. Hivi kwa nini yale mabonde wasipewe wananchi wanakalima mipunga. Kwa sababu kile kiwanda hakina faida kwa wananchi wa Zanzibar, kipo kipo tu. Huyo muwekezaji aliyepewa hatuoni anachokifanya.

Mheshimiwa je, yale mabonde yetu ya mipunga si bora tukazalisha mipunga watu wakala au wananchi wetu wakala na watoto wao, kuliko kujiwacha tunasema tuna kiwanda kipo lakini hatuoni faida inayozalisha. Mheshimiwa naomba kama tumekusudia kuboresha viwanda basi tuboresheni viwanda ili wananchi wetu tuone kama sasa hivi tunatoa mazao.

Tukiboresha viwanda tutatoa mazao na tutasafirisha baada ya karafuu tutakuwa tuna biashara nyengine za kusafirisha nje. Lakini siku zote sisi tunavyonunua kutoka nje ni nyingi zaidi kuliko tunavyosafirisha. Kwa hivyo kama tutaweka viwanda tutasafirisha na tunavyo vitu vya kufanya hivyo hivyo vidogo vidogo vilivyokuwepo. Maana kama kuna pilipili kama anavyosema Mhe. Mussa kama kuna pilipili zinazalishwa halafu kuna kiwanda zinasindikwa, zinaweza zikauzwa na ikawa ni biashara nzuri nje.

Halafu pia juice za matunda zinaweza zikatengenezwa zikasafirishwa nje tukapata biashara nyengine. Kuna wakati watu wanakuwa wanazalisha mananasi kuna msimu yanakuwa yapo kwa wingi hapa Zanzibar, yale yanaweza yakakamuliwa tukauza juice nje. Kwa hivyo tunakuwa tunakuza biashara ya kuuza nje. Kuliko sisi tunaagizia tu kila kitu lakini sisi hatusafirishi. Inakuwa pesa zetu zote tunazitoa kwa kuagizia nje kuliko kuzunguka hapa hapa petu.

Kitu chengine ambacho nataka nikizungumze ni kwamba tuige kutokana na wenzetu, tuwe na uchoyo ya kuiga kwa wenzetu. Wezetu kilimo wameweka Benki ya Kilimo, wanazalisha watu wa kilimo wanakwenda wakichukua Benki wakikopa. Kwa nini wakasi na sisi tuna zao kubwa hili la karafuu tusiweke Benki ikawa ya watu wa karafuu tu wanakopa, wanaweka, zile fedha zetu zitakuwa zinazunguka hapa hapa. Kwa nini hatuweki Beki ikawa benki hii ni Benki ya Kilimo lakini hasa zao la karafuu. Watu ikawa wanaweka pesa zao, wanakopa pesa zao.

Wenzetu wana Benki za Kilimo, wana CRB na nyenginezo. Na sisi tukuzeni benki zetu ziwe nyingi baada ya Benki ya Watu wa Zanzibar, tuwe na benki nyengine ya Watu wa Zanzibar lakini inayohusu mambo ya karafuu. Wataweka pale pesa zao, watakopa na ninavyojua mimi zao la karafuu likizaliwa tu, basi inakuwa Wananchi wa Zanzibar wanakula karafuu. Mwenye mtoto wake anataka skuku anamnunulia kwa zao la karafuu ingawa hazijachumwa karafuu lakini anaanza kukopa kwa ajili ya lile zao la karafuu. Watu walikuwa wanakopeshwa pesa, wanakopeshwa majamvi, wanakopeshwa kila kitu. Naomba kama na hili ulizingatie tuone litaletea faida kwa wananchi. Mhe. Waziri wa Fedha, yupo pale anasikia kwamba tuanzishe Benki ya kilimo kwa ajili ya wakulima wa karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (SWA) aliyenijaalia uhai, uzima, tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na kumshukuru au kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mfupi mno nianze na ukurasa wa 48 unaogusa hali ya viwanda Zanzibar.
Mhe. Mwenyekiti, mjumbe aliyekaa aliigusa hasa mada ambayo ndiyo ambayo iliyonifanya nisimame na kuomba kuchangia. Nadhani historia inatukumbusha Zanzibar viwanda inawezekana kwa sababu tulikuwa tunavyo, viwanda vya sukari, viatu, maziwa na hivyo vyote vilikuwa vikijiendesha na hapakuwa na hasara. Nidhahiri kwamba endapo tutalizingatia na kulipa kipaumbele ni jambo ambalo linawezekana kabisa. Lakini nadhani kwamba bado hatujaamua kweli tunahitaji viwanda?

Sababu tumesema tunahitaji kuboresha viwanda vyetu. Katika kitabu chake Mhe. Waziri anasema anataka kuifanya Zanzibar iwe eneo tengefu la kiuchumi. Hivyo tujiulize hayo maeneo ambayo tumeyatenga na sisi tunasema kwamba bado hatujayawekeza miundombinu ambayo itarahisisha kumfanya muwekezaji avutiwe na aingiwe na hamu kwa ajili ya kuwekeza. Maeneo hayo hayana umeme, hakuna barabara, hakuna maji. Je tupo tayari?
Nasema kwamba hatujawa tayari. Kama tumeamua kuwa tayari serikali ni lazima iliangalie hilo kwa kina kuweza kuweka miundombinu hiyo ambayo inaweza kuleta mabadiliko ya kweli ya kuweza kuleta viwanda ambavyo vitatoa ajira ya kweli kwa Wazanzibari. Shida yetu ni ajira, vijana wetu wengi wanazubaa zubaa bila ya kukosa kazi za msingi na hatimaye kutumbukia katika makundi mabaya. Tukiumiza fedha zetu nyingi kuona kwamba wanaangamia katika madawa ya kulevya. Hili linatokana na kwamba vijana wetu hawana kazi.

Naamini kwamba vijana hao kama sekta hii tutaiboresha vyema ya viwanda ina uwezo mkubwa wa kuwaajiri vijana wengi na vijana wetu wengi wakawa wanaweza kujikomboa kiuchumi na kuachana na mambo mabaya ambayo kwa sasa tumejipangia wizara maalum ya kushughulika na vijana wa madawa ya kulevya, jambo ambalo tukiacha hilo inawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, nia yangu kuu nilikuwa nagusia hasa zaidi kuhusu Kiwanda cha Sukari Mahonda. Kiwanda hichi amepewa muwekezaji nao ni muda mrefu sasa. Kiwanda hichi hakizalishi chochote kinazalisha pombe. Hilo sio lengo letu. Kiwanda hichi kinazalisha pombe, wanaofanya kazi katika kiwanda kile ni wachache mno tena maeneo yetu makubwa ambayo Wazanzibari ndugu zetu wananchi wetu wanyonge walikuwa wakiyatumia katika sekta ya kilimo maeneo hayo sasa yamekaa bure tu.

Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati Mhe. Waziri nakuomba utakapokuja hapa uneeleze kwa kina nikuelewe, vipi muwekezaji huyu anaewaondoshea utaratibu mzima wa maisha yao watu wa Mkoa wa Kaskazini, ambao kwa miaka ya nyuma kiwanda kilifanyakazi kiliwaajiri watu wengi mno. Wananchi wamefika kupelekwa katika Mahakama kwa kushtakiwa kwa eneo hilo ambalo amepewa muwekezaji. Hili ni tatizo.

Muwekezaji huyu ameleta matatizo makubwa, ameleta usumbufu, nina uhakika, nina ushahidi, alijaribu kutoa baadhi ya maploti wakapewa wananchi wakatumia kidogo. Hayo ambayo wametumia na hali bado njaa na shida wanazo, walipoyaona matupu walijaribu kulima. Ikatokea patashika nguo chanika, wananchi hao wakawekwa sehemu za vizuwizi, jeshi la polisi likatumwa. Hawa ni Wazanzibari, wana haki na wao ndio wenyewe. Hayo manufaa kwa muwekezaji wetu yako wapi?

Nakuomba Mhe. Waziri, unieleze kwa kina Wazanzibari wa Kaskazini wanasubiri kwa hamu jibu lako. Kwa sababu wana hamu ya kulima lakini eneo la kulima hawana, maeneo yote ambayo amepewa muwekezaji ndio maeneo hasa waliyokuwa wakitumia kwa shughuli za kilimo, imekuwa yanaleta hasama baina ya wananchi na viongozi wao. Nadhani toleo lilitoka, hali ya mzozo ilitoka katika vyombo vya habari. Namuomba Mheshimiwa hili unipe maelezo ya kina.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika ukurasa wa 38 inagusa kwenye hii sehemu ya biashara. Niseme ukweli Zanzibar ni visiwa kwa kuwa Zanzibar ni visiwa havina ardhi ya kutosha kwa ajili ya kufanya shughuli zake hasa za kilimo ikawa zinakidhi haja ya uchumi wa Wazanzibari. Kihistoria Zanzibar ni kitovu cha biashara. Wanaokumbuka historia Zanzibar ilikuwa ipo katika mfumo wa biashara.

Ipo haja sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kukaa na wafanyabiashara. Ni lazima akae nao na serikali ifikirie hasa kuweza kubadilisha haiba ya Zanzibar taswira yake ibadilike katika mji wa Zanzibar ili tuone kwamba tunamudu kufanya biashara hiyo kweli. Maduka yaliyokuwepo katika Mji wa Zanzibar ambayo ni taswira tosha ya kuonesha mji wetu kwa kweli hayana hadhi ya kuitwa maduka ya ushindani wa kibiashara na kusama hasa tunataka kuingia katika sekta ya kibiashara.

Nidhahiri kwamba kaa nao mimi naamini wafanyabiashara wana uwezo mkubwa na wana utamaduni mkubwa. Tubadilishe hali tuweze kujenga maduka ya ghorofa ili tuweze kuleta ushindani hasa wa kibiashara. Wafanyabiashara wakubwa watapata nafasi hiyo na wataingia katika ushindani huo, lakini na wale wadogo neema hiyo itawafikia na nuru ya Zanzibar itakunjuka katika utaratibu mzima wa shughuli za kibiashara. Huo ndio utaratibu.

Vyenginevyo tukiwa tumezowea kutoa leseni na kukusanya habari hizi kwa ajili ya kupata pato la taifa kupitia kodi nadhani hatutofika twendapo na siku zote tutakuwa tunazungumzia biashara. Lakini naamini kwamba kama utawatumia vizuri wafanyabiashara wa Wazanzibar ambao wengi wao ni waungwana na wao ni Wazanzibari, wana lengo zuri na naamini wana uwezo mzuri. Kaa nao Mhe. Waziri, uzungumze nao na baadaye utubadilishie taswira ya Zanzibar ili kuijenga hamu na kuwajenga hamu wageni wetu ambao wanaingia Zanzibar, waweze kuwekeza na wao katika mambo mbali mbali wikipitia katika shughuli za kibiashara katika mji wetu kitaswira.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda wako umekwisha naomba niseme kwamba nitaunga mkono hoja hiyo baada ya kupata majibu ya kutosha kuhusu kiwanda cha sukari kwa hivyo naomba kukaa kitako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe uliyemalizia. Waheshimiwa Wajumbe Bajeti hii ya leo ilibahatika kuchangiwa au kuombwa kuchangiwa na wachangiaji 17 waliobahatika kuchangia ni 16 tumebakiwa na mchangiaji mmoja ambaye atakuwa ni Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Dokta Mwinyi Haji Makame, ambaye atakuja kumalizia kesho asubuhi tukijaaliwa. Baadaye tutamkaribisha Mhe. Waziri ili aweze kufanya majumuisho katika bajeti hii.
Baada ya maelekezo hayo nichukue fursa hii kutamka kwamba tunaakhirisha kikao hadi kesho tarehe 7/08/2012 siku ya Jumaane saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:00 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 7/08/2012 Saa 3:00 za asubuhi)